Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Ishirini na Sita - Tarehe 11 Julai, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

### HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010**
**Wizara ya Maliasili na Utalii**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza nitoe taarifa tu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amesafiri leo asubuhi kwenda Shinyanga kwa shughuli za kikazi na amemwachia kuongoza shughuli za Serikali Mheshimiwa John Z. Chiligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. (*Makofi*)

Kama kawaida upande wa upinzani, namwomba Mheshimiwa Masoud bado mambo yanamnyookea tu anaendelea tu na kwa hiyo nampongeza sana. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, orodha niliyonayo hapa sasa kuna wachangiaji watano na ninadhani wote watapata nafasi kwa sababu tunao muda na ninaomba niwataje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto na hatimaye Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia.

Kwa sasa tutaanza na Mheshimiwa Damas Paschal Nakei, atakayefuata ni Mheshimiwa Lwanji na ajiandaye Mheshimiwa Kigwalilo.

**MHE. DAMAS PASCHAL NAKEI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru tu asubuhi hii kwa kuwa mchangiaji wa kwanza kabisa katika hoja hii ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa hotuba nzuri ambayo imeandaliwa vizuri lakini vilevile nimshukuru Waziri na timu yake yote katika Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya na kuwatumikia Watanzania vizuri.

Vilevile nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati ya Maliasili, Utalii na Mazingira kwa kazi nzuri vilevike wanayoifanya kwa kushirikiana na Wizara hii lakini pia niwashukuru kwa namna ya pekee Kamati hii ikiongozwa na Mheshimiwa Job Y. Ndugai kwa kufika Babati Jimboni kwangu mwezi Januari mwaka huu na kufanya kazi nzuri na ninasema karibuni tena Babati na mjisikie nyumbani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kama tunavyofahamu ni tajiri imejaliwa utajiri mkubwa lakini jambo la kusikitisha ni kwamba utajiri huu tunashindwa kuutumia, tunashindwa kuutunza na kwa hiyo tunashindwa kujinasua katika makucha ya umaskini kutokana na hali hiyo ya kutoutumia vizuri utajiri wetu. *(Makofi)*

Labda niseme tu kwamba tuna kazi kubwa mbele yetu ya kutumia raslimali ambazo Mwenyezi Mungu ametujalia.

Mheshimiwa Spika, tangu jana Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamekuwa wakielezea utajiri wa utalii tulionao katika nchi hii. Utalii wa utamaduni, ikolojia au *eco tourism* na kadhalika.

Sasa mimi pia nikijaribu kuona utajiri huo katika utalii ningependa tu nianzie humuhumu Bungeni kwa kusema kwamba Historia ya Nchi yetu Bunge ni utajiri au ni Utalii tosha kama tukiitumia fursa hii vizuri. Wageni wengi huja hapa Bungeni wageni kutoka ndani na nje ya nchi kuja kuangalia Bunge letu linavyofanya kazi.

Lakini nadhali hawaji hapa kuja kuangalia jinsi tunavyokaa humu ndani isipokuwa ingekuwa vizuri zaidi kama tungeweza kutumia fursa hii ya kuelezea historia ya Bunge letu. Mimi naamini kabisa Bunge hili lingeweza kuwa mojawapo ya *tourist attractions* katika nchi hii kama mazingira mazuri yakiandaliwa. Kwa mfano ikiandaliwa historia nzuri ya Bunge letu tangu Bunge la ukoloni, Bunge la nchi huru yaani tangu tulipopata uhuru wetu lakini vilevile mabadiliko ambayo Bunge letu lime *undergo* katika historia yake.

Sasa hivi ingekuwa ni vizuri vilevile kufahamu kwamba Bunge letu limekuwa likifanya kazi yake vipi, Maspika wake yaani tangu Spika wa kwanza hadi Spika wa sasa yote haya ni historia ambayo watalii wangeweza kuja kujifunza hapa. Kwa hiyo, ningeshauri Ofisi ya Bunge kuhakikisha kwamba mazingira yanaandaliwa ili ikishirikiana na Wizara hii ya Maliasili na Utalii iweze kufanya Dodoma na Bunge letu hili likawa ni mojawapo ya kivutio cha watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba na labda nizungumze habari ya mapori ya akiba. Katika kitabu hiki cha Bajeti cha mwaka huu na hata cha mwaka jana sikuweza kuona juu ya msitu wa akiba au msitu wa hifadhi wa Nowu ambao uko katika Wilaya ya Babati na niseme msitu huu tunauita *NOWU Reserve Forest wenye* hekta 13,000 ni msitu ambao kwa kweli ni mzuri sana kwa utalii na hasa kwa *nature* yake kwa jinsi ulivyo. Ningependa tu kusema kwamba ni watalii wachache ambao mara nyingi wanafika pale kufanya *camping* na kadhalika katika suala zima la kufuatilia nature ya msitu ule. Lakini mara nyingi wanashindwa kufika katika mazingira yale kwa sababu ya miundombinu ambayo ni hafifu yaani miundombinu ya barabara. Kwa hiyo, ninapenda kuishauri au kuomba Serikali kujenga au kuiboresha barabara ya kutoka Merr, Endelaha hadi Madunga ili kuwezesha mazingira yale yaweze kufikika kwa urahisi.

Vilevile niseme kwamba msitu wa NOWU ambao kama nilivyosema sikuuona katika mpango wowote wa Wizara basi uangaliwe kwa sababu jinsi ambavyo uvunaji unafanyika katika msitu ule mazingira yale ni hatari kujaribu kufanya *extinction* ya msitu ule. Hali ilivyo sasa hivi ni kwamba kuna uvunaji haramu wa mbao, sasa ninaomba Serikali ihakikishe kwamba ulinzi unaimarishwa katika msitu ule na kudhibiti shughuli zote za uvunaji haramu ili zisiendelee na kuhatarisha hali ya msitu ule.

Mheshimiwa Spika, nizungumze juu ya wanyama waharibifu wa mazao. Kule kwangu Babati vijijini kuna tatizo la hawa wanyama wanaoitwa Tembo. Ukanda wote wa Hifadhi ya Taifa ya Tarangire kumekuwa na tatizo kubwa la muda mrefu, tatizo la kushambuliwa kwa mazao ya wananchi kama vile mahindi na mbaazi. Hili linatokana na kutokuwa na doria ya kutosha. Ninaishauri Serikali iweke vituo vya kudhibiti wanyama hawa waharibifu ili wasiendelee kuharibu mazao ya wananchi. Hali ilivyo sasa hivi ni kwamba wananchi wanalima mazao yao vizuri lakini wakati wa mavuno ukifika wavunaji ni wanyama hao waharibifu. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali isaidie wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, pia niseme tu kwamba mwaka jana 2008 ekari 2447 ziliharibiwa na wanyama hawa kiasi cha kuathiri wananchi 453. Mwaka huu 2009 tayari kuna *report* ya uharibu wa ekari 1500 na taarifa zinazidi kuja katika Ofisi za Serikali. Sasa taarifa zimeshapelekwa Serikalini ikiomba fidia au tuseme kifuta machozi kwa wale ambao wameathiriwa na tatizo, lakini mpaka sasa hatua hazijachukuliwa au fidia hii haijatekelezwa kwa ajili ya wananchi hawa ambao wamepata hasara kubwa kutokana na madhara haya waliyoyapata.

Kwa hiyo, ninaomba Wizara iitikie kilio cha wananchi hawa na niseme katika suala la kuhakikisha kwamba hali hii isiendelee ya uharibufu kituo ambacho ni muhimu katika eneo la ukanda wa Tarangire kianzishwe pale.

Lakini niseme vilevile kuna utafiti unafanyika yaani utafiti wa namna ya kufukuza wanyama hawa yaani Tembo. Wanasema kuna matumizi ya Tumbaku au matumizi ya Pilipili inasaidia sana katika kuwafukuza wanyama hawa. Sasa huu ni utafiti ambao tunapenda kuona matokeo yake yafanyika mapema ili kuondokana na adha hii ambayo wananchi wetu wanakabiliana nayo kwa muda mrefu siku zijazo basi mambo haya yasiendelee kuathiri wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la Hifadhi ya Taifa yaani *Tanzania National Parks (TANAPA).* Napenda tu niseme kwamba naishukuru *TANAPA* kwa ushirikiano mzuri iliyonao na wananchi wa maeneo husika au maeneo ya jirani. Sisi Halmashauri ya Wilaya ya Babati ni mojawapowa watu ambao tumenufaika kutokana na miradi ya ujirani mwema.

Mimi ningependa ushirikiano huu ambao upo uzidi kudumu na sisi wenyewe tutashirikiana na *TANAPA* ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na ushirikiano mzuri kwa ajili ya maendeleo yetu na kwa ajili ya kutunza vilevile wanyama ambao tunapakana nao. (*Makofi*)

Lakini niikumbushe Serikali; kwamba pamoja na shukurani hizi nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba *TANAPA Tarangire* yaani eneo la Tarangire kuna vijiji vitatu vya Gijedabug, Ayamango na Gedamar ambavyo kwa muda mrefu sasa vimekuwa na mgogoro na *TANAPA* na mgogoro huu si mgeni Serikalini na mwaka huu ni wa nne sasa tunajaribu kuzungumzia mgogoro huu. Lakini hatua ambayo tumeifikia ni kwamba tuko kwenye hali ambayo si ya kwenda mbele wala nyuma lakini tumebaki katikati hakuna hatua zinazochukuliwa mpaka sasa. Wananchi wale walikuwa wapewe eneo mbadala lakini Serikali haijafanikiwa kufanya hivyo. Kwa hiyo, bado wazo letu la awali la kuona kwamba ardhi ambayo sasa hivi wanaishi basi ihawilishwe kama namna ya kupata ardhi mbadala imeshindikana basi wasaidiwe kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini juu ya yote ombi letu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba angekuja Babati na kuona au kujionea yeye mwenyewe mazingira ya pale Babati na kuonana na wananchi wa eneo hilo. Itakuwa msada mkubwa sana, na vilevile ni vizuri na ni namna rahisi zaidi ya yeye kutatua tatizo hilo. Kwa hiyo, ningependa Waziri mwenyewe aje Babati au anapohitimisha hapa atuambie wananchi wa Babati anatuahidi nini? Anakuja lini? Ni ili tujiandae kwa mapokezi ambayo atastahili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nisisitize tu kwamba kuna kazi kubwa mbele yetu ya kuhakikisha kwamba raslimali zetu hizi tunazitunza, tunahakikisha kwamba zinatupa manufaa sisi Watanzania na kila mmoja akichukua nafasi yake basi mimi naamini tunaweza kuleta maendeleo kwa nchi yetu na kuhakikisha maendeleo endelevu kwa raslimali tulizonazo. Nimalizie tu kwa kusisitiza yale ambayo nimeyasema hapa mwanzo kwamba kifuta machozi kwa wananchi wa vijiji nilivyovitaja kifanyike mara moja lakini vilevile barabara niliyoiomba kwa ajili ya msitu wa *NOWU* niliyoiomba ifanyiwe kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nikushukuru kwa nafasi hii ambayo nimepata asubuhi hii kuelezea yale ambayo wananchi wa Babati wamenituma niwasilishe hapa. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja hii asilimia mia moja na ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Damas P. Nakei, na ninamwita sasa Mheshimiwa John P. Lwanji, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo na wakati huo Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto ambaye hayumo ukumbini popote alipo ajiandaye. (*Kicheko*)

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja hii muhimu ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze pacha wangu Mheshimiwa Chiligati kwa kupasha moto kiti cha Waziri Mkuu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Ndugu zangu Mama Mwangunga na Mheshimiwa Maige kwa hotuba nzuri na kwa kweli sisi watu tunaoishi katika mbuga zile za Rungwa, Muhesi na Kizigo na zile *open area* za uwindaji za Chaya tuna kila sababu ya kuwashukuru hawa watu na katika muda mfupi tangu tumewapelekea matatizo wamejaribu kuyatanzua matatizo haya. Mwelekeo ni mzuri na ninawatakia kila la kheri hawa watu waweze kufanya kazi yao vizuri.

Tunaona kuna dalili ya uzalendo kwa hawa watu, ka uzalendo maana hii Wizara ina vishawishi vingi lakini kinachotakiwa ni kuweka maslahi ya nchi kwanza na uzalendo na kama tunavyofahamu sekta ya utalii imechangia sana katika pato la Taifa na hivyo kujaribu kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunaona kwetu kule kuna mabadiliko kutokana na na juhudi za Wizara hii katika Kata za Rungwa, Mgandu, Idodyandole, Itigi na kadhalika tunaona kuna mabadiliko na ni juhudi za hawa watu.

Mheshimiwa Spika, hapa ndani nina mjasiriamali mlemavu ambaye ulimtambulisha yuko kule *gallery* yeye ni mlemavu hana mkono mmoja lakini kutokana na juhudi za Wizara hii wamejaribu sana kumboreshea kwani huyu mtu anachimba visima kule Rungwa kwa kutumia Nyundo na Tindo.

Sasa waliona juhudi zake na mpaka juzi tayari wameshampatia mashine yaani pampu ya maji pamoja na jenereta. Sasa kama alivyokuwa anaseme Ndugu yangu Ole Nangoro hapa kwamba *conservation with the human face* ndiyo hiyo na mambo mengine mengi kwani tumechimbiwa visima vya maji kwa kweli tuna haki ya kuweza kushukuru.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kama tunavyofahamu ni tajiri sana lakini ukiangalia katika orodha ya nchi 50 hapa duniani zilizo maskini sana Tanzania ni mojawapo.

Lakini sasa unashindwa kuelewa ni kwa nini tuwe hapo ingawa tumepanda kwani ukiangalia katika tovuti katika zile nchi 10 maskini sana Tanzania hutakuta katika zile nchi za kwanza 10 maskini duniani. Ukienda katika nchi zile 20 huwezi kuikuta, ukienda zile nchi 30 huwezi kuikuta lakini ukienda katika zile nchi 50 utaikuta hapo lakini Kenya na Botswana hawapo. Hii inaonyesha kwamba kuna juhudi kabisa za makusudi za Serikali kuondoka kule mkiani na kupanda ili kuondokana na umaskini wa kutupwa.

Mheshimiwa Spika, tusipotumia raslimali zetu vizuri hatuwezi kuendelea na tutafanana na watoto au wazawa wa Esau. Unakumbuka katika kitabu cha Mwanzo katika Biblia, Esau aliuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa kitu kidogo tu. Aliuza haki yake ya kuwa mzaliwa wa kwanza kwa chakula cha Dengu tu! Alitoka kuwinda lakini aliporudi nyumbani alikuwa ana njaa sana akamwambia mdogo wake Yakobo kwamba Bwana nipatie chakula, akamwambia Bwana ninaomba unikabidhi haki yako ya mzaliwa wa kwanza. Basi yule Bwana kwa sababu ya njaa akampa na akapoteza vyote alivyokuwa navyo vya urithi na kadhalika kwa sababu ya Dengu tu.

Mheshimiwa Spika, ninawaomba watumishi wa Serikali na hasa wa Wizara hii tuwe makini tusije tukauza haki yetu kwani vitu vyetu vinaporwa na watu wa nje na sisi wenyewe tunaendelea kubaki maskini. Kwa hiyo, ninaomba tuzingatie hilo na tuwe makini kama ambavyo wenzetu wanataka kuonyesha njia sasa hivi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, tunazo changamoto kwa mfano matatizo ya wanyamapori wetu bado yapo. Nadhani mkiangalia ukutani Waheshimiwa Wabunge mtakuta kuna Simba na safari hii Mheshimiwa Mmoja aliniambia je utazungumza habari za Simba? Nikamwambia ndiyo Simba wapo lakini wale wanaokula binadamu hawapo.

Nadhani mnawaona hapa, sasa hao Simba waliokuwa wanakula watu sisi kwtu walishughulikiwa vizuri sana tatizo hilo likaondolewa na binadamu wanaishi bila hofu kwa hiyo ninaishukuru sana hii Wizara.

Lakini tatizo lingine ambalo bado lipo ni tatizo la Tembo mnaita Ndovu au Tembo lakini tatizo hilo lingali lipo kwa upande wa mazao yetu yanaharibiwa na hawa wanyama. Ninaomba Wizara hii iwe makini na ijaribu kuona kama tatizo hili linaweza nalo likaondolewa.

Sasa Wizara inasema kwamba katika kipindi cha mwaka 2005-2008 Wizara ilipeleka shilingi bilioni moja na laki nane kwa Halmashauri za Wilaya zenye utalii wa uwindaji lakini sasa nashangaa katika Wilaya ya Manyoni mpaka sasa hatujapokea hizo pesa. 2005-2008 lakini sisi Wilaya ya Manyoni kwa mwaka ulioisha wa 2008 hatukupata hizo pesa ingawa miaka ya nyuma ndiyo tulipata lakini nazungumzia mwaka 2008 hatupata hizi pesa. Sasa tunaomba wenzetu waliangalie ili tatizo ili tuweze kumaliza matatizo hayo ya wanyama waharibifu pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, hatujapata kifuta machozi, watu wetu walioharibiwa mazao, waliopoteza uhai wao kutokana na wanyama hawa Simba pamoja na Tembo mpaka leo hatujapata fidia kwa hawa watu, hawa watu mpaka sasa hivi wanadai fidia zao ndugu zao pamoja na wale walioharibiwa na orodha tulishapeleka wizarani kupitia KDU lakini mpaka sasa hivi hatujapata malipo hayo. Ninaomba wenzetu kero hizi waziondoe ili tuweze kusonga mbele vizuri na wananchi waweze kushughulika na mambo yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nilishauri mwaka jana kwamba zao la Asali ni zao muhimu pamoja na Nnta. Nilipendekeza kwamba basi waone uwezekano wa kuunda Bodi ya Asali, sasa hili zao ukiliangalia utafiri kama ni zao ambalo linakwenda kiulanguzilanguzi halina soko maalum hasa ni zao la hamu mtu anapotaka Asali anakuagiza lakini Mamlaka hasa ya kusimamia zao hili bado haijaundwa.

Nadhani Wizara ilizungumzia suala hili kwamba kuna Mamlaka ambayo itaundwa ili iweze kushughulikia. Naomba sana na ninapendekeza tena pia ninashauri kwamba iundwe Bodi ya Asali na Bodi ya Nnta kwa pamoja ili iweze kushughulikia zao hili muhimu.

Mheshimiwa Spika, pia sambamba na hilo hizi *Game Reserves* mimi nadhani umefika muda kwamba zingekuwa na Mamlaka yake tofauti na *TANAPA* kwa sababu Mamlaka hii ya *TANAPA* nadhani iko *over stretched* kwenye hifadhi hizi.

Sasa ninapendekeza kwamba hizi Mbuga za Hifadhi yaani *Game Reserves* nazo zingeundiwa Mamlaka yake ili mbuga hizi ziweze kusimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inajua umuhimu wa Bwawa la Rungwa, hili Bwawa lilivunjika likapelekwa na maji, likabadili kabisa maisha ya watu wa Rungwa, watu wa Rungwa bila Bwawa hilo hawaelewi maisha yanakwendaje kwa sababu hayaendi vizuri pamoja na kwamba jitihada zimefanywa kwani wamechimbiwa visima na vingine havikuwa na maji lakini wanajikongoja na juhudi za watu wengine binafsi kuweza kupata maji lakini Bwawa hilo lilikuwa ni *multipurpose* kwani maji yake yalitumika kwa binadamu, wanyama na pia kilimo.

Sasa lile Bwawa ninapenda kupata majibu kutoka kwa wahusika hapa kwamba ni lini litaanza kujengwa? Nimesikia fununu lakini ni vizuri iwekwe wazi kwamba hili bwawa la Rungwa na hizi fedha zilizotengwa takribani shilingi milioni 500 mimi naona hizi pesa zinatosha kabisa kama tunaweza tukapata lambo au bwawa kwa shilingi milioni 100 sasa hizi milioni 500 zinasubiri nini? na kila siku tunavyozidi kwenda gharama zinapanda na pesa nyenyewe inazidi kushuka thamani.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba jibu kutoka kwa wenzetu kwamba tuelewe moja Rungwa tunasimama vipi? Hili Bwawa litajengwa na kama linajengwa mwaka huu ni lini? tukitoka hapa ndiyo wanakwenda kuanza kazi?

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo tunalo ambalo kwenye maeneo yetuya Rungwa ni tatizo la Mbung'o. huwa tunapita hiyo barabara tunapokuwa tunasafiri ole wako usipate *break down* utakuwa na matatizo makubwa. Lakini tatizo la Mbung'o linajulikana kwamba linasababisha ugonjwa wa Sotoka kwa mifugo na ugonjwa wa Malale kwa binadamu.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo ninaomba hili tatizo liangaliwe kwa sababu pamoja na kwamba linaonekana kwamba ni dogo lakini athari zake ni kubwa kwa sababu limesababisha hii sekta ya mifugo kwa upande mwingine liweze kuwa na matatizo kwa sababu ya tatizo la Sotoka pamoja na upande wa binadamu kuna tatizo hilo la Malale.

Mheshimiwa Spika, mimi nirudie tena kuwashukuru ndugu zetu na kwa kweli tunawatia moyo waweze kututumikia kwa uadilifu, waepuke tu hilo suala nililosema la, vishawishi, watulie wafanye kazi ili nchi yetu iweze kupata neema kwa kutumia raslimali zetu zilizopo ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi ninaunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Lwanji, ni zamu sasa ya Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, atafuatiwa na Mheshimiwa Kabwe Zitto Zuberi, ambaye sasa tayari, baada ya kusikia wito wa Spika, akatoka kwenye chai sasa yuko hapa. (*Kicheko*)

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, pia nampongeza Naibu wake, na Katibu Mkuu, Wataalamu husika na Wakurugenzi pia.

Pia nampongeza kwa namna ya pekee, Mkurugenzi wa Wanyama Pori, kwa kuwa kuna siku nilikuwa nasafiri kati ya Nangurukulu kwenda Liwale, nilipata matatizo na ilikuwa karibu na Miguruwe kambi ya Selou.

Walinipa msaada mzuri mkubwa, nashukuru kwamba, nilisafiri vizuri hadi kufikia Liwale. Naomba muendelee na tabia hiyo, kiasi cha kwamba, hata maendeleo ya wananchi yawafikie kikwelikweli kama msaada mlioweza kunipa mie binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hotuba kama nilivyosema ni nzuri, lakini ninachowaomba ni kwamba, itekelezeke, na naomba sana sana, Mheshimiwa Waziri, huyu mama ambaye ni dada yangu pia, asaidiwe kikamilifu, maanake msimsaidie kutayarisha hotuba peke yake, mumsaidie pia katika utekelezaji wa hotuba hii kikamilifu. Hilo ndilo jambo la msingi, vinginevyo, itakuwa mnamuweka katika mahala ambapo kila siku tutaendelea kumlaumu.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi Waziri aliyeko madarakani hajatembelea Mbuga za Wanyama huko Liwale. Sasa, wanamwogopesha nini? Na nashangaa Mheshimiwa Ndugai, ambaye ndiye Mwenyekiti, wa Wizara hii katika Kamati husika, na hata yeye hawezi kumshawishi Waziri. Kila siku namuona na yeye anakwenda huko Kaskazini, kuna nini? Sisi hatuna hoteli kule? Ndiyo maanake, siyo? Mnafuata nini? (*Kicheko*)

Naomba hili mliangalie, kama mnataka kuwa karibu na wananchi wa Liwale, basi mje karibu na matatizo ya wananchi, ambayo yanatokana na wanyamapori, ambao nyie ni ndugu zenu. Naomba sana hilo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tuko katika `Kilimo Kwanza'. Nina wasiwasi kama hatua hii ya Kilimo Kwanza, kweli itaweza kutekelezeka Liwale. Hii inatokana na kwamba, kuna wanyamapori waharibifu, pia wanahatarisha maisha ya wananchi, hilo wanalijua na *games scouts* tulionao kwa Liwale, ni sita tu. Eneo la Liwale lina *games scouts* Sita tu, na kuna vijiji 42. *Game scouts* sita watawezaje kudhibiti wanyamapori ili wananchi hao waweze kutekeleza vizuri Kilimo Kwanza? Naomba Serikali kupitia Halmashauri zetu, iwe na mpango kabambe wa kuongeza *game scouts. Historically,* Liwale ilikuwa na *game scouts* zaidi ya 40 wakati wa ukoloni, na tatizo kubwa lilikuwa ni wanyamapori, na hatujaondokana na tatizo hilo. Sasa leo hii kadri siku zinavyokwenda, ndivyo kadri tunavyoweza kupunguza idadi ya askari wa wanyamapori katika maeneo yetu. Mwanzoni mlisema lazima wawepo wenye Diploma, lakini sasa hivi nimesikia kwa Mheshimiwa Waziri kwamba, kuna utaratibu wa kuweza kuajiri vijana wa JKT ambao watafanya kazi hiyo, ambao hawatakuwa katika kiwango kile cha Diploma, naomba kazi hiyo ifanyike haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya hivyo ningependa washirikishe vijana ambao wako katika vijiji vile vinavyohusika kwa wilaya ya Liwale, vinginevyo mkituletea wageni katika vijiji vyetu, gharama zitakuwa kubwa kuwapeleka likizo huko kwao, na nini na nini. Sasa ningependa kwamba, hawa vijana, na hata historia inaonesha kwamba, sisi wenyewe tulikuwa tunalinda hawa wanyama wale, kwa hiyo vijana walioko sasa hivi, kama ni suala la JKT, wachukuliwe kutoka maeneo husika ambayo sisi tunakaa na hao wanyamapori. Naomba Serikali ifuatilie hili, ili ituwezeshe sisi kufanya kazi zetu vizuri kwa ushirikiano na Serikali, na pia wananchi wenyewe waridhike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hii la `Kilimo Kwanza' sisi mwaka huu tumeanzisha kilimo cha umwagiliaji katika vijiji vitatu. Tumeanza na Ngongoele, baadae itakuja Mtawango, halafu Mtawatawa. Vijiji hivi kama kweli tunataka vizalishe chakula, tunahitaji *game scouts* wa kutosha. Kwa hiyo, suala la *game scouts*, naomba serikali ilitilie maanani vizuri sana, vinginevyo wananchi wa Liwale wataendelea kulishwa chakula na Serikali, kila siku. Na sijui kwanini tusifanye utaratibu mwingine katika miradi ya Wizara hii, kwanini msiweze kulima mashamba ya *sample*, ya yale mazao ambayo kusema kweli yanalimwa na wananchi, kama korosho, mtama, mahindi, pamoja na viazi? Unakuta hawa wanyamapori, hasa tembo wanayapenda sana.

Sasa huko kuna misitu mngejaribu kuwatengenezea mashamba, bustani zao ili ku-*divert interest* yao badala ya kwenda kwa wananchi, waende kwenye mashamba hayo, hamuwezi kufanya hivyo, au kupunguza kasi hiyo? (*Makofi/kicheko*)

Hili linawezekana kwa kuwa mimi najua watalii wanapenda kuja kuwaangalia wanyama hao, na pia nyie wenyewe mnashirikiana vizuri sana na hao, kwa hiyo wako tayari kutoa pesa kufanya miradi ya aina hiyo. Nadhani Mheshimiwa Ndugai, unaielewa vizuri Liwale kwa kuwa, kazi yako ya kwanza ulianzia kule Liwale, naomba na hili ulifuatilie kwa karibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nazungumza kila wakati kuhusu ahadi ambayo Wizara hii imekuwa ikitoa kwa ajili ya wananchi wa Liwale. Kuna Boma la zamani ambayo *GTZ* waliahidi kupeleka shilingi milioni nane, na niliishaahidiwa kwamba, shilingi milioni nane, zitapelekwa. Mpaka leo hii, hakuna cha shilingi milioni nane, wala senti nane, na ningeomba wa-*submit* hizo pesa haraka iwezekanavyo kwa Mkurugenzi ili kazi hiyo ya ukarabati wa boma la Liwale ifanyike.

Na siyo hivyo tu, kuna mambo mengi ambayo walikuwa wameahidi na moja wapo ni kuona kwamba, kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu, wanaweza kufufua barabara ya kutoka Liwale kupitia Ndapata, mpaka kufika Ulanga Mashariki. Kazi hiyo haijafanywa, na inashangaza kwamba, Wizara hiihii ikiongozwa na Mheshimiwa Prof. Maghembe, alikuwa ameahidi hivyo, na msaidizi wake aliahidi hivyo, lakini inaelekea kumbukumbu hapa katikati zimepotea. Naomba wataalamu mpeni kumbukumbu hizo nzuri kwa maendeleo ya Liwale, Mheshimiwa Waziri Shamsa Mwangunga.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru Serikali na Wizara, kusema kweli kwa kujaribu kutengeza barabara katika mbuga za wanyama, lakini *technology* wanayoitumia katika ujenzi wa barabara hii kusema kweli, inafuata sana miinuko, milima, juu kwa juu. Sasa mara nyingi barabara

hizi huwa ndefu na hazipiti vijijini kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa barabara hizi, zinawasaidia sana wao wenyewe ili kuangalia wanyamapori wao.

Kuna barabara ambayo imejengwa kutoka Liwale mjini, kwenda Mpigamiti. Mimi niliwahi kupita njia hiyo, tangu enzi ya Banduka, wakati huo akiwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi, mara moja, na watu wa Selou, lakini baada ya hapo haitumiki tena kwa watu wa kawaida.

Kwanza, inapita maeneo ambayo wananchi hawapo, pili ni ndefu mno, kwani kufuata milima ni ndefu. Kwa hiyo, nachosema ni kwamba, pamoja na nyie kufanyakazi yenu vizuri, kutengeneza barabara hizo kwa manufaa yenu zaidi, basi pia wananchi wajengewe maeneo fulanifulani ya barabara zao, ambazo zinaweza kutoka kijiji kimoja, kwenda kijiji kingine, hasa maeneo yale ambayo yako chini ya Selou.

Naomba sana utaratibu huu ufuatwe kwa ajili ya wananchi, vinginevyo haya mnayoyaeleza kwamba, mnajenga barabara, mnajenga barabara, kwa Liwale, barabara hizo ni zenu nyie wenyewe. Kwa hiyo, ninaomba sana, na hata zile ambazo unaweza kupita labda atapita Mkurugenzi au Mbunge, nae atapita kwa vibali maalumu, wananchi hawawezi kutumia barabara zile za Selou kwa kuwa, kwanza kuna mikakati mikubwa sana ya kuwafanya wao wasipite.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ihimize kutatua matatizo yanayowakumba wananchi katika wilaya ya Liwale. Kwa hivi sasa unakuta kuna baadhi ya wananchi mazao yao yamepotea au kuharibiwa na wanyamapori, na pia kuna watu waliopoteza maisha au waliojeruhiwa, zile ahadi ambazo tulipewa kwamba, watapewa kifuta machozi, hazijakamika, na hayo yote yanazungumzwa kila siku, na msemaji aliyetangulia kayasema hayo.

Mimi naomba utafutwe utaratibu ambao kweli unaweza kutekelezeka, vinginevyo tutakuja hapa kuzungumza bajeti, hatumalizi, utekelezaji wake haupo, vinginevyo basi labda bajeti hii isizungumziwe katika Bunge lako Mheshimiwa Spika, izungumziwe huko kwa wanyamapori porini, labda itakuwa na maana maalum. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kuna pia msemo kwamba, sasa hivi Utalii unakwenda Kusini. Kwa kiwango gani? Hakuna mtu anayejua, kwa kuwa kinachofanyika ni kwamba, walewale ambao wanamiliki utalii Kaskazini, ndio wanakwenda Kusini. Hamtoi mwanya kwa baadhi ya wenye uwezo kushiriki katika Utalii unaokwenda Kusini.

Wapo wanaojaribu, wanashindwa kupenya. Sasa maana yake nini? Maana yake ni kwamba, mlima Kilimanjaro unasogea mpaka Kusini au nini? (*Makofi*)

Naomba serikali ifuatilie hili, msitupe tu maneno ya kuturidhisha, wakati haya hayatendeki. Kwa hiyo, tunaomba kabisa itafutwe njia ya kuona wale wenye uwezo wa kushiriki utalii wa Kusini, basi washiriki. Kwa mfano, kwa Liwale palikuwa na Vita ya Majimaji, na hivi vinawezekana vikawa kabisa ni vigezo, lakini unakuta haizungumziwi Majimaji Liwale.

Hata hiyo Majimaji, kusema kweli tunapotosha historia, Kingindo ilikuwa Machemache, na ni kwamba, adui au Mwingereza, au Mzungu akipiga risasi unatakiwa useme Machemache, risasi hii itayeyuka itakuwa maji, na waganga wa shughuli ile walitoka Liwale, na hiyo hatimaye ikafikia hatua kwamba, wamishionari au wale waliotaka kwenda kueneza dini Liwale, waliofika karibu na Liwale, katika kijiji cha Mikukuyumbu, waliuawa kwa kufikiriwa kwamba, hawa bado ni Wazungu wale ambao wana vita ya majimaji.

Makaburi yao yapo, inashangaza wenyewe Wakatoliki wa Ujerumani, wamejenga kanisa zuri kubwa Liwale kwa kumbukumbu hiyo, lakini unakuta Utalii hawatoi mwanya wa kuonyesha kwamba, kuna kitu cha aina hiyo, na hata watalii ambao pia wana dini zao wangeweza kuja kuangalia maeneo hayo, katika makaburi yale, na sasa hivi inakuwa kama sehemu ya kwenda kuhiji kwa Wakatoliki wa madhehebu hayo.

Sasa hili pia liangaaliwe kwamba, tunazo sehemu za vivutio na nyinyi mjaribu kutusaidia kuona namna gani vivutio hivyo vinatumika.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tulikuwa tunazungumzia kuhusu asilimia 25. asilimia 25 kutokana na kitabu chao *pages* 88 na 89, wametoa kabisa *data*. Mwaka 2004/05 Liwale haikupata kitu, 2005/06 Liwale ilipata jumla ya shilingi milioni 43 na kuendelea, 2006/07 Shilingi Milioni 44, mwaka 2007/08 tulipata Shilingi Milioni 16 tu, na hapohapo nilipojaribu kufuatilia kwa karibu nikaambiwa kwamba, tofauti mtaletewa. Basi mpaka leo hii sijapata tofauti hiyo na Mkurugenzi wangu anasema hizo pesa hazijapelekwa Liwale, pesa hizo zimekwenda wapi?

Mwaka 2004/05 kuna maeneo ambayo walipata, pamoja na Monduli, sijui Kilombero na wapi na wapi, lakini Liwale ambayo kusema kweli, inaonekana kwamba, katika uwindaji inafanya vizuri, haikuwekewa kabisa pesa, na hazikupelekwa na waliahidi kabisa kwamba, pesa zitakwenda, zimekwenda wapi? Na hii shilingi Milioni 16 mlisema kwamba, mtaongeza ifikie kiasi cha shilingi Milioni 40, pia mpaka leo haijafika, zimekwenda wapi? Na siyo hivyo tu, mwaka 2007/08 mpaka leo hii kusema kweli, haya maelezo yanayozungumzwa itakuwa ni kitendawili.

Naomba sanasana pesa hizi ambazo ndiyo tegemeo la wananchi kuwaletea maendeleo, ziweze kupelekwa haraka iwezekanavyo ili ziingie katika mkumbo wa maendeleo ya wananchi katika wilaya yangu ya Liwale. Naomba sana Serikali izingatie hilo.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kumuomba Mheshimiwa Waziri, baada ya kueleza hayo yote ambayo nimejaribu kuyafuatilia kwa karibu, anijibu.

Kwa kuwa ameishanijibu kwa maandishi kwamba, pesa zitapelekwa shilingi Milioni nane kwa ajili ya ukarabati wa Boma la Liwale, na mambo mengine mengine, hayo yote aliishaeleza kwamba, atapeleka lakini mpaka dakika hii napokuja kusimama hapa tena leo kutoa mchango wangu, kitu hicho hakijafanyika. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, ufuatilie wewe mwenyewe kwa karibu, wataalamu wako wakushauri vizuri ili uweze kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nasema, ndiyo naunga mkono hoja. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

**MHE. KABWE Z. ZITTO**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na pia kukuomba radhi kwa kuhitajika kunitangaza, maanake nilikuwa nimeishakata tamaa kwamba, nitaweza kuzungumza leo baada ya kuona ile listi ya jana.

Nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Nina masuala machache ya kuchangia katika Wizara ya Maliasili na Utalii, kuhusiana na shughuli nzima za Wizara hii, lakini kabla sijaendelea, kiustarabu na kuonyesha *level* ya *political tolerance,* nipende kuchukua fursa hii kumpongeza Mbunge wa jimbo la Biharamulo Magharibi, kwa kujaza nafasi hiyo na kuwaambia Wabunge wengine kwamba, 2010 inakaribia kwa hiyo, tutakutana huko, muone zile asilimia za Biharamulo Magharibi, labda inawezekana ndio zikaelekea huko kwenye majimbo yenu. Ahsante Mheshimiwa Spika .(*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na Kigoma. Sisi tuna hifadhi mbili kule ambazo ziko chini ya TANAPA, hifadhi ya Gombe na hifadhi ya Mahale, na kumekuwa na juhudi mbalimbali za kuweza kuhakikisha kwamba, watalii wengi zaidi wanaenda katika hifadhi hizi. Kwa sasa hali ya utalii Kigoma ni ndogo sana kwa sababu, hazijafanyika juhudi za makusudi za kuutangaza Mkoa wa Kigoma, pamoja na hifadhi hizi mbili, kama eneo la utalii.

Kwa mfano, mwaka jana Gombe walifika watalii ambao waliingiza shilingi milioni 180 tu ambazo wala haziwezi kuendesha shughuli za hifadhi yenyewe. Tungeamua kwamba, kila hifadhi ijiendeshe yenyewe, hifadhi kama Gombe hivi zisingeweza kujiendesha kabisa. Kwa hiyo, inabidi tushukuru tu kwamba, TANAPA kwa sababu ya *diversification* ya hifadhi mbalimbali, imeweza kuifanya hifadhi ya Gombe, iweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo kubwa sana la miundombinu Kigoma. Unafikaje Gombe? Hilo ndilo tatizo kubwa sana, na watalii wengi sana katika juhudi mbalimbali ambazo tumezifanya za kuweza kuhakikisha kwamba, wanafika Kigoma na kutembelea hifadhi zetu mbili hizi, na hata tunapounganisha pamoja na Katavi, ili mtu apate *package* moja ya Gombe, Mahale na Katavi, bado inakuwa ni tatizo kidogo. Kwa watu wa Mahale, angalau Katavi inawasaidia kwa sababu mtu anaweza aka-*charter* akaenda Katavi pamoja na Mahale, kwa pamoja.

Lakini kwa watu ambao wanakuja mpaka Kigoma kwa mfano, wanashindwa kwenda Mahale kwa sababu ya usafiri, na kumekuwa na juhudi ambazo Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini, amekuwa akizungumza na watu wa TANAPA kwa ajili ya uboreshaji wa barabara, ambayo inaelekea kule Kalya ili TANAPA waweze kuchangia kidogo kuhakikisha kwamba, tunafungua njia ya barabara ya utalii kwenda kule Mahale. Kwa hiyo nilikuwa naomba, Waziri na kwa sababu uongozi mzima wa Wizara uko hapa, ujaribu kuangalia hili kwa ajili ya kuifungua Mahale, ili iweze kupata watalii wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Gombe, hivi sasa na ninapenda nimshukuru kwa dhati kabisa Waziri wa Miundombinu, Wizara ya Miundombinu, imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Gati la Kagunga, mpakani kabisa na Burundi kwa sababu zamani watalii waliokuwa wanakuja Mahale, walikuwa wanaanzia Uvira-Kongo, wanaenda Burundi ndio wanakuja Gombe.

Lakini baadae baada ya vurugu na matatizo ya miundombinu, hali hiyo ikawa imebadilika kidogo. Kwa hiyo, sasa nirudie kusema kuwa, nawashukuru sana Wizara ya Miundombinu kwamba, wanajenga Gati pale Kagunga, kwa hiyo itakuwa ni rahisi sana kwa watalii kutokea Uvira-Kongo, Bunjumbura-Burundi, kuingia Kagunga kwa ajili ya kwenda Mahale.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho nigependa kuomba Wizara iangalie ni kwamba, hifadhi ya Gombe ile inapakana na vijiji viwili kwa upande wa Ziwa Tanganyika.

Kijiji cha Mtanga na kijiji cha Mwamgongo, na kijiji cha Mwamgongo ni kijiji maarufu sana ndiyo anakotoka Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya. Ni kijiji maarufu kwa siku nyingi sana, watu wa kule wamekuwa wafanyabishara wa muda mrefu sana na tungependa vijiji hivi viwili, Mtanga na Mwamgongo viwe ni vichocheo vya utalii. Watalii wafike waangalie tamaduni za watu wa pale, wale chakula cha watu wa Kigoma, washiriki kwenye uvuvi na kadhalika.

Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba kuangalia katika bajeti hii na hata bajeti inayofuata kama kuna uwezekano wa kujenga angalau magati madogo, kwa Mtanga na Kagunga ili watalii sio lazima wakifika waende wakakae kwenye *rest houses* za hifadhini. Wafanyabiashara wadogowadogo, na watu wa Kigoma ni wafanyabiashara sana, wanaweza wakajenga maeneo ya watu kukaa, na fedha zikawa zinabaki ndani ya vile vijiji.

Tunaweza pia kutumia ule Mpango wa kuondoa Umasikini kupitia Utalii katika vijiji hivi, ili kuweza kusaidia kuleta maendeleo kule. TANAPA wamejenga kituo cha utalii pale Kigoma, kama *tourist information centre* lakini bado ni ya *TANAPA* kwa sababu utalii wa Kigoma ni zaidi ya hifadhi.

Utalii wa Kigoma ni pamoja na Ujiji. Ujiji kama mji wa mwanzo kabisa duniani, jana nilisikia hapa watu wanatetea Tabora, wanatetea Songea, lakini bado hakuna mji ndani ya Tanzania ambao ni mzee, "Mkongwe" yaani wa muda mrefu kama Ujiji, kwa sababu Ujiji na Nairobi, ziliundwa pamoja lakini hali ya Ujiji sasa hivi ni mbaya sana.

Kwa hiyo tunaweza tukaangalia pia ni jinsi gani ambavyo tunaweza tukasaidia na hasa kile kituo cha Dr. Livingstone, ili kuweza kuhakikisha kwamba, watu wa Kigoma wanafaidika kutokana na utalii.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo ambalo tunalo sasa hivi kwamba, kuna Sokwe ambao wako nje ya hifadhi, hawahifadhiwi. Kuna kama Sokwe 940 hivi wanazagaa katika mapori ya Rugufu, Uvinza kule na kadhalika. Sasa tulikuwa tunaomba tuangalie uwezekano wa kuwa na programu maalum kwa ajili ya kuwahifadhi Sokwe hawa.

Watu wa *Jane Goodal Institute* wameanza programu ya kuweza kuona ni jinsi gani mbavyo watajua vizazi vya hawa Sokwe na kadhalika, lakini juhudi za Serikali katika hili bado hatujaziona na Sokwe hawa wanaweza kuwa ni chanzo kikubwa sana cha utalii. *Actually* Sokwe ambao wako nje ya hifadhi za Gombe na Mahale, ni wengi zaidi kuliko Sokwe ambao wako ndani ya hifadhi. Kwa hiyo, hilo nalo nilikuwa naomba tuweze kuliangalia.

Tulipokuwa kwenye kampeni, Biharamulo, tumekutana na tatizo moja kubwa sana ambalo ningependa tuweze kulizungumzia maanake bahati mbaya Biharamulo wamekuwa hawana Mbunge toka mwaka 2007 mpaka alipopatikana ndugu Oscar jana hapa. Kuna tatizo la Ndovu, kuvamia mazao ya wananchi, hasahasa katika Kata ya Nyakahura, na suala hili jana *by the way* nilikuwa namsikia Mheshimiwa Masilingi, anazungumza wakati tuko kwenye kikao cha Kamati ya uongozi kule kwamba, kwanini pori hili la Buriji lisiondolewe? Lakini mimi napenda sana hifadhi, lazima tuangalie faida na hasara za kuondoa au kutokuondoa.

Lakini lazima tuangalie pia jinsi gani ambavyo tunalinda raia wetu, kwa sababu kwa kule Buriji, inaonekana kwamba, Tembo wale ni bora kuliko wananchi, kitu ambacho kwa kweli ni kibaya sana. Mkienda wanasiasa wananchi wanalalamika, wanalia sana kwa jinsi ambavyo wengine wamekuwa hawalimi sasa kwa hiyo wamekuwa masikini sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri aweze kuliangalia suala hili na jinsi ya kuweza kulitatua. Tatizo hilohilo lilo Nguruka pia. Upanuzi wa ile *Game Reserve* umepelekea wananchi wakose maeneo ya kulima na kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu sana, na kwa hili kwa kweli nilikuwa naomba Naibu Waziri, ajaribu kuangalia kwenye ratiba yake, Naibu Waziri kwa sababu najua Nguruka jinsi ilivyo.

Kwa hiyo siwezi kumwomba Waziri, maanake wewe ni kijana mwenzangu, uangalie kwenye ratiba yako na labda ushauriane na Mbunge wa kigoma Kusini, kuweza kwenda kule Nguruka kuona jinsi gani tutakavyotatua hili tatizo la maeneo ya wananchi kulima, kwa sababu jinsi ambavyo wananchi wanaondolewa katika maeneo yao ya kulima, inasikitisha sana, na wanazidi kuwa masikini sana, na mnafahamu kuwa Nguruka ina ardhi yenye rutuba sana.

Mheshimiwa Spika, la tatu ambalo ningependa kulizungumzia ni suala ambalo Mheshimiwa Ndesamburo alilizungumzia kidogo hapa jana lakini, halijawekwa kwenye muonekano ule mpana zaidi.

Serikali iliamua kubinafsisha Hoteli ya *Seventy Seven* na watu wakawa wameomba waweze kuipata ile hoteli. Miongoni mwa walioomba ni kama yule mtu ambaye anamiliki Impala Hotel, lakini baadae Serikali, hatujui kwa taratibu zipi ambazo zilitumika ambazo ningependa Serikali iweze kutoa maelezo, kwa sababu hata katika Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, tumeshindwa kupata hayo maelezo kutoka kwa *Consolidated Holdings*, Serikali ikawa imemnyang'anya yule mtu ambaye alishinda ile zabuni ya kununua ile hoteli, na akapewa mtu mwingine.

Yule mtu akaenda mahakamani, akashinda na akatakiwa alipwe fidia, Serikali ikashindwa kumlipa fidia, akaenda Mahakama ya Rufaa, Mahakama ya Rufaa, ikakazia ile hukumu ambayo ilitolewa na Mahakama Kuu ili huyu mtu apewe fidia.

Lakini baadaye Serikali ikaamua kufanya mazungumzo ya nje ya Mahakama kumlipa fidia yule mtu wa Impala Hotel, lakini wakati huohuo ikampa na hoteli ya *Moshi Hotel* bure. Yaani fidia yake, akalipwa na akapewa *Moshi Hotel*, bure. Wakati anapewa *Moshi Hotel*, bure tayari kule Moshi *Hotel*, utaratibu wa ubinafsishaji ulikuwa unaendelea na mtu mwingine alikuwa ameishapewa hoteli ile. *(Makofi)*

Sasa mpaka leo yule mtu hajarudishiwa fedha zake alizolipa kama asilimia 25 kwa ajili ya Moshi *hotel*, suala liko Mahakamani. *Moshi Hotel* haifanyi kazi sasa hivi, kuna wafanyakazi zaidi ya

250 ambao mpaka sasa hawajalipwa mafao yao, wafanyakazi wa *hotel Seventy Seven* mpaka sasa hawajalipwa mafao yao, kwa sababu Mfilisi amekataa kuwalipa.

Kwa hiyo, suala hili tulikuwa tunapenda kupata maelezo kutoka kwa Serikali. Kwanza, ni utaratibu upi uliotumika kumnyang'anya mtu aliyeshinda zabuni, na baadaye kwenda kuzungumza naye na kumrudishia hela zake, na baadaye kwenda kumpatia hoteli nyingine ambayo wala hakuiomba?

Kwa hiyo, nilikua naomba Serikali iweze kutupatia maelezo katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, suala la nne kwa ufupi tu ni kwamba, kuna haja ya kuangalia upya usimamizi wa Sekta ya Utalii. Sasa hivi utangazaji wa utalii unafanywa na Bodi ya Utalii, lakini vilevile watu kama *TANAPA* wanafanya pia utangazaji wa Utalii.

Lakini kazi ya *TANAPA*, kimsingi ni uhifadhi na kulinda zile hifadhi zao, na tumekuwa tukiweka *pressure* nyingi sana kwa *TANAPA* kwa mambo mengi sana, *of course* hata sisi tunafaidika kwa njia moja ama nyingine, kule jimboni kwangu kule vijiji mbavyo vinapakana na hifadi, wasichana wamejengewa mabweni, kitu ambacho nashukuru *actually* napenda niipongeze *TANAPA* kwa hilo, kule Bugamba limejengwa bweni kwa ajili ya wanafunzi na kadhalika lakini, kuna haja ya kuangalia namna ya ku-*harmonize*, ni vyombo vipi ambavyo vinasimamia sekta ya utalii?

Mapendekezo ambayo sisi tumekuwa tukiyatoa hayajawa rasmi ni kwenye mijadala, ni kwamba, kuwe na Mamlaka ya Utalii, ambayo itaunganisha shughuli ambazo hivi sasa Bodi ya Utalii, wanafanya, shughuli ambazo zinafanyika za utoaji wa leseni za shughuli za utalii na mahoteli, na vilevile shughuli za kutangaza. Kwa hiyo, kutakuwa na *marketing arm* ya Mamlaka ya Utalii, na Sheria ya Utalii imeunganisha hizi Sheria zote. Kwa hiyo, ni muhimu tuweze kuangalia, kuhakikisha kwamba tuna-*hamornize*, vinginevyo inakuwa ni tatizo kubwa sana. Utakuta kuna *delegations* nyingi *TANAPA* ina *delegation* yake, Bodi ya Utalii ina *delegation* yake, na inakuwa ni gharama sana.

Lakini vilevile nirudie taarifa ambayo tuliitoa kwenye Kamati ya Mashirika ya Umma kwamba, Serikali ijiondoe kwenye uendeshaji wa Mashirika haya ya kila siku, na jana Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, amezungumzia taarifa ya *Controller* na *Auditor General,* ambayo bado Kamati inaifanyia kazi kuhusiana na suala la malipo ya matangazo ya *CNN.* Yale malipo ukiyaangalia kwa haraka, utapeleka lawama zote *TANAPA,* lakini hali halisi ni kwamba, lawama zote zinaenda serikalini kwa sababu Serikali iliingilia kazi za *TANAPA.* Kwa hiyo, hili suala inabidi uweze kuliangalia kwa mapana yake.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni hili ambalo jana Mheshimiwa Anne Malecela alilizungumza kuhusiana na suala la nyara ambazo zilikamatwa Vietnam. Taarifa ambayo tuliipata kutoka serikalini ni kwamba, Serikali ilikuwa inafanya uchunguzi kwa kushirikiana na *Interpol* kwa kushirikiana na Lusaka *Agreement.*

Kwa hiyo, tungependa wakati Waziri anatoa maelezo yake, aweze kutupa *details* ni nini ambacho hasa kilitokea kuhusiana na suala hili la nyara za taifa kukamatwa nchi ya kigeni, tena Serikali ya nchi ya kigeni ndiyo ikatutaarifu sisi. Ina maana huku kwetu kote ilipita bila kuwa *detected*. Kwa hiyo, tungependa kupata maelezo ya kina kuhusiana na suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo niliweza kujikusanyakusanya baada ya kuwa, nimekata tamaa kwamba, sitaongea. Lakini naamini kabisa kwamba, kuna hoja ambazo nimeziweka. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zitto mchango wako mzuri tu. Sasa Mchangiaji wa mwisho kwa mujibu wa orodha yangu hapa ni Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia.

**MHE. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi na mimi nichangie juu ya hoja hii. Awali ya yote nataka kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu

Mkuu na watumishi wote kwa hotuba nzuri waliotuletea. Jambo la tatu nataka kuishukuru Wizara kwa kazi nzuri waliofanya kule Rufiji hususan katika kuhimiza na kuendesha ufugaji wa nyuki na umefanikiwa vizuri na naomba tu kwamba Wizara itusaidie kutupatia masoko.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Wizara imejitahidi sana kukarabati viwanja vya ndege vilivyoko katika hifadhi ya Selous, Kiwanja cha Mtemela, Kiwanja cha Nyakingupira kazi nzuri. Nataka niseme tu kwamba nimsifu Mheshimiwa Waziri kwa hatua za haraka alizochukua kwa sababu kule Rufiji tumeletewa *DC* huyu ni mchapakazi mno, nataka nimtamkie hapa Nakasi Majaliwa tangu aje yeye zimeshakamatwa roli za mbao nyingi, umeshakamatwa mkaa gunia 2,500 na wale Wamalira wanaoingia porini kwenda kukata mikaa sijui wanatoka Mbeya au sijui wanatoka wapi watu 25 wamepelekwa kortini na kupata adhabu moja kwa moja. Jambo hili lilitutia nguvu Warufiji wote kwamba maliasili sasa imepata mtu wa kuangalia vizuri na hafanyi kazi peke yake anakwenda na Kamati ya Ulinzi yote ya Wilaya. Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutuondolea Ofisi mmoja alikuwa ana *backer break* operesheni hii. Tulivyokuletea jina nasikia umeamua mara moja hayupo, hongera sana Mheshimiwa Waziri. Jambo lingine sasa turudi kuboresha hali ya *Selous, Selous* kama ujuavyo ina ukubwa wa *square kilometre* 54,600 ndio kubwa katika Afrika ni kubwa kuliko nchi nyingi hasa Switzerland nchi za Ulaya hali ya mle ndani inahitaji kazi kubwa hasa katika barabara zake. Katika jibu la msingi hapa wiki mbili zilizopita Mheshimiwa Waziri alituambia barabara ndani kule ni nzuri lakini naomba atupie macho zaidi ili kama changarawe iwe changarawe inayopitika mwaka mzima. Barabara zingine ni za masika tu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini ilishindwa kwenda *Stigler's Gorge* kwa sababu hiyo barabara ya kufika kule wakati wa masika inakuwa chepechepe haipitiki, kwa hiyo nilikuwa naomba hili alitilie mkazo kuhakikisha kwamba barabara za ndani ya Selous zinapitika. Hii inakuwa haieleweki sana wakati Selous inatengeneza shilingi bilioni 8 lakini hata kutengeneza barabara imebidi ikopwe shilingi milioni 300. Sasa isingekuwa angalau mkaweka shilingi bilioni moja mkatengeneza barabara ya Selous na shilingi bilioni 7 mkafutika kibindoni.

Kwa hiyo naomba hili lizingatiwe kwa sababu ndio litaboresha hiyo hifadhi ya Selous ambayo ni urithi wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunalo tatizo la kuifikia Selous. Kwa hiyo ningeomba sana TANAPA au Wizara itafute namna ya kuisaidia Halmashauri ya Wilaya kutengeneza barabara inayotoka Utete kwenda Kingupira takribani kilomita 75.

Kama ikiwezekana barabara hii ingechukuliwa na Wizara ili iweze kupitika hatuombi lami kule lakini tunaomba changarawe inayopitika mwaka mzima ili watu waweze kufika Kingupira kirahisi. *Ofcourse* utasema kuna kiwanja cha ndege pale, ndiyo, lakini kama unataka kupanua utalii wa ndani watu wengi watatumia sana barabara kuliko kuruka na ndege kwenda Kingupira.

Vile vile katika *Eastern Selous* upande wa Mloka barabara inayotoka Mkongo kwenda Mloka takriban kilomita 100 hivi kwa kweli ikiachiwa tu Wilaya au sasa hivi tuseme *Town Road* Mkoa tungependa nguvu ya Wizara nayo ionekane pale kwa sababu ile barabara ndiyo inahakikisha kabisa watu wanaotaka kwenda Selous kwa kupitia Mloka ndio barabara ya uhakika na takribani ukienda kule kila siku utakutana na watalii wako njiani wanakwenda Selous. Sasa utakuta tu kwamba mara nyingi wanakwama njiani sasa mtu ana nia ya kwenda kutazama pori hili hazina ya Kimataifa, urithi wa Kimataifa anakwenda kule badala yake ananasa njiani, nilikuwa nadhani tungeweza kabisa kusaidia barabara hii ikawa nzuri.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nizungumze juu ya kupanua nyanja za utalii katika nchi yetu. Kuna vivutio viwili tu nilitaka nivitamke nayo ni pale Mji wa Utete liko boma kubwa la Wajerumani na boma lile halikuja bure ilikuwa ni alama ya *resistance* wananchi wanakataa Wajerumani wasiingie Tanganyika, pale ndipo ilipiganwa vita, Mzee mmoja Majihumbi Mzuzuri koo zake marehemu Ditopile akapiga risasi kumpiga Kamanda mkubwa wa Jeshi la Ujerumani pale na akafa pale pale Utete na Wajerumani wakatamka hapa itajengwa hapa boma kubwa la aina yake kwa ajili ya kutawala Tanganyika. Boma likajengwa na hapo ndipo ninaposema lingekuwa

jambo zuri likaongezwa boma hili katika utalii. Jambo lingine hapo hapo Utete Mungu ametujalia kuna chemchem ya majimoto, chemchem hii nilikwisha izungumza hapa lakini ina mambo.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Serikali ya Kijerumani, Wajerumani Tanganyika nzima walikuwa wanakwenda Rufiji kwenda kuoga maji ya moto kutoka chemchem ile na watu wakioga chemchem ile hawapati ugonjwa wa ngozi kabisa.

Nilikuwa naomba umeshafika wakati sasa kwamba Serikali yetu, Wizara hii ipanue utalii huu kwa nchi nzima, kila mahali na kupatangaza na taarifa hizi zipelekwe Ujerumani kwamba wazee wenu kule walikuwa wanaoga maji ambayo ukioga basi hupati tena ugonjwa wa ngozi.

Nilikuwa naomba sana wakati fulani Naibu Waziri aliyepita anajibu swali langu nilimkaribisha kule hata hivyo nazidi kuwakaribisha Mheshimiwa Waziri na Naibu wake njooni Utete muone majimoto haya muone mtasaidia namna gani ili kupanua utalii na kuongeza vivutio vya utalii hapa nchini na hasa Kusini katika wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba sana kuiambia nchi na Serikali yetu watanabahi upya kwamba Wizara hii ndiyo inayotunza maliasili ya nchi hii lakini ina watumishi wachache sana na Bajeti yake ni finyu na ukitaka kuifanyia haki Wizara hii *Manpower* yake lazima upanue mara mbili na Bajeti yake upanue mara mbili pia.

Bila ya hivyo tutaona tu na tutaendelea kulaumu kwamba utoroshaji wa maliasili unaongezeka na hii ni kwa sababu macho yanayotazama maliasili hii ni machache kuliko maliasili tuliyonayo au uwezo wa macho hayo. Huwezi kuwa na duka kubwa halafu ukawa na mlinzi mmoja mahali pa walinzi watano. Nilikuwa nadhani hili ni jambo muhimu sana kuzingatia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nakushukuru sana kwa kunipa nafasi naunga hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana Profesa Idris Mtulia. Naomba kujua hizo dakika.

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge sasa ni wakati ambapo tutasikia kutoka kwa Wizara husika. Tukianzia na Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye atafanya majumuisho kuhusu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa dakika zisizozidi 15 halafu atakuja Mheshimiwa Waziri ambaye yeye haki yake ni dakika 30 ingawa ametaka muda zaidi, lakini tutaangalia namna anavyokwenda.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa sote uzima hata tukaiona siku ya leo, lakini pia nishukuru kipekee kwangu binafsi kwa jinsi anavyonijalia na kunipa nguvu za kuweza kufanya kazi ambazo yeye mwenyewe inampendeza nizifanye.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niwashukuru sana wananchi wenzangu wa jimbo la Msalala mkoani Shinyanga ambao ni wapiga kura wangu kwa kweli wamekuwa ni watu wa faraja na *support* kubwa kwenye mazingira yangu ya kazi hapa Wizarani lakini pia kule jimboni. Wamekuwa wakinipa moyo sana na ushirikiano mkubwa. Niwahakikishie kwamba juhudi kubwa za kufanya Mapinduzi ya kasi ya maendeleo kwenye jimbo letu ambazo wengi wamejionea hata wale waliokuwa na mashaka awali sasa wanashuhudia kwamba jimbo letu la Msalala linapiga kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, niwaombe tu kwamba ushirikiano huu ambao tumeuonyesha kwa miaka takribani 3 iliyopita tuuendeleze kwani kwa hakika yako mengi ambayo tutafanikisha tukiendelea na umoja huo. Pia naomba nitoe shukrani za kipekee sana kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Waziri wangu, Katibu Mkuu Dr. Komba, Wakurugenzi na watumishi wengine katika Wizara ambao pia pamoja na ugumu na wingi wa majukumu katika Wizara lakini hakika wamekuwa wakinipa msaada mkubwa sana na kunipa moyo na kwa kiasi kikubwa ninafarijika na naona tunakwenda vizuri. Lakini kipekee nafikiri ni vizuri nikamshukuru sana msaidizi wangu wa karibu dereva wangu Bwana Oswald Mayunga. Kijana huyu amekuwa

akifanya kazi kwa bidii na kwa kweli nampongeza sana. Baada ya shukrani hizo bila ya kusahau kuwashukuru pia familia yangu akiwepo mke wangu na watoto wangu ambao nao wamekuwa faraja yangu na watu wa kunipa moyo. Sasa naomba nipitie tu baadhi ya hoja ambazo zimesemwa na Waheshimiwa Wabunge hasa kwa kuzingatia suala la muda nitajitahidi kwenda haraka kwa sababu hoja ni nyingi sana lakini tutajitahidi kuhakikisha kwamba tutazizungumzia kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge wengi nitawataja akiwemo Mheshimiwa Dr. Chegeni, Mheshimiwa Killimbah, Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Yona Stanley Kevela, Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo, Mheshimiwa Ameir A. Ameir, Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa na Mheshimiwa Stephen Galinoma. Hawa pamoja na wengine kwa sababu nime-*capture* hii *list* haraka haraka mwishoni kuongezea majina yaliyojitokeza mwisho haijawezekana. Wote wamezungumzia sana suala la kuongeza wigo wa utalii, kuzungumzia kwamba utalii usilenge sana ukanda wa Kaskazini peke yake tujaribu kutangaza na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango wa utangazaji wa utalii na kubainisha maeneo Kitaifa upo. Kanda za Utalii tumezigawanya kwenye kanda mbalimbali na kila kanda ina mikakati yake. Kwa upande wa Kanda ya Ziwa kuna Shirika linaitwa la Uholanzi linatusaidia sana katika kubainisha na kuratibu ubainishaji wa utalii asilia. Tayari wameshaanza kufanya mafunzo kwa watu wa maeneo ya Bujora na Butiama katika mikoa ya Mwanza na Mara. Lakini pia kuna mafunzo yanaendelea kwa mkoa wa Kagera. Mwaka 2004 Wizara yangu ilifanya zoezi la kubaini vivutio vya utalii katika mikoa ya Kagera, Mara na Mwanza zoezi lilishakamilika, orodha ya vivutio tulishavibainisha sasa hivi tunaendelea na hatua ya pili ambayo kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa kwenye maeneo hayo ya kuvitangaza vivutio hivyo. Kulikuwa pia na suala la kutangaza mji wa Mikindani kule Mtwara na fukwe zake. Eneo hili pia liko kwenye ukanda wa utalii wa Kusini ambao utangazaji wake unahusisha pia maeneo ya Lindi, Kilwa ambayo tayari nayo mpango wake umeshakamilika kinachobaki sasa ni hatua zile za utangazaji. Kipekee kulizungumziwa kutangaza maeneo ya mambo ya kale. Mji wa Ujiji ameusema rafiki yangu kijana mwenzangu Mheshimiwa Zitto, Mji wa Tabora ameusema Mheshimiwa Mchemba, Mji wa Songea na maeneo mengine kadha wa kadha.

Mheshimiwa Spika, haya maeneo kila moja limewekewa mkakati wake. Kwa upande wa Tabora na Vijiji njia ya watumwa kuanzia Bagamoyo hadi Kigoma kila eneo ambalo kulikuwa na kituo kumeshabainishwa na kuna mpango kabambe wa kufufua njia hiyo ambayo inahusisha mji wa Tabora na Mji wa Kigoma. Upande wa Mji wa Songea kwenyewe tumeshabainisha na tunakusudia kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge kutambua mji huu kama mji wa kihistoria ambayo ni taratibu za kisheria.

Baada ya hatua hiyo kukamilika hatua ya pili sasa ni kuanza kutangaza maeneo hayo ambayo yatakuwa tayari yameshabainishwa.

Mheshimiwa Spika, kulijitokeza pia hoja na kutangaza mikoa ya miongoni mwa wengine Iringa na Mbeya ambazo hasa lilitajwa na Mheshimiwa Galinoma, Mheshimiwa Kevela. Mkoa wa Iringa una vivutio vingi na vingi vimeshaanza kutangazwa na *TTB* pamoja na *TANAPA. Ruaha National Park* pamoja na Kitulo kipekee vinatangazwa. Tatizo ambalo limekuwepo kwa upande wa *Ruaha National Park* ni suala la miundombinu. *TANAPA* wamefanya kazi kubwa sana katika miaka miwili iliyopita mwaka 2007/2008 na 2008/2009 wametumia jumla ya shilingi 1,800,000,000 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya *Ruaha National Park.* Katika kufanya hivyo wamejenga madaraja wanatengeneza barabara, wanatengeneza hosteli kwa ajili ya wageni wanaotembelea eneo hilo, lakini pia wametengeneza *information centre* ya kisasa kabisa kwa ajili ya kupokelea wageni na kutoa taarifa za utalii.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya utekelezaji wa Sheria ya Utalii iliyotolewa na Mheshimiwa Herbert Mntangi. Sheria hii ya Utalii ilikwishakamilika, kanuni zake zimekamilika, kwa hiyo hatua sasa hivi inayofuata ni ya kutoa elimu kwa umma na kuanza kutekeleza kanuni ambazo tayari zimeshakamilika. Kulikuwa na hoja ya uhamasishaji wananchi uendelezaji wa utalii wa

ndani. Hii imesemwa na Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Zakia Meghji, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Dr. Wanyancha na Mheshimiwa Selelii.

Mheshimiwa Spika, tuna mikakati mingi tunayoifanya kutangaza utalii. Kwanza tunaendelea kushiriki katika maonyesho mbalimbali ya biashara hapa nchini. Kuna maonyesho ya utalii yanaitwa *"Karibu Fair"* kule Arusha, tumekuwa tukishiriki na kuonyesha na kutangaza vivutio vyetu Maonyesho ya Saba Saba, Nane Nane na kwa kweli kwa wale ambao walitembelea banda letu hata mwaka huu wameona jinsi ambavyo tunajitahidi kutangaza vivutio vyetu. Lakini pia katika kutangaza utalii wa ndani tumeendelea kudhamini mashindano mbalimbali ambayo pia ni njia mojawapo ya kutangaza utalii, kuna mashindano ya Mbio za Kilimanjaro, kuna Mashindano ya *Bongo Star Search* ya muziki lakini pia kuna mashindano ya aina mbalimbali ambayo wanapokuwa wakishindana tumekuwa tukidhamini na hivyo kutangaza utalii wetu. *(Makofi)*

Kuna pia vichapisho mbalimbali vimechapishwa na kusambazwa sehemu mbalimbali za nchi lakini pia tunaendelea kushirikiana sekta binafsi ili kuwashawishi watengeneze *packages* ambazo zitarahisishia wageni wetu au wanaotembelea vivutio vyetu waweze kuvitembelea.

Kuna vipindi vya redio na televisheni vinaendelea ambavyo vimekuwa vikisaidia kutangaza utalii na vivutio vyetu lakini pia kuna misafara ya Waandishi wa Habari ambayo tumekuwa tukiifadhili kila mwaka kutembelea vivutio vyetu na hivyo kutoa habari ya vivutio vyetu kwenye vyombo vyao vya habari. Shirika la Hifadhi ya Taifa *(TANAPA)* wamekuwa wakijitahidi sana kuboresha hosteli kwenye maeneo ya mbuga zao ili wageni waweze kupata *accommodation* ya bei nafuu. Kuna Basi pia ambalo linamilikiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ambalo linawasafirisha watalii kutoka mji wa Arusha kwenda Ngorongoro kila *weekend* na linafanya kazi vizuri na nafikiri mpango huu pia unaboreshwa ambalo limekuwa likifanya kazi hizo toka mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Killimbah aliyotaka Mheshimiwa Waziri azungumzie jinsi Serikali inavyojipanga kukabiliana na ushindani wa utalii katika ukanda wa Afrika Mashariki. Mkakati wetu kwanza katika kutangaza kuna mazungumzo yanayoendelea ya kuona namna gani tunaweza tukatangaza vivutio vyetu kwa pamoja. Tunategemea njia hii ya kutangaza kwa pamoja *East Africa Destination* itatusaidia kuweza kutangaza vivutio vyetu. Lakini wageni wanapofika mpango wetu ni kuhakikisha kwamba vivutio vyetu wanavitembelea kwa malipo ambayo hayawekwi katika *package* ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kama *Destination* na hivyo tunafikiri kwamba mpango huu utaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya Dr. Mwita Haji Mwita anazungumzia bandari ya Zanzibar ni ya kuvutia na hivyo inahitaji kutangazwa, ni wazo zuri tumelichukua tunalifanyia kazi. Kuna hoja ya Mheshimiwa Mariam Mfaki pamoja na Mheshimiwa Estherina Kilasi wamezungumzia tupanue vyuo vyetu ili kuweza kutoa mafunzo kwa wahifadhi wengi zaidi. Mpango wa miaka mitano ijayo ni kupanua Chuo cha Wanyamapori Mweka kinachodahili kwa sasa wanafunzi 418 kufikia 700. Lakini pia Chuo cha Pasiansi chenyewe kinapanuliwa kwa sasa hivi kinadahili wanafunzi 100 na tunategemea kitafikia angalau 150 mwisho wa mwaka ujao.

Kwa hiyo, hili tumelichukua na pia tulipendekeza na tunaendelea na mazungumzo ya kutoa mafunzo ya haraka kwa wahitimu wa JKT ili waweze pia kuajiriwa katika mtindo wa *Fast Track*. Mazungumzo yanaendelea nafikiri hilo nalo litatusaidia kuweza kupata jibu la uhaba wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi ameomba tujenge kituo cha *TANAPA* kwenye mji wa Musoma. Ni wazo zuri lakini matatizo ya kifedha kwa sasa kutokana na mtikisiko wa uchumi hayatupi nafasi ya kulifanya jambo hilo lakini tutalizingatia katika Bajeti zetu hasa kuanzia mwaka ujao wa fedha kutegemea na hali ya uchumi. Mheshimiwa Aloyce Kimaro amezungumzia kufungua njia mpya hili tulizungumza naye vizuri sana jana tukaelewana kwamba jambo hili ni zuri lakini linahitaji utafiti na utafiti unaendelea baada ya Bajeti kupitishwa ambayo ni maombi yetu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu yeye amezungumzia suala la Mabwana Nyama kuwa ni wachache na hawana usafiri. Ni tatizo lakini tunaangalia namna ya kuweza kusaidia tatizo la usafiri kwenye eneo hilo. Hili tumelichukua na tutalifanyia kazi. Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa amezungumzia suala la kupandisha ada za kuingia kwenye pori la akiba la Ugalla pamoja na wananchi kubambikiziwa kesi.

Suala la kiingilio kwenye hifadhi kwamba ni kikubwa ni kama ambacho tumekipokea ingawa kwenye maeneo mengine hatujapata malalamiko haya tunafanya utafiti kujua ni nini hasa tatizo la eneo hili kwa sababu viingilio katika hifadhi zote ni sawa lakini hapa kunaonekana kuna tatizo.

Tatizo la kubambikiziwa kesi hatuna ushahidi nalo sana kwa sababu mara nyingi mambo haya yanakuwa ni ya hisia zaidi. Kwa hivyo tunafikiri ni vizuri tukatoa elimu kwa wananchi ili waweze kuelewa na kujua mipaka yetu lakini pia kwa askari wetu ili kama kuna watu ambao si waadilifu wanaofanya mambo hayo waweze kuacha na ikibainika basi hatua kali zitakuwa zikichukuliwa.

Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni amezungumzia wafugaji wanaoingia kwenye hifadhi hutozwa faini kubwa, hili ni suala la kisheria na kanuni zake ambazo zimeweka faini hizo. Nafikiri ni vizuri tu tukiwaelimisha wasiingie kwenye hifadhi badala ya kuzungumzia faini zipunguzwe ili waingie kwa wingi kitu ambacho kitakuwa kina-*contradict* misingi ya uhifadhi.

Kaka yangu Mheshimiwa Msindai amezungumzia suala la askari wanyamapori wahamishiwe Serikali Kuu. Ni wazo ambalo sisi tunafikiri lina-*contradict* ile dhana ya *D by D* tunafikiri pengine tutafute namna ya kutatua matatizo ya utumishi wao badala ya kuzungumzia kuwahamishia kwenye Mamlaka ya Ajira.

Kwa hiyo, tunamshauri kwamba pengine atupe nafasi tuendelee kufanya kazi na wenzetu wa TAMISEMI kuona namna gani tunaweza tukaboresha au kudhibiti upungufu wa kimaadili katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, amesema pia Idara ya Wanyamapori iwe na Mamlaka. Sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009 imependekeza hivyo na baada ya Kanuni zake kukamilika basi mara moja jambo hilo litaanza kutekelezwa. Mheshimiwa Kayombo pia amependekeza kuanzisha WMA kwenye eneo la akiba la Liparamba na Litumbandyosi. Ni wazo zuri lakini utaratibu ni kwamba wananchi lazima washirikishwe na tutatumia wataalamu wetu wa eneo hili kuweza kuwahamasisha wananchi pamoja na yeye Mheshimiwa Mbunge ili waweze kuridhia kutumia ardhi yao kwa ajili ya uhifadhi badala ya matumizi mengine. Kaka yangu Luhahula sijui kama yupo, lakini alizungumzia kuchimbwa bwawa la Nsango kule kwetu Bukombe. Wazo hili ni zuri na tutalizingatia.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri sasa nitamwita mtoa hoja ambaye ndiye Waziri wa Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo kuhusu hoja walizotoa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali walipokuwa wakichangia hotuba ya Wizara yangu ya Bajeti mwaka 2009/2010. Kwanza naomba kutoa shukrani kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ikiongozwa na Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kwa kushirikiana na Wizara yangu katika kuandaa Bajeti ya mwaka 2009/2010.

Wizara ilifarijika sana kwa maelezo na maelekezo mbalimbali yaliyotolewa na Kamati hii kwa lengo la kuboresha taarifa ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuongea na waliochangia kwa maandishi kwa michango yao mizuri ambayo kwa kweli yote ina faida na ni mambo ambayo ya muhimu katika Wizara yangu. Kabla ya kuanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge naomba sasa kuwatambua jumla ya Waheshimiwa Wabunge 24 waliochangia hotuba ya Bajeti yangu kwa kuzungumza hapa Bungeni kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Msemaji wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi na Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Anne Killango Malecela, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Halima Mamuya na Mheshimiwa Kaika Telele.

Waheshimiwa Wabunge wengine ni Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo, Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mchemba, Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto na Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, naomba pia kuwatambua Waheshimiwa Wabunge 72 waliochangia hotuba yangu kwa maandishi kama ifuatavyo. Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu, Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mheshimiwa Ramadhani Athumani Maneno, Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya, Mheshimiwa Steven Galinoma na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengine ni Mheshimiwa Dr. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Dr. Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Juma Killimbah.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia kuamka nikiwa mzima. Nakupongeza wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umahiri wako wakati kutuongoza humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Hotuba ya Waziri, utajua ama utafahamu Wizara inafanya kazi nzuri ila bado iko haja kujua mapengo ama dosari zilizopo zinazotoa mianya ya walanguzi kuua ama kutukosesha kipato cha nchi yetu. Tunajua njia mojawapo ya uchumi wetu ni kupitia utalii, lakini tujue kwamba, utalii unaathiri mila zetu. Utamaduni wa nchi yetu, unatoweka siku hadi siku. Naiomba Wizara inieleze ni kiasi gani itagharimia kulinda utamaduni wetu? Mara nyingi tunasikia taarifa za wizi wa pembe za ndovu. Serikali inasema ina ulinzi katika maeneo yetu ya wanyamapori. Napenda kujua ni kitu gani kinachopelekea wizi huu ufanyike? Ninashangaa sana kuona bidhaa hizi zinatokea katika kiwanja cha ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hasara inayoingizwa nchini kutokana na magogo, utaona ni ukosefu wa Watendaji wetu kuwa hawana imani ya nchi yao. Utashangaa sana kuona magogo yetu yanaingizwa Kenya kila leo. Jambo ambalo linatoa wasiwasi mkubwa, juu ya nchi yetu na umaskini. Inakuwaje magogo yetu kuingizwa Kenya?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Utalii ni muhimu sana katika ustawi wa nchi yoyote ile. Tanzania ni nchi iliyojaliwa vivutio vingi vya utalii, ikiwa ni pamoja na Mlima Kilimanjaro, mrefu kuliko yote Barani Afrika na Ngorongoro Crater, moja ya maajabu saba ya dunia na kadhalika. Pamoja na kuwa na vivutio hivi, bado serikali imeshindwa kuboresha

vivutio hivyo, ikiwa ni pamoja na miundombinu mibovu, lakini pia ujengwaji holela wa hoteli ndani ya hifadhi zetu na hivyo kusababisha baadhi ya wanyama kuhama na hivyo kudidimiza utalii wetu na vivutio hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TANAPA* ni nyeti na lingeweza sana kuingiza pato kubwa kwa Taifa, kwani Tanzania ina mbuga nyingi sana za wanyama. Mbuga hizi zimevamiwa na hivyo wanyama wengi hupotea kwa kuhamishwa na kupelekwa nje. Sasa hivi kumekuwa hata na viwanja vya ndege karibu na hifadhi hizi ili kusafirisha wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyara za serikali kwa miaka mingi zimeibwa sana na hata majangiri hao wamekuwa wakiua wanyama ili kupata nyara hizo. Tukio kubwa likiwa ni makontena yaliyosafirishwa kwenda Vietnam na tunashukuru kuwa uongozi wa Bandari ya Vietnam walitoa taarifa. Inasikitika kuona kwamba, Uongozi wa Wizara ya Maliasili ulishindwa kugundua kontena hilo. Hii ina maana, hakuna ulinzi au kama upo basi Watendaji walishiriki katika hujuma hii. Pamoja na wizi huu wa kutisha, tumeona pia nyara nyingi zikiibwa. Tunaomba Wizara iwe makini ili tuweze kupambana na majangiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa ndani ni muhimu sana kwa nchi, lakini cha ajabu, wananchi wanazaliwa hadi kufa bila kuona utalii wao. Hali hii imechangiwa sana na gharama kubwa za usafiri na malazi katika mbuga zetu. Kuna haja ya kuwa na hoteli za gharama nafuu ili walau Watanzania waweze kuona utajiri wa rasilimali za Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maliasili ya misitu tuliyonayo, bado mbao zimekuwa zikipanda kwa kasi sana. Hali hii imepelekea wafanyabiashara kuingiza mbao toka nje. Kibaya zaidi, hata Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), huagiza nguzo za umeme kutoka Afrika Kusini. Kwa nini hali hii? Moja ya sababu ni utozwaji mkubwa na wingi wa kodi.

Mwisho, Wizara ijitahidi kuwabaini wanaochoma misitu hasa katika miteremko ya Mlima Kilimanjaro, lakini pia waboreshe miundombinu ya barabara, maji na kadhalika.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, katika dhana nzima ya uwajibikaji na kutoa haki pale ambapo mtu anayetuhumiwa na kupelekwa mahakamani kwa mazao ya misitu (mbao) na mahakama kutoa suluhishi na hatimaye mhusika asipewe mazao yake (mbao); ni jambo baya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana Makame Ali Baruti, alikamatwa na mazao ya misitu (mbao) tarehe 9 Januari, 2006 na kufunguliwa kesi Namba CC/328/2006 – Mahakama ya Temeke na kesi ilimalizika mwaka 2007. Mshtakiwa alitakiwa kupewa mbao zake, ambazo zilikuwa jumla 1981. Kwa tathmini ya maliasili wakati huo, ilikuwa shilingi milioni nane, lakini hali halisi ya kibiashara ni zaidi ya shilingi milioni kumi na mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Makame Ali Baruti mbao zake 1981 zimechukuliwa? Japokuwa ni chache, apewe haki ili kuheshimu Mahakama; au kuna siri gani au ubadhirifu? Naomba nipatiwe jibu wakati wa majumuisho, kwani nimeshamfikishia tatizo hili Mheshimiwa Naibu Waziri, nimekwenda Wizarani na kijana mhusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri serikali itangaze zaidi utalii katika mambo ya hifadhi ya kale kama mapango na magofu; kwa mfano Mafia, Kilwa, Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri serikali iongeze kiwango cha kifuta machozi kwa mtu anatakayejeruhiwa angalau kifikie Sh. 500,000 na atakayeuawa na mnyamapori basi serikali itoe kifuta machozi cha Sh. 2,000,000.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wasaidizi na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii, kwa kazi ngumu lakini nzuri sana wanayoifanya; *keep it up.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu wa miti kwa matumizi ya ujenzi na kuni na kadhalika katika maeneo mbalimbali nchini, nashauri Wizara ichukue hatua za makusudi na endelevu za Ofisi za Maliasili (W) kuwa na vitalu vya miche na iwe lazima kwa taasisi zote za serikali, kupewa idadi maalum ya miti ya kupanda kila mwaka, hasa wakati wa masika. Taasisi hizi ni pamoja na Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo, Zanahati, nyumba za watumishi wote, Mahakama za Mwanzo na Wilaya, Ofisi za Mifugo, Ofisi za Vyama vya Siasa. Ofisi za Vyama vya Ushirika na kadhalika. Ukiongezea pia na taasisi zote za watu binafsi na wananchi kwa ujumla; kupanda miti. Uhamasishaji uwe mkubwa zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. Bei za miche ziwe chini, kiasi kinachowezekana ili wananchi wengi zaidi waweze kumudu. Utaratibu wa sasa wa siku moja ya kupanda miti kitaifa, bado haitoshelezi kwa kuwa tarehe hiyo maeneo mengi nchini huwa yako kwenye kipindi cha ukame.

Wizara isikilize kilio cha wananchi wanaosumbuliwa na wanyama wala watu (mamba) na kadhalika na waharibufu wa mazao (viboko), sehemu mbalimbali hapa nchini. Katika Jimbo la Magu kwa mfano, mamba hula sana watu kandokando mwa Ziwa Victoria na kando kando mwa Mto Simiyu, hasa sehemu mto huu unapoingia Ziwani.

Taarifa zilizopo, mamba hawa wamezaliana sana na hivyo kuwa tishio kubwa kwa watu. Kupungua kwa samaki Ziwani na kufyekwa maeneo mengi ndani/kanda kando mwa Ziwa, zimefanya wanyama hawa watawanyike kila mahali. Naomba Wizara ifanye kampeni maalum ya kuwavua mamba hawa.

Viboko wameenea sana maeneo haya na pia katika vijiji vinavyozunguka hifadhi ndogo katika Vijiji vya Salama, Sayaka na kadhalika. Wananchi wanaomba sana Serikali (Idara), iende Kijii cha Salama, Kata ya Ng'haya, Jimbo la Magu. ikawavune viboko hawa. Wanasababisha madhara makubwa sana kwa mazao ya wananchi. Wananchi wamepanda miti na kuikuza wao wenyewe, wanapoamua kuikata kwa ajili ya kujengea nyumba zao ama kuchoma mkaa na kuuza ili kupata fedha kwa ajili ya matumizi kama vile kulipia ada, kuchangia maendeleo ya vijiji/kata, kwa nini wanakamatwa na kutaifishiwa mbao/mkaa na baiskeli?

Watu hawa ni maskini na uonevu kama huu unawadidimiza zaidi kwenye dimbwi la umaskini. Kama lengo ni kulinda mazingira; kuzuia ukataji ovyo wa miti, ndiyo maana nimeshauri spidi ya kukata miti na spidi ya kukamata wakataji wa miti, iende sambamba na spidi kubwa zaidi ya miti kupandwa kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kazi nzuri wanayofanya kwa niaba ya taifa zima. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara. Nawatakia ari mpya katika majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielekeze mchango katika maeneo yafuatayo:-

Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Chuo cha Misitu Olmotonyi, kilipangiwa kiasi cha Sh. 380,000,000, mbali na kwamba, fedha hizi pia hazikuletwa zote. Ongezeko la wanachuo, limefanya mazingira ya uendeshaji wa chuo hiki kuwa mgumu sana. Kana kwamba haitoshi, bajeti ya mwaka huu imepungua mpaka Sh. 250,000,000. Upungufu wa takriban Sh. 130,000,000. Hali hii husababisha baadhi ya shughuli kusimamia na ni kasoro kubwa sana na haivumiliki.

Naomba Wizara hii, hususan Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Maliasili na Utalii, atoe upendeleo wa pekee kwa Chuo hiki muhimu katika kuandaa wataalam wa misitu na Nyuki. Zitafutwe fedha za kufidia upungufu huu (nakisi) ya kibajeti. Nitapenda kupata maelezo ya kina juu ya hali ya Chuo hiki cha Olmotonyi. Wafanyakazi wa Chuo hiki, kama walivyo wafanyakazi wengine katika nchi hii, wanastahili kupata motisha kwa kazi yao nzuri ya kufundishwa na kutunza mazingira na maliasili za taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa Olmotonyi wanaishi kwenye nyumba zilizochakaa na zilijengwa wakati wa ukoloni. Hata hivyo, bado wanakatwa *house allowance.* Nashauri serikali iache kuwakata watumishi hawa *house allowance* na nyumba wanazoishi iwe ni motisha ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, apokee ombi la kilio cha wafanyakazi wa Olmotonyi ili wasamehewe kulipa kodi ya nyumba ambazo wanaishi sasa ili iwe motisha kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, kwa ushindi wa Ubunge. Ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, naomba kuwashukuru sana GTZ na Hifadhi ya Pori la Selous, kwa kutusaidia ujenzi wa miundombinu. Selous wametengeneza barabara kadhaa, ambazo zimo katika vijiji vinavyozunguka Pori la Hifadhi ya Selous. Pengine ni jambo jema kutamka waziwazi kwamba, wametengeneza madaraja kama ya Mto Mgeta na vidaraja saba kati ya Gomero na Kisaki Station. Utawala wa Pori la Selous wanashirikiana vyema sana na wananchi kupitia Jukumu, ambacho ni chombo cha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba, Wizara sasa inasaidia wananchi katika kutayarisha na kupitisha katiba mpya ya Jukumu, kwa madhumuni ya kuwapatia wananchi hawa kupata WMA. Hapa lazima nitoe tahadhari kwamba, Katiba mpya ambayo inasaidiwa kutayarishwa na serikali yenyewe. Katiba hii mpya lazima ipitishwe na kila kijiji ili isije ikagomewa na baadhi ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mahusiano kati ya Wizara ya Maliasili na Halmashauri zetu. Wawindaji wanatakiwa kuelekezwa na Wizara, kuripoti Wilayani kwanza na wakati wa kuondoka ili kuhakiki kinachowindwa na nyara zinazochukuliwa.

Nakala za leseni ya kila mwindaji, sharti ibakizwe Wilayani, kama kitalu hicho kipo Pori la Akiba, Afisa Wanyamapori Wilaya, ambaye pori hilo lipo ni budi apate taarifa ya uwindaji na kupata vivuli vya leseni zilizotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo hayo mawili niliyoyataja hayafanyiki, kwani Wafanyakazi wa Wizara wanaviita "Siri ya Wizara". Hili linatoka wapi? Ili kudhibiti kipato na mwenendo mwema wa uvunaji wa maliasili yetu, hili lazima lifanyike na Wizara iache ukiritimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Idara ya Misitu, kuna utata zaidi. Wananchi wanapanda na wanatunza maliasili yetu, lakini jambo la kushangaza ni kwamba; wakati wa kuvuna Wilaya yote hawana mamlaka ya kusimamia uvunaji. Vibali vya uvunaji vinatolewa na Mkoa. Nyundo za kugonga mbao zipo Mkoani. Wavunaji wa maliasili hawa wanatoka Mkoani na kwenda moja kwa moja kwenye misitu na kuvuna, wakati wananchi wanaangalia na kuchukizwa kwa vitendo hivi na hivyo kuamua kutoitunza misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE OSLER KATAGIRA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Timu nzima ya Wizara, kwa kuandaa bajeti na kuiwasilisha, lakini hasa kwa wanavyoendesha shughuli za Wizara.

Kumekuwa na matukio ya kuchoma manyatta na nyumba za wafugaji ili kuwahamisha kwa kuwa wamevamia mbuga. Nashauri katika hali kama hii, busara itumike, ili wananchi

wasionekane wanadhalilishwa na hivyo kujenga uhasama wa kudumu kati ya wananchi wawekezaji ambalo siyo suala zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nami nafasi nichangie kidogo katika hoja iliyopo hapa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na waliozungumzia misitu (mti) na kwamba, unatozwa kodi nyingi sana. Walitolea mfano wa Kiwanda cha Saw Hill – Iringa. Zile kodi za VAT (20%); toka mti ukiwa porini kuna 20% kwa gogo na kuwa kodi nyingi sana unaposafirisha unalipa kodi lukuki mpaka kufikisha sokoni, mbao inauzwa bei ghali sana. Mzigo huu wa kodi analipa mwananchi ambaye ni mlala hoi na kusema kweli hana, mlo wake ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka kuwapatia maendeleo wananchi wetu, yaani wajenge nyumba bora, waondoke kwenye nyumba za tembe, maana yake mlango au milango yake lazima iwe ya mbao. Mbao hii ambayo hadithi yake nimeieleza hapo juu. Akiweka mlango wa bati au debe kweli ndio maendeleo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba serikali itoe kodi au ipunguze ili wananchi wamudu bei ya mbao za nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ilani ya Uchaguzi 2005, tunasema tutapeleka umeme vijijini. Sasa kupeleka umeme vijijini/mjini au Makao Makuu ya Wilaya zote, kwanza kabla ya kuunga waya, tunahitaji nguzo za kuwekea nyaya za umeme. Hizi nguzo kutoka SAO Hill ni ghali kwa sababu ya kodi hizi; ni ghali kuliko nguzo zinazotoka Afrika Kusini. Hivi kwa nini ziwe ghali kuliko za nje? Tumeangalia na kuona kuwa, kitu chetu lazima kiwe rahisi kwani hatuna gharama za usafiri toka nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba serikali yetu ipunguze au itoe kodi na iangalie kwa nini wenzetu mbao au nguzo zao ziko bei poa ili nasi tutumie mbao au nguzo zetu za Tanzania. Kwa njia hii tutafanikiwa kufikisha umeme vijijini. Kwa lugha nyingine, isiwe sababu ya ughali wa mbao au nguzo zetu kushindwa kutekeleza ahadi zetu au malengo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa zikiuzwa bei poa au chini ya bei ya mbao au nguzo toka nje, sote tutapata maendeleo na mwisho wa siku maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa Chuo cha Nyuki Tabora kukumbukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa asali nyingi ya Tabora inatoka katika moja ya Kata za Jimbo langu, nayo ni Kata ya Maambali. Utashangaa kuna hata nchi jirani kama Burundi na Rwanda, wanakuja kununua asali pale Maambali na wananunua kwa bei poa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, naomba serikali waweke kiwanda ili Wanyaruanda wakija wanunue iliyo-*be packed*, yaani *added value* ili wananchi waondokane na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Shamsa Mwangunga (Mb) - Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu wake - Mheshimiwa Ezekieli Maige (Mb) na Katibu Mkuu - Dkt. Ladislaus Komba, kwa kazi nzuri waliyofanya katika utayarishaji na kuwasilisha Hotuba hii ya Bajeti. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imebarikiwa maliasili nyingi na zenye thamani kubwa. Maliasili hizi ni tete kweli kweli *(very fragile).* Misitu yetu inaondoka kwa haraka mno na kuondoka kuna athari kwenye hali ya hewa, uoto wa nchi na utajiri wetu. Wakati umefika tuitumie kushiriki katika carbon trade na biashara hii ifanywe na Idara ya Misitu; tulirudishe jeshi la kulinda misitu *(forest guards)* kama ilivyokuwa kabla ya mwaka 1990; Mfuko wa Kulinda Misitu kama

ilivyopendekezwa katika *Forest Act, 2004*, uanzishwe ili kulipia jeshi la kulinda misitu na *management* ya misitu; Hifadhi zote za misitu za kupanda na za asili ziwe na uongozi, zijenge miundombinu na hifadhi, kupanda miti, kufanya inventory na *controlled harvesting.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujangili katika mapori yetu unaongezeka katika mapori ya wazi, mapori tengefu na katika Hifadhi za Taifa. Ni vizuri juhudi za ulinzi ziongezwe. Kama juhudi za ulinzi hazitaongezwa; si muda mrefu kutoka sasa, wengi wa wanyama wetu watatoweka. Tutakuwa kama Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina rasilimali kubwa sana ya nyuki. Aina za nyuki (Epis melifera na varieties zake) ni nyingi Tanzania kuliko eneo na nchi yoyote Duniani. Uharibifu wa ecologia katika maeneo muhimu wanapokaa nyuki inatishia aina, uwingi, maficho na malisho ya nyuki. Aidha, wakati umefika kuhifadhi kwa nguvu zaidi Misitu ya Miombo, Misitu katika Mabonde makubwa ya mito yetu, Mbuga za Majani zenye umuhimu kwa nyuki na Mradi mkubwa wa ufugaji nyuki uanzishwe ili kuwaongezea wakulima njia mbadala wa mapato na tutumie ufugaji nyuki kulinda hifadhi zetu. Kama wananchi wana mizinga yao ndani ya misitu, mbuga au eneo lingine, hawawezi kulichoma moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba TANAPA katika mahusiano yao na jamii, wawasaidie majirani zao wa Mgagao, Pangaro na Karamba katika Wilaya ya Mwanga. Vijiji hivi vimepakana na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia na kumi.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa hotuba nzuri sana. Pia nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuitembelea Wilaya ya Karagwe na kujionea hali halisi ya uharibifu wa mazao/mashamba ya wananchi, unaofanywa na tembo. Nashukuru kwa gari la wanyamapori tulilopewa Wilaya ya Karagwe. Linatusaidia lakini halitoshi, kwani maeneo yanayoshambuliwa na tembo ni mengi na Wilaya ni kubwa mno. Hivyo, tunaomba magari zaidi kama manne au matano. Pia wataalam wa wanyamapori waongezwe kwani hawatoshi. Mafuta ya kuendesha magari ni kidogo nayo pia yaongezwe ili yaweze kukidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyamapori hasa tembo, wamezagaa Wilaya nzima ya Karagwe na wanazidi kuzaliana na kuwa tishio. Siku zote nimeomba vituo vidogo vya wanyamapori vijengwe, hasa maeneo ya Kata ya Nyakakika, Nyakasimbi, Kihanga na Ndama. Tatizo hili ni kubwa, naomba litafutiwe ufumbuzi wa kudumu kabla ya mwisho wa 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Kimisi imemega kwa kiasi kikubwa, maeneo ya Wananchi wa Kata za Nyakasimbi, Nyakakika na kadhalika. Wananchi wamekosa maeneo ya malisho na matumizi mengineyo. Hivyo, tunaomba sana eneo hilo limegwe kwa kilomita tano kuingia ndani ya hifadhi. Jambo hili ni muhimu ili kuondoa tatizo la wananchi kulisha mifugo yao ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Oktoba, 2008, nilileta swali hapa Bungeni lililouliza kwamba; je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza viwango vya mapato yatokanayo na vitanda ili sehemu fulani iende moja kwa moja kwenye Halmashauri zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya *reference* ya Hansard ya Mkutano wa 13 na Kikao cha Nne cha tarehe 31 Oktoba, 2008. Majibu ya Waziri yalikuwa mazuri sana kwamba; Wizara inaandaa utaratibu mpya utakaotumika hivi karibuni. Utaratibu huu ni kama ifuatavyo: Mgawanyo utakuwa 80% kwa ajili ya Halmashauri na Jumuiya za Wananchi (Halmshauri 15% na 65 Jumuiya za Wananchi na 20% tu ndiyo itakwenda Serikali kuu); na kwamba % hizo ni kwa mapato

yote ya makusanyo ya ada, ikiwa ni pamoja na *bed night fee.* Hivyo, utaratibu huu utaongeza mapato kwa wananchi na Halmashauri, ikiwemo Halmashauri yangu ya Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua ni kwa nini hadi sasa utaratibu huu haujaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kujua ni sababu zipi zinakwamisha utaratibu huu, ambao unasubiriwa kwa hamu kubwa na Halmashauri zetu, ikiwemo Halmashauri yangu ya Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri anieleze nini hatma ya wakulima wangu wa Serengeti ambao wameliwa mazao yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii. Hotuba ni nzuri, naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Wana mtazamo na dira nzuri sana. Vilevile Katibu na Watendaji wote ni wachapa kazi, dosari kama zipo ni ndogo sana ambazo zinarekebishika. Vijiji vimenituma mimi Mbunge wao niwatetee juu ya adha wanayopata Wananchi wa Vijiji vya Mambegu, Malangali na Mpanga mpya katika Kata ya Luguda Wilaya ya Njombe, wanatishiwa kuwa wako ndani ya Hifadhi ya Mpanga-Kipengere. Ukweli ni kwamba, tayari walishahama na kulipwa fidia, hata kama ni ndogo. Walihama mara ya kwanza, tena wanasema wahame mara ya pili wakati huo hawamshirikishi Mbunge wala Diwani wa Kata husika. Naomba Waziri atoe tamko la kutowahamisha wananchi wangu, kwani wanashindwa kushiriki shughuli za maendeleo.

**MHE. ALOYCE BENT KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri *concession fee* zibakie dola 25 kama wadau walivyokubaliana 2007. Kama *camping* ni dola 20 hadi 60; iweje hoteli zilipe kiwango kidogo hivyo?

Tuanze na dola 25, lakini lengo liwe dola 100 kulingana na hadhi ya hoteli. Hoteli yenye nyota tano haiwezi kulingana na nyota mbili ama *camps.* Kama ni kupunguza, basi tupunguze *park entries,* lakini wakishaingia ndani tuwatumie sana na kupate ushuru mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magogo bado ni tatizo. Misitu inaangamia na wanaoiangamiza ni wageni. Kupiga marufuku *export* ya magogo haijasaidia kwa kuwa sasa wana-*export* mbao. Nashauri ushuru wa *export* wa mbao uwe mkubwa ili kuwalazimisha wawekezaji waanzishe viwanda vya fanicha hapa hapa, tuajiri watu wetu. Kama hawataki tuache misitu yetu iendelee kunawiri na kuhifadhi mazingira.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuipongeza Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuendeleza maliasili zetu pamoja na utalii.

Pamoja na pongezi hizi, napenda kuwasilisha hoja na maombi ya Wananchi wa Manyoni Mashariki.

(i)Ili kuendeleza Kizigo/Mhezi Forest Reserves, Halmashauri ya Wilaya na Wananchi (Vijiji) wanaozunguka hifadhi hizi, wapewe 25% ya mapato yatokanayo na uwindaji. Mapato haya ni kidogo na huletwa katika mtiririko usiotabiriwa. Ombi ni kuongeza asilimia ya mapato na yaletwe katika mtiririko wa uhakika.

(ii)Wananchi hungiliwa na wanyama waharibifu mara kwa mara, lakini Idara ya Maliasili katika Halmashauri ya Manyoni hawana gari na wakati mwingine hawana hata risasi. Kikosi cha Kupambana na Majangili (KDU) kilichopo Manyoni, nacho kimeelemewa na shughuli. Ombi ni kuimarisha Idara ya Maliasili kuwapa gari.

Wananchi wa Wamanyoni wamepata mwamko wa ufugaji wa nyuki. Aidha, asali ya Manyoni mwaka 2007/08, iliwahi kupata *gold medal* kwa ubora. Ombi ni kwamba, Wizara iongeze uwezeshaji wa kukuza zao hili kwa kufanya yafuatayo:-

(iii)Kushirikiana na Halmashauri kuanzisha vitalu vikubwa vya miche ili kuongeza kasi ya upandaji miti katika Wilaya ya Manyoni.

(iv)Tunapongeza jitihada za Wizara katika kuendeleza na kuboresha ufugaji wa nyuki. Tunaomba Wizara ishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ili kuvutia uwekezaji katika kuanzisha kiwanda cha kusindika na kusafirisha asali.

(v)Tunazidi kushirikiana katika kampeni ya ufugaji bora wa nyuki ili kuongeza mapato ya wananchi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kutoa pongezi kwa Wizara hii, kwa kazi nzuri ya kuitangaza Tanzania, kwa lengo la kupata watalii wengi zaidi na mapato makubwa zaidi.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja linanikera sana moyoni mwangu, sio lingine bali ni mazingira ya uuzaji wa Moshi Hotel. Habari ambazo ninazo, hii hoteli aliuziwa Bw. Frank Marealle na alilipa Sh. 165 milioni. Alinyang'anywa na kupewa Impalla Hotel kama fidia ya Hoteli ya 77 aliyokuwa ameshinda tenda, lakini akanyang'anywa na kupewa Hotel KEMPISK. Impala, akafidiwa kiasi cha pesa na kupewa Moshi Hotel kama fidia ya Hotel 77 aliyonyang'anywa. Yote haya yamefanyika bila utaratibu wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi naandika barua hii, mnunuzi wa kwanza Bw. Frank Marealle, ambaye ndiye mnunuzi wa kwanza, hajaarifiwa ni nini kinaendelea na wala hajarudishiwa pesa zake alizokuwa amelipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri alieleze Bunge lako Tukufu ni utaratibu gani ulitumika kumpa Impalla hiyo hotel na hatima ya Frank Marealle. Watu wa Moshi wanataka kujua, kwani Moshi Hotel ni kitega uchumi kikubwa, kilichokuwa kinatoa ajira kwa zaidi ya watu 200 wakazi wa Mjini Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri aifungue njia ya Old Moshi Kidia ili kufungua Utalii kwa Wakazi wa Moshi Mjini ili wawe wanaweza kwenda kwa one day trip. Hii ndio njia iliyo karibu kuliko njia nyingine zote. Pia katika njia hii, kuna ziwa lililo kwenye altitude ya juu kuliko ziwa lolote duniani. Hili ziwa lingekuwa kivutio kikubwa kwa watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naambatisha hapa Paper 1 na 2 ya Gazeti la The Guardian la tarehe 19 Aprili, 2009; story inayozungumzia kwa undani jinsi Moshi Hotel ilivyotolewa bure kwa Impala na Marealle hajalipwa hata senti moja.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Hongera Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wote.

Napinga kauli ya Mbunge wa Ngorongoro kuwa, watu wasihamishwe Ngorongoro. Wahamishwe hata kama ni wote; basi wabaki wachache.

Kilimo *completely* ni marufuku na msilifanyie mzaha hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAKIA H. MEGHJI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Viongozi wa Taasisi na Wafanyakazi wote, kwa kazi nzuri. Napenda pia kumpongeza Waziri, kwa hotuba nzuri.

Napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Suala la utalii wa ndani *(Local Tourism),* inabidi litiliwe mkazo. *Experience* ya kuyumba kwa uchumi duniani, inaonesha *impact* katika utalii wetu kwani zaidi tunategemea watalii kutoka nje. Jambo muhimu katika mkazo ni miundombinu katika hayo maeneo. Bila ya miundombinu, wananchi hawawezi kufika katika maeneo mbalimbali. Jambo muhimu kuangalia ni jinsi gani utalii wa ndani utatoa mchango katika uchumi wetu. Ni kweli wananchi wanapaswa kutembelea maeneo yao, lakini pia ni kweli kuwa serikali lazima ipate mapato. Wawekezaji hasa wa ndani, wahamasishwe kujenga hoteli za kawaida ambazo wananchi watamudu gharama. Mabenki yatoe mikopo na hoteli zijengwe katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha utalii wa ufukwe, ni muhimu kwa wawekezaji waweze kupata maeneo ya kuwekeza katika maeneo haya. Hivi sasa kuna baadhi ya wananchi na wawekezaji, wamehodhi maeneo hasa ya fukwe za pwani. Ni muhimu kwa Wizara kushirikiana na Wizara ya Ardhi ili maeneo haya yaachwe kwa ajili ya ujenzi wa hoteli, kumbi za mikutano na kadhalika.

Kuimarisha utalii wa mikutano – *Conference Tourism*. Sote tunajua kuwa njia mojawapo ya kuingiza mapato serikalini ni kutilia mkazo ujenzi wa kumbi za kisasa za mikutano. Hivi sasa mikutano mingi inabidi ifanyike Arusha, kwa kuwa kuna *Arusha International Conference Centre*. Kwa hiyo, uwekezaji wa kumbi za kisasa Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Kilimanjaro na kadhalika utiliwe mkazo.

Kuhusu suala la kupanua mipaka ya hifadhi au kuanzisha hifadhi; ili kuondokana na migongano na wananchi, ni vizuri wakati wa mchakato basi wananchi washirikishwe kikamilifu. Wakati huu ni muhimu kuwaelimisha wananchi juu ya faida ya uhifadhi.

Katika suala ya WMAs, jambo muhimu la kutiliwa mkazo ni kuimarisha WMAs, lakini pia wananchi wapate uelewa mzuri.

Mafunzo lazima yatolewe katika masuala ya *Business Plan,* lakini pia jinsi ya kutunza fedha na mapato kwa ujumla, wakati WMAs hivi sasa baadhi yao wanapata fedha nyingi. Haisaidii wananchi kwa fedha hizi kubaki benki tu. Ni muhimu fedha hizi ziweze kutumika kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. *Concept* ya WMA itakuwa tu na maana, ikiwa wananchi watasimamia wanyamapori na kuleta maendeleo.

Kutokana na tatizo la miundombinu, TANAPA kwa kutumia ndege ya Caravan wanaweza kuanza kufanya biashara ya kupeleka watalii Kusini. Hili lilifanyika hata kule Kaskazini pale mwanzo kwa kutumia magari ya TANAPA. Nina hakika baada ya hapo, wafanyabiashara wengi wataanza safari za kupeleka watalii kusini ili kutilia mkazo Utalii wa Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kukupongeza na naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakuomba niwapongeze Waziri wa Maliasili na Utalii - Mheshimiwa Shamsa Mwangunga (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara – Dkt. Ladislaus Komba, pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Binafsi, nikiri kwamba, juhudi kubwa inafanyika katika kuibua vivutio mbalimbali pamoja na kuvitangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, naomba nimuulize Waziri kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Sera ya Utalii ya Mwaka 1997, Sheria Na. 10 ya Mwaka 1964 iliyofanyiwa marekebisho na kuwa Sheria Na.22 ya 1979 ya Mambo ya Kale. Inasema kuwa, kitu au eneo linaweza kutangazwa kuwa urithi wa mali kale endapo kutakuwa na ulazima wa kufanya hivyo na Waziri ataamua kutangaza, lakini itaingia *automatically* pale itakapokuwa imefikia miaka 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Waziri yaliyonifurahisha ya kupandisha hadhi ya Makumbusho ya Majimaji; je, ni lini Mji huo wa Songea utatangazwa kuwa ni mji wa kihistoria na kishujaa kwa ajili ya watalii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza kazi ya utalii katika Mkoa wa Ruvuma; ni vyema Wizara yako iwasiliane na Wizara ya Mambo ya Nje ili iwafuatilie wenzetu Wajerumani, kuwa tusahau ile historia mbaya ya kuuana/kunyonga iliyofanyika wakati huo wa vita ya majimaji; na badala yake, wakumbuke thamani waliyoiona wakati huo na hivyo kuwezesha kusaidia miundombinu ya mji huo, kama vile barabara ili hata watoto wao waendelee kuona Songea/Ruvuma ni mahali pazuri pa kuwekeza.

Vile vile Waingereza tuliwasaidia katika Vita Kuu ya II ya Dunia (1939 – 1945). Jumla ya watu wetu (askari) 270 waliuawa; watatu kati yao wakiwemo wanawake; Hadija Ali Juma Bakari SNO. DT. 190796 akiwa CPL, Hadija Y. S. Mbalamka Service No. TMN. 104189 (PTE) na Sophia Salehe S. Ngwelegulile (PTE); wote hao wanaonekana kuwa na asili ya Tunduru.

Chifu aliyesifika na kuwa na nguvu sana na hivyo kusikilizwa na wenzake; Chifu Kundenda alikuwa mwanamke.

Hivyo, Mkoa wa Ruvuma kuwa na historia nzuri ya kuthamini wanawake katika uongozi na kazi maalum kama za uaskari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma una historia ya kuenzi wanawake kwa kuvipatia vijiji au miji ya ukoo, majina ya wanawake; mfano, akina Komba (Wamatengo), wanawake ni akina Kitonda na kuna kijiji chao cha Kitonda kule Mbinga. Hali kadhalika, Pelekano, Ughano, Ngindo na kadhalika. Vile vile katika kufuata jinsia ke/me, Mkoa wa Ruvuma una mawe makubwa sana, ambayo huwezi kuyazunguka kirahisi, jiwe (me) linaitwa Mbuji na jiwe (ke) linaitwa Mweyelo; ni vivutio sana.

Biashara ya watumwa ilipopigwa marufuku maeneo mengine hasa ya kati, Waarabu waliendelea kufanya biashara hiyo katika maeneo ya Tunduru mpaka Lituhi (Nyasa) mpaka miaka ya 1902 – 1908. Hivyo ni vyema pia kutambua *route* hizo kama ilivyofanyika katika *route* ya kati.

Jengo la Halmashauri ya Songea Mjini ni sehemu ya maboma anzilishi ya Wajerumani. Kanisa la kwanza kusini (Ruvuma), lilijengwa Peramiho. Kama ilivyo sasa, makanisa ndio yalifanya kazi ya kuwekeza katika taaluma na hivyo kuwekeza katika Elimu na Afya. Lakini Serikali ya Captain Klips na Camisa Hatmen Douglus 1897, iliomba msaada wa wataalam kuendesha utawala kutoka Bishop Antony. Jina Tanganyika na mipaka yake imo katika historia hii, yaliyopelekea kurekebisha mipaka ya Mkoa wa Ruvuma na Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marehemu Baba wa Taifa alisema toka mwaka 1958 kwamba, ujengwe mnara utakaowakumbuka mashujaa wetu, wazee waliopigana vita vya majimaji hawakuwa waasi, bali walipigania haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii itasaidia vipi kusukuma suala la ujenzi wa kisima cha mafuta ya ndege au tenki ili kuwezesha ndege kutua Songea na kuwezesha kukuza utalii? Kwani kiwanja ni kizuri ila tatizo ni mafuta.

Mwisho, nilielezwa na Ndugu Masika wa South Africa, kuhusu uandaaji wa Mashindano ya Kombe la Dunia, yatakayofanyika South Afrika. Je, tumeshaanza maandalizi kama bado tunangoja nini?

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nashukuru kwa kutoa ruhusa ya kuweza kuwasilisha mchango wangu kwa njia ya maandishi. Pamoja na shukrani hizo, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri. Aidha, nitoe pole nyingi kwa changamoto nyingi, wanazokumbana nazo ndani ya Wizara hii. Pamoja na kuwa wanafanya kazi nzuri, ushauri wangu ni kwamba, wawe jasiri katika kupambana na changamoto, wafanye kazi yao kulingana na ujuzi walionao, watambue kuwa wako katika Wizara nyeti na yenye rasilimali nyingi.

Baada ya hayo, naomba nitoe mambo machache yanayohusu Mkoa wangu wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida una Game Reserves zifuatazo: Rungwa, Mhesi, Kizigo na kadhalika, zote hizo zina-cover 60% ya Wilaya ya Manyoni kwa eneo. Nasikitika kuwa, mchango mkubwa unaopatikana kuchangia taifa, bado ni 25% ya mapato yote ndio hulipwa Halmashauri; kiasi hiki ni kidogo sana. Pamoja na udogo wa mchango huo, bado fedha zile hazifiki kwa mtiririko unaoeleweka. Hivyo, maombi yangu ni kwamba, tuongezewe kiasi cha 25% hadi 35% to 40% na pia zije kwa wakati unaoeleweka.

Jambo la pili ni wanyama waharibifu. Kumekuwa na wanyamapori waharibifu katika maeneo yaliyopo karibu na Game Reserves hizi. Wanyama wanakula mazao ya watu, pia wengine wanadhuru binadamu. Hali hii inatokana na uchache wa askari wa maliasili, pia hawana silaha za kutosha na walio na silaha, wakati mwingine wamekuwa hawana risasi. Kituo cha Maliasili Manyoni hawana gari; hivyo kazi inawawia vigumu sana. Hivyo, naiomba Wizara itutazame kwa jicho la huruma itupatie vitu nilivyovitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida una vivutio mbalimbali mfano, Boma la Wajerumani – Ibasa/Mkalama; na Njia ya Dr. Livingstone, Route inapita Kilimatinde – Itigi – Tabora.

Hivyo, ninaoimba Wizara inapotazama vivutio vipya ni vyema ikavitazama na hivi na kuvifanyia *promotion* ili wananchi wa eneo husika wafaidike navyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwa mzima na kuweza kutoa mchango wangu kuhusu Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukupongeza wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wako wote, kwa jinsi mnavyotuvumilia katika michango yetu na kuendesha Bunge kwa *speed and standard.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wake wote, kwa jinsi walivyoiandaa hotuba hii kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu, ametujalia kila sifa nzuri za nchi hii ya Tanzania, kwa kuwa na mabonde, milima, mito, maziwa, wanyamapori wa kila aina na mandhari nzuri ya kupendeza ya kuweza kuwa kivutio kizuri na kikubwa kwa nchi yetu. La kusikitisha zaidi, nchi imo katika *list* ya nchi maskini duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tungepanga mikakati mizuri ya nchi hii, basi sisi tusingekuwa katika *list* ya umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wa sekta hii, kwa kweli hali inasikitisha sana, kwani utalii wetu unawanufaisha zaidi mataifa ya nje kuliko sisi wenyewe ambao Mwenyezi Mungu ametujalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa sana kusikia kama Rais amepunguza *Visa* na kuwa 50; naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwani *Visa* ni $ 50 tangu mwanzo sasa wanalipa $ 50; ndio wamepunguza au ndio bei ya kawaida; kama wamepunguza basi ingekuwa $ 25 tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya zaidi ni watalii wanaolipa nje ya nchi, kiasi kwamba kinaikosesha nchi hii mapato makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoteli ni ghali sana, kiasi mtalii wa ndani anashindwa kulala katika hoteli hizo halafu tunasisitiza Watanzania wafanye utalii; kweli watamudu hali hii na watu wa ndani ni maskini sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba serikali iwawezeshe wawekezaji wa ndani ili na wao waweze kujenga hoteli ambazo zitakuwa ni rahisi na Watanzania waweze kuwa watalii ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba serikali iwe na dhamira ya dhati kwa kuwaletea maisha bora kwa kila Mtanzania, isiwe na longolongo ya kuwanyanyasa wafugaji kwa kuwanyang'anya sehemu zao za kufugia kwa kugeuza sehemu hizo kuwa sehemu za Hifadhi ya Taifa na hao wananchi wakiendelea kuteseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna ulazima wa kuwahamasisha, basi serikali iwaandalie mahali pazuri na vile vile kuwalipa vizuri ili pasiwe na mizozo isiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuvuna misitu, yaani magogo yanayopelekwa nje bila ya kibali, yanapita njia za panya; hivi kweli serikali haina habari maana gogo si kitu cha kuweza kukificha ni lazima usafirishe kwa kutumia container, lakini utashtukia magogo yako China na serikali haina habari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba serikali izidi kujipanga kwa kuziba mianya ambayo inatupotezea mapato ya taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu, nakushukuru sana.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya makaridio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2009/10 kwa asilimia mia moja. Nawapongeza Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga (Mb), Waziri wa Mawasiliano na Utalii na Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na Timu yao yote ya Watendaji wa Wizara, kwa kazi nzuri na usikivu walionao katika kutatua matatizo ya Wizara na usimamizi wa kuhakikisha kuwa, malengo yamefikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Wizara kwa kuyapokea malalamiko ya Wananchi wa Mbarali kuhusu mipaka ya maeneo yaliyoingizwa kwenye Hifadhi ya Taifa Ruaha Usangu na kuyafanyia kazi. Ombi ni kutaka kujua ni lini timu aliyoahidi Mheshimiwa Waziri, ataituma Mbarali ije kumaliza migogoro hiyo kwa kuwashirikisha wananchi kabla ya masika kuanza ili kuweza kuyafikia maeneo hayo kwa urahisi?

Pili, wakati wa majadiliano ya muda wote inaonesha kuwa, Serikali au Wizara imetoa pesa nyingi za kuwafidia wananchi walioathirika na upanuzi wa hifadhi hiyo, zaidi ya kiwango kilichopangwa kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la fidia bado ni kubwa sana, viwango vilivyolipwa vimekuwa vikilalamikiwa sana. Baadhi ya wananchi walipewa fidia ambazo hazikuweza hata kuwafikisha walikotakiwa kuhamia na kuanza maisha mapya. Ninaomba kujua ni mkakati gani uliopo ili tuweze kumaliza tatizo hili, hasa kwa kushughulikia malalamiko yaliyokwisha hakikiwa na Halmashauri na TANAPA tu?

Chuo cha Wanyamapori cha Mweka ni muhimu sana, kama Waziri alivyokisemea kwenye hotuba yake; chuo hiki bado kinahitaji ukarabati na usimamizi wa karibu sana ili kiendelee kuvutia wanafunzi kutoka nchi za jirani ili kiweze kujiendesha.

Mwisho, ninapongeza sana jitihada zinazofanywa na taasisi zilizoko chini ya Wizara hii kama TANAPA, Ngorongoro, na Idara ya Wanyamapori katika kuhakikisha kuwa, zinachangia Pato la Taifa. Pendekezo langu ni kuwa, bado Shirika la TANAPA linahitaji kujiendeleza, kwa hiyo, badala ya ziada ya mapato ya TANAPA kupelekwa Hazina kama ilivyopendekezwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ni vizuri zikabaki TANAPA kwa maendeleo zaidi. Kwa hiyo, TANAPA wajitahidi kuweka mpango mkakati wa jinsi ya kutumia pesa yoyote ya ziada kwa maendeleo ili kuvutia watalii wengi na kuongeza Pato la Taifa kwa upande mwingine.

**MHE. DAMAS P. NAKEI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Shamsa Mwangunga (Mb), Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa hotuba yake ya bajeti. Naiunga mkono hoja yake hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia utajiri wa nchi yetu tuliojaliwa na Mwenyezi Mungu, siku zote tunalenga Wizara hii yenye dhamana ya maliasili zote za nchi hii. Ni Wizara ambayo ni *custodian* wa mali zetu za asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Waziri kwamba, Wananchi wa Jimbo la Babati Vijijini, wanaopakana na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, kwa muda mrefu sana wameendelea kusumbuliwa na wanyama wakali na waharibifu wa mazao ya mashamba yao.

Wanyama wanaozungumziwa hapa ni Tembo waharibifu. Wanashambulia mahindi, mbaazi na mazao mengineyo. Maeneo yanayoathirika ni pamoja na Minjingu, Sangaiwe, Mamire, Galapo na Qash.

Mwaka 2008, ekari zisizopungua 2447 za mashamba ziliharibiwa sana na tembo. Hii iliwaathiri wananchi 453.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tulishapeleka madai ya fidia au kifuta machozi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Babati kwenye Wizara (Wizara ya Maliasili), kwa barua yenye Kumb. Na. DED/BBT/G.1/VOL.V/105 ya tarehe 26 Septemba, 2008. Vijiji vilivyotajwa kwa fidia hiyo ni Qash, Orng'adida. Kwaraa, Endakiso, Mamire, Mwikantsi na Parokia ya Galapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuomba wakulima hawa walipwe fidia, naomba pamoja na Rombo, Simanjiro na Bunda, serikali ijenge vituo viwili ili kukabiliana na wanyama tembo, wasisababishe uharibifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo hivyo vijengwe katika maeneo ya ukanda unaopakana na Hifadhi ya Tarangire.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna habari ya utafiti juu ya matumizi ya pilipili na tumbaku katika maeneo yenye matatizo sugu ya tembo waharibifu. Tunaambiwa kuna mafanikio. Je, wakulima wamepata ufahamu huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia kitabu cha bajeti ya mwaka huu wa 2009/10 na kile cha mwaka wa fedha wa 2008/09, sikukutana na habari yoyote juu ya Msitu mkubwa wa Nowu. Msitu huu ni maarufu kwa uzuri wake na ukubwa wake; ni hekta 13,000. Msitu huu wa asili unayo *ecosystem* nzuri sana; hivyo unafaa kwa *ecotourism.* Watalii wachache sana wanaopita kufanya *camping,* hupata taarifa ya accessibility kwa maana ya barabara. Hivyo, naomba Barabara ya Err-Merr – Endalaha – Madunga, yenye karibu km 25, iweze kujengwa japo kwa changarawe. Itaboresha huduma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msitu huu huvunwa mbao bila ruksa, wahalifu wameendeleza uvunaji haramu wa mbao kwa muda mrefu na kuonyesha kila dalili ya msitu kuisha kimya kimya. Ulinzi mkali uwekwe kwenye msitu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukru sana kwamba, TANAPA ina uhusiano mzuri na wananchi. Jimbo langu la Babati Vijijini pia limenufaika na miradi ya ujirani mwema. Naomba ushirikiano uliopo uendelee kudumu. Pamoja na shukrani hizo, napenda kuikumbusha serikali kwamba, mgogoro wa TANAPA – Tarangire na wanavijiji vitatu vya Ayamango, Gedamar na Giyedabung, bado haujatatuliwa. Kwa maana hiyo, maombi yetu ya kuhawilisha hekta 8,000 za ardhi ya maeneo ya mgogoro bado yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali tuliyofikia ya *stalemate*, njia pekee yenye busara ni kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kufika pale site na kujionea hali halisi kama ambavyo amefanya sehemu nyingine nchini. Bado Waziri hajafika Babati, pamoja na hali ya wananchi kuteseka. Mimi nauliza Babati kuna nini?

**MHE. LUCAS L. SELELII**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Wizara inalo jukumu la kuendeleza utalii. Ninashauri yafuatayo:-

(a) Iwepo Siku Maalum ya Utalii kama zinavyosherehekewa Siku ya Maji, Siku ya UKIMWI na kadhalika.

(b) Ianzishwe Kaulimbiu Maalum ya kuendeleza Utalii na mimi napendekeza iitwe Utalii kwa Maendeleo ya Nchi.

(c) Utalii wa ndani upewe uzito zaidi hasa kwa kuwapa elimu hiyo watoto kuanzia shule za awali.

(d) Pawekwe mkazo wa kila mkoa kuwa na sehemu walau mbili za utalii.

Maduhuli yanayotozwa katika Msitu wa Serikali wa Sao Hill, yatazamwe upya. Kodi na ada ni nyingi, kiasi cha kufanya bei ya mbao ipande kuliko bei ya mbao za nje. Serikali kwa ujumla wake, ione ni jinsi gani inaimarisha Shirika la Ndege (ATCL) ili liweze kufanya kazi ya kuleta watalii kutoka maeneo ya mbali. Pia ifanye juhudi ya kuuza viwanja vya ndege vya KIA na DIA ili mashirika mengi yaje moja kwa moja *(Direct Flight).*

Mwisho, ninawapongeza mno kwa kazi kubwa mnayofanya. Endeleeni na ninaamini Wizara hii itakuwa kiongozi kwa mapato ya nchi. Hongera sana.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuitumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wote walioshiriki katika maandalizi ya hotuba hii. Ni hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninayo michango yangu ya jumla kama ifuatavyo:-

Mimi binafsi, kwa jinsi nifahamuvyo, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu, watu hawa ni waadilifu sana. Nimekuwa nao katika nyakati mbalimbali. Kwa jinsi nilivyojifunza kwao, nimeshawishika kuamini hivyo. Natambua binadamu ni ulimwengu unaojitegemea.

Tatizo langu ni kuwa kwa muda gani Wizara hii itaendelea kutuhumiwa kwa rushwa, hongo na ubadhirifu? Je, Uongozi wa Wizara hii unajisikiaje unapopata tuhuma hizi? Je, ubovu huu kwa mtazamo wa Wizara ni wa kweli? Naomba Mheshimiwa Waziri, atoe tathmini kwa tuhuma hizi. Uwoga wangu ni kuwa, kama watumishi waadilifu katika Wizara hii, ambao ni wengi, kwa imani yangu watakatishwa tamaa na tuhuma hizi na hatimaye washawishike kudumbukia katika mtego wa kujiunga na kikundi kinachoharibu jina na sifa za Wizara kwa kukosa uzalendo na kujijengea mila na desturi za kuendekeza rushwa kwa nguvu zote.

Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, atoke mbele kwa lengo la kuitetea Wizara na watumishi waadilifu na wazalendo katika Wizara hii. Ninaomba sana. Ni vyema akemee tena kwa vitendo, watumishi wanaoharibu jina na sifa za Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo malalamiko kuwa, waajiriwa wapya wanakaa muda mrefu bila posho za kujikimu na mishahara. Watumishi hawa wanakaa hata kwa kipindi cha miezi 4 -6 bila kuanza kupata mishahara, lakini mojawapo ya kazi wazifanyazo watumishi hawa ni kufuatilia mienendo ya watu wanaotorosha mazao ya misitu. Je, tunawaweka katika nafasi zipi vijana hawa hata kama watawakamata wahalifu hao?

Nionavyo mimi, huu ni utaratibu wa kujenga tabaka la watumishi wala rushwa ndani ya Wizara. Tutaondoaje rushwa ndani ya Wizara hii iwapo tunaanza kuwalea watumishi wapya wa Wizara hii kama watoto wa bata; utaratibu wa nenda upendako utakachopata halali yako na yatakayokupata ni yako?

Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, afuatilie utaratibu wa ajira ya watumishi wapya na urahisi wa kuanza kupata fedha ya kujikimu na mishahara.

Yaliyomo katika hotuba yatekelezwe kwa vitendo

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kushiriki nami kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji, kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii ni taasisi inayoingiza mapato mengi sana katika nchi yetu na Mungu katupenda sana, kwa kutupa vivutio vingi vinavyopendwa na wageni (watalii), kama vile wanyama katika mbuga zetu, Mlima Kilimanjaro, Mapango ya Asili, pamoja na Fukwe nzuri sana Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yote haya lazima tumshukuru Mungu, kwa kuvitunza vivutio hivi kwa kuweka mazingira mazuri sehemu zote zenye vivutio hivi. Ninaiomba serikali, kwa kuwa kuna rasilimali nyingi ambazo hazijafikiwa kama walivyozungumza wachangiaji wengi, kuzifanyia tafiti sehemu hizi ili kupanua maeneo zaidi na baadaye wazitangaze ili kutumia na kuongeza mapato ya nchi na ajira kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukuza utalii, nimefurahi sana kusikia Wizara ina mpango wa kujenga chuo cha utalii ili kuimarisha mafunzo ya hoteli na utalii, kwa lengo la kuongeza wingi na ubora wa watumishi wa huduma hizo. Hali hii ni ya kupongezwa, kwani tutaelimisha ndugu zetu, pamoja na kuwapatia ajira wazalendo wa ndani na kuacha kutegemea wafanyakazi kutoka nje ya nchi yetu. Kutekeleza haya, tutatekeleza pia Ilani ya CCM na Ahadi ya Rais wetu ya kutengeneza ajira milioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu ni njia mojawapo ya uhifadhi wa mazingira. Bila misitu hakuna mazingira hakuna maji. Tanzania ina maeneo mengi sana, ambayo misitu imepotea kwa kukatwa kwa ajili ya mbao na mkaa bila kupanda miti mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile sheria ya kukata miti panda miti iko wapi? Tusiposimamia vizuri katika hili, nchi yetu itageuka jangwa na mambo mengi yataondoka na hiyo asali ambayo sasa imekubali biashara kubwa haitozalishwa. Kwa hiyo, kuna haja sasa suala la kupanda miti liwe la kudumu na liendelezwe na kila mmoja wetu, tukizingatia miti ni mazingira, miti ni maji. Mbegu za miti sasa zisambazwe nchi nzima na mafunzo zaidi yatolewe. Pia hatua kali ichukuliwe kwa wanaochoma misitu na wale wanaokata miti ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii, kwa mategemeo ya kupata Maendeleo zaidi, aliyoyaahidi Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake. Lililobaki apewe fedha aanze kazi aliyotumwa na taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu Waziri, Mheshimiwa Maige, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara. Pongezi zimfikie Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitamke rasmi kuwa, ninaunga mkono hoja, pamoja na kwamba ninahitaji ufafanuzi kwenye maeneo machache yafuatayo na pia maombi yangu yafikiriwe:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Milima iliyoko Kilimanjaro ukianzia Wilaya ya Siha mpaka Wilaya ya Same kupitia Wilaya ya Hai, Moshi Vijijini, Rombo na Mwanga, imekuwa kivutio kikubwa kwa wananchi na wageni wakiwemo watalii. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurusa wa 48 aya ya 77 na 78, imezingumzia mradi wa kupunguza umaskini kupitia utalii, uliotekelezwa huko Pangani. Ni jinsi gani mpango huu utaendelezwa kwenye maeneo mengine ikiwemo Kilimanjaro ambayo watu wake wote wanaishi kwenye miteremko ya milima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 42 aya ya 67 tumeelezwa kuhusu kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa. Katika aya ya pili imefafanuliwa kuhusu MKUKUTA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaomba kunukuu: "Mpango huu unahusisha upandaji miti kwa kutumia wadau wenye vipato mbalimbali, hivyo utafaa kutekelezwa katika dhana ya MKUKUTA. Kwa sasa unatarajiwa kujaribiwa katika nchi za Tanzania, Malawi na Indonesia, kwa ufadhili wa Serikali ya Norway."

Kwa kuwa ukataji miti una *speed* kali kuliko upandaji miti; na kwa kuwa theluji ya Mlima Kilimanjaro inayeyuka kwa kasi kubwa sana; je, serikali iko tayari sasa kuuweka Mkoa wa Kilimanjaro katika list/orodha ya mikoa itakayofadhiliwa katika kuotesha miti? Hapa ninaomba ieleweke wazi kuwa, Wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro, wako tayari na wana nguvu ya kuotesha miti na kuurejesha Mlima Kilimanjaro katika hali nzuri kama ilivyokuwa. Wanachohitaji ni elimu, miche na uwezeshwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wote wa Kilimanjaro, katika michango mbalimbali wamekuwa wakiuliza mgao wa ujirani mwema kutoka Kilimanjaro. Bahati mbaya sana, hakuna hata jedwali moja lililoonesha takwimu za mgao huo wala ulivyoboreshwa. Nitashukuru endapo wakati wa majumuisho, Mheshimiwa Waziri atafafanua. Wanawake wa Kilimanjaro wanaomba kufikiriwa 2009/2010.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri.

Nianze kuchangia hoja hii kwa kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii, kwa kazi kubwa wanayoifanya usiku na mchana, kuhakikisha kuwa Wizara inachangia kwa kiasi kikubwa Pato la Taifa letu. Aidha, Mawaziri hawa wameweza kuondoa kero mbalimbali na za miaka mingi na kusababisha Wizara kuwa karibu na wananchi. Ziara zao za kukutana na wadau mbalimbali mijini na vijijini, ndio chanzo kikuu cha kuleta mahusiano mazuri baina ya Wizara na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zangu, nami nianze kuchangia hoja kwa kuiomba Wizara kuangalia uwezekano wa kutangaza eneo la Delta ya Mto Rufiji kuwa ni eneo la utalii. Hii inatokana hasa na fukwe zake, ambazo ni za mchanga mweupe. Fukwe hizi zipo hasa katika Vijiji vya Pombwe, Jaja, Mbwera Mashariki, Kiasi na Kiombini. Fukwe hizi ni ndefu na zinafaa sana kwa kujenga hoteli kubwa za kisasa na kufanya utalii wa mashua/boti. Ni vizuri sasa serikali kwenda na kuyaona maeneo hayo na hatimaye kuyatangaza kwa wawekezaji ili utalii uweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu uvunaji wa misitu ya asili, ambayo ni pamoja na ile ya mikoko. Kwa zaidi ya miaka mitano sasa, uvunaji wa mikoko umesitishwa kutokana na serikali kuweka utaratibu wa uvunaji endelevu wa miti hii. Nakubaliana na serikali kuhusu utaratibu huu unaofanywa, kwani kwa kiasi kubwa utaweka mahitaji halisi ya miti katika nchi yetu kwa kila mwaka; kwani sensa itafanyika ili kupata takwimu sahihi za mahitaji yetu na miti iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kwa serikali kuharakisha mchakato huu wa sensa ya miti ili wananchi wanaoishi katika misutu hii waweze kunufaika kwa shughuli za kibiashara inayotokana na miti hii. Ni vizuri pia kwa serikali kurahisisha utaratibu wa upatikanaji wa vibali vya kukata miti, pindi serikali itakapokamilisha mchakato huu wa sensa. Vibali vya miti ya mikoko vinapatikana Wizarani tu, kitu ambacho kinawakosesha fedha na haki, wakataji miti wadogo wadogo

wanaozunguka na kulinda miti hiyo. Naishauri serikali (Wizara), iweze kukasimu madaraka yake kwa Mkuu wa Wilaya ili wananchi hao waweze kupata nafuu ya upatikanaji wa vibali vya kukata miti, pindi mchakato huu utakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu doria kwa eneo zima la Delta ili kulinda miti hii ya mikoko. Kwa sasa eneo zima la Delta, ambalo lina urefu wa zaidi ya km 70, lina boti moja tu ya doria, ambayo ipo Nyamisati. Boti hii ina matatizo mengi na hatimaye kushindwa kufanya kazi zilizokusudiwa. Baadhi ya matatizo hayo ni:-

- Ukosefu wa mafuta ya kuendeshea boti hii.

- Nahodha anayeendesha boti hii hajapata ajira (ni kibarua), kwa zaidi ya miaka kumi sasa. Kijana huyu ambaye Mheshimiwa Naibu Waziri anamfahamu; ni vizuri akapatiwa ajira kwani anafanya kazi kubwa na kwa uaminifu mkubwa.

- Boti hii haina uwezo wa kufanya doria kwa eneo zima la Delta, kwani ni eneo kubwa sana.

Ushauri wangu ni kuwa; ni vizuri sasa serikali (Wizara), ikaweka vituo vidogo pamoja na boti za doria katika Vijiji vya Kiasi pamoja na Jaja. Vituo hivi kama vitakubaliwa, vitasaidia sana kulima mikoko yetu na hivyo kuvunwa kwa uangalifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii, kushukuru kwa kupata fursa ya kuchangia hoja hii kwa maandishi. Awali ya yote, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Wasaidizi wake wote, pamoja na Watumishi wote wa Wizara hii na taasisi zote.

Juhudi za Wizara hii za Mpango wa Bajeti wa 2009/10, zimesheheni dhamira njema kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa taifa letu, una vitungo vya rasilimali mbalimbali, hivyo kwa umoja wa rasilimali hizi, zinaimarisha hali ya uchumi wetu wa kuwezesha kujengwa matakwa ya ujamaa na kujitegemea.Umoja endelevu wa rasilimali mfano, kuendelezwa madini, kilimo, ufugaji, utalii, rasilimali misitu na vyote vilivyopo hapa Tanzania, vitatuwezesha kutekelezwa malengo ya taifa kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali ya hifadhi ya maliasili ambayo ipo katika mbuga za kuhifadhi wanyamapori, imekuwa na msukosuko wa kugombana na wakulima na wafugaji.

Chimbuko la misukosuko kati ya wafugaji na wakulima kwa hizi hifadhi ya mbuga za kuvutia utalii, kadiri miaka inavyozaliwa upya, ndivyo migongano nayo inavyozaliwa upya.

Wanyamapori wanazaliana, binadamu wanazaliana na mifugo inazaliana lakini ardhi haizaliani. Kwa kuwa ardhi haizaliani, lakini walengwa wa kutumia ardhi wanazaliana hadi wanazalisha migongano ambayo inatishia amani na inatishia uhai kwa wanyamapori na kwa mifugo ni kugombania maji ya kupatia mifugo; sasa mamlaka ya hifadhi ya mbuga za wanyamapori wanapopanua wigo wa hifadhi na hivyo kumeza maeneo ambayo yalikuwa ni mtandao wa mifugo, mfano, mabwawa ya maji yaliyokuwa ni maeneo ya mifugo kabla ya kupanuliwa eka za hifadhi. Je, Wizara ina mpango gani wa kufidia miundombinu inayomezwa na upanuzi wa hifadhi ili mifugo nayo isiingie katika hifadhi?

Kwa kuwa ardhi haizaliani; je, Wizara ya Maliasili na Utalii ina mpango gani wa kujenga suluhu ya kuondoa migongano ya misukosuko ya wafugaji kunyemelea huduma za maji kwa wafugaji na umwagiliaji wa kutumia maji ya visima virefu ya kusukumwa umbali wa kutosha kufikia vijiji vinavyodai kunyemelea unyevunyevu wa ardhi zilizopo karibu na hifadhi mbalimbali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya serikali ni kujenga uwezo wa maisha bora kwa kila Mtanzania. Sasa Wizara hii ndio mhimili wa rasilimali misitu ambayo huzalisha nyenzo muhimu ya

kufaulisha majenzi ya nyumba bora kwa maisha bora ya Watanzania; je, bei za malighafi za misitu zina uwiano gani kwa kipato cha Mtanzania hivyo amudu kununua mbao za kujenga nyumba bora? Je, azma ya kutafuta uhuru na hivyo rasilimali za Tanzania kuwa kwa maslahi ya Tanzania zinathibitishwa na hatua zipi za kumwezesha Mtanzania wa kipato cha kawaida atumie mavuno ya misitu ya Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ana mpango gani wa kuzipunguzia Halmashauri bei za mavuno ya misitu yetu kwa sababu ambazo serikali haitozi huduma ya mitambo inayoletwa na NGO kusaidia ustawi na maendeleo ya huduma mfano, afya, elimu na umeme?

Baada ya hoja hizi kujibiwa, nami nitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha. Ahsante.

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, sina budi kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri inayoendelea kufanywa na Wizara hiyo. Aidha, ninaipongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri, jinsi ilivyopangiliwa na yenye mwelekeo mzuri wa kukuza uchumi wetu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu kuchangia maeneo machache yafuatayo ambayo nami ninaona ni vyema niyagusie kidogo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna bahati kubwa kwa kuwa na eneo kubwa la pori, ambalo lina wanyama wengi wenye kuvutia na wanaopendwa sana kuonwa na watalii na hata wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba, bado tuna kazi kubwa ya kupambana na maharamia wanaovuruga kwa kuwauwa wanyamapori wetu. Hivi sasa kuna hatari ya upungufu mkubwa wa wanyama aina Tembo, Kifaru, Nyati na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi zetu hivi sasa zinadharaulika; baadhi ya wananchi hivi sasa wanachoma moto ovyo, wengine wanathubutu kulima na hata kukata kuni. Jambo ambalo linajulikana kabisa kwamba ni makosa, lakini bado uasi huo unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kushauri kwamba, elimu kwa wananchi lazima ichukue nafasi yake kwa haraka. Aidha, ninashauri kwamba, askari wa wanyamapori waimarishwe na wapewe nguvu zaidi

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna bahati ya mabaki ya mambo ya kale mengi. Tanzania tuna magofu katika pembe zote kama vile Zanzibar, Mtwara, Tabora, Bagamoyo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna magofu mengi hayana huduma na baadhi yanaporomoka kama yale ya Mtwara, Bagamoyo na baadhi ya sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri mafogu hayo yafanyiwe ukarabati wa kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna eneo kubwa sana la bahari, katika mwambao wake tuna fukwe za bahari nzuri sana. Kutokana na uharibifu wa kufyekwa mikoko, inasababisha fukwe hizo kuharibika na kufuja mandhari nzuri alizotuwekea Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kisiwa chetu kizuri kiitwacho Maziwe, lilikuwa eneo la Pangani. Kisiwa hicho kina historia nzuri, kwa utangazaji wa kasa na ndege wazuri. Kisiwa hicho kimefyekwa pori lake na sasa kimezama na kubaki fungu la mchanga tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iendelee na juhudi zake za udhibiti wa maeneo yetu, ambayo yanachangia vizuri uchumi wa taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya machache hayo, kwa heshima kabisa, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii, kwanza, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa hotuba yao kwa ushirikiano na Watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, Utalii wa Tanzania bado, naiomba serikali izidishe juhudi ya utekelezaji kwa Sekta za Utalii na kutoa elimu kwa wadau ndani ya nchi na nje kwa faida ya taifa ili uchumi wetu uzidi kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia wanyamapori na vitalu vyetu viendelezwe na wanyama kuhifadhiwa na kuvitangaza ili watalii waweze kuja nchini na tupate fedha za kigeni. Misitu inahitaji usimamizi mzuri ili itumike kama inavyohitajika, pamoja na vivutio vyote kwa maslahi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara isimamie vyema utekelezaji wa kazi na utendaji zaidi, kuweka uzalendo na kujali maendeleo ya nchi yetu na maslahi yake kwa miundombinu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, panapo mipango mizuri, hakuna sababu ya kutofanikiwa; sina shaka tukijipanga vizuri tutafika.

Kwa niaba ya Wananchi wa Magogoni, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. JUMA SAID OMAR**: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri, Naibu wake, pamoja na Watendaji, kwa kuwasilisha bajeti yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina wanyamapori wa aina mbalimbali, ambao ni rasilimali kubwa na muhimu sana katika kukuza uchumi na kuchangia Pato la Taifa, lakini asilimia ndogo sana ya mapato yapatikanayo kutokana na wanyamapori. Je, serikali ina mipango gani madhubuti na ya uhakika itakayochangia kikamilifu Pato la Taifa kutokana na rasilimali hii ya wanyamapori?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utalii ni Sekta mojawapo muhimu ya kukuza uchumi na kuleta maendeleo. Kuna vivutio vingi katika maeneo mbalimbali kama vile fukwe nzuri, chemchemi za maji moto, maporomoko ya maji, hifadhi za wanyama mbalimbali na kadhalika. Kwa kuwa Sekta ya Utalii hapa nchini imeathirika kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani; je, serikali imejiandaa vipi ili Sekta ya Utalii iweze kuchangia Pato la Taifa kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko ilivyo hivi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema serikali ikaweka mazingira mazuri na kuhamasisha utalii wa ndani, badala ya kutegemea utalii wa nje zaidi ili uchumi wa nchi uweze kukua na hivyo kuchangia Pato la Taifa na kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, serikali iwawezeshe wawekezaji wazalendo, kujenga hoteli katika maeneo mbalimbali ya vivutio ili manufaa yaweze kupatikana kwa Wananchi wa Tanzania, badala ya kuwanufaisha wageni peke yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi yenye misitu na mapori mengi ya asili, ambayo yakitumiwa vizuri yanaweza kusaidia kuongeza Pato la Taifa. Hivyo ni vyema rasilimali hizi zikatunzwa vizuri ili watu wasijikatie miti ya mbao na wengine kuchoma mkaa, mambo ambayo yanaharibu mazingira na kudhoofisha uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wahamasishwe kuhusu ufugaji wa nyuki, kwani hii ni njia mojawapo itakayowawezesha kupata kipato na kuweza kujikwamua kutokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia kwa wanaouawa na wanyamapori iangaliwe upya, ikiwa ni kama kifuta machozi.

**MHE. DKT. SAMSON F. MPANDA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba nzuri aliyoitoa Mheshimiwa Waziri, pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii, kuna mambo machache ningependa kuyaelezea.

Katika Jimbo la Kilwa Kaskazini, tumebahatika kupata maeneo mengi mazuri ya kitalii, kama yangeendelezwa ipasavyo, yangeongezea uchumi nchi yetu.

Kuna mapango yapatayo 26, ambayo yapo katika Wilaya ya Kilwa, Tarafa ya Kipatimu; ni kivutio kikubwa sana kwa utalii, kwani mapango hayo yana historia ndefu ya kutumiwa katika Vita vya Majimaji (1905 – 1907). Napendekeza mapango hayo yaendelezwe. Mheshimiwa Waziri, kama ungepata nafasi ya kuja kuyaona, ungeona maajabu yaliyopo katika mapango hayo.

Nasikitika sana kuona watu wanasahau walipojikwaa na kukumbuka walipoangukia. Hii ina maana, Vita vya Majimaji vilianzia Kilwa Kipatimu na kusambaa kwingineko. Ajabu ni kwamba, kulikoanzia vita hivyo hakupewi umuhimu, badala yake kipaumbele kinapewa kule kulikoishia vita hivyo.

Ningependa Sheria ya Fidia ya Wadhurikao na Wanyama Wakali, iwape kipaumbele walioumizwa badala ya kuwapa kipaumbele waliokufa. Walioumizwa na wanyama wanapata kifuta jasho kidogo mno. Napendekeza Sheria hii iangaliwe tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wizara kutueleza kuna Chuo cha Utalii kinajengwa kwa kushirikiana na Ufaransa, lakini Chuo kile ni matarajio yangu kitaweza kutoa mpaka shahada na stashada. Kwa ajili ya *training*, kulikuwa na chuo kizuri cha Forodhani, ambacho kimekufa na kugeuzwa Mahakama ya Rufaa. Mpaka Chuo kipya kiwe tayari na hakuna Chuo cha Serikali ambacho huwa ni bei nafuu kuliko vyuo vya watu binafsi; je, serikali haioni haiwatendei haki wanafunzi kwa kukosa Chuo cha Serikali mpaka hicho kipya kijengwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa makampuni ya watu binafsi yanapokwenda kuhuduria Maonesho ya Utalii huwa yanakuwa na bei sana. Inabidi kununua tiketi, malazi, chakula na kulipia banda siyo chini ya $ 5000; ni fedha nyingi. Kwa kuwa huwa tunakwenda kuitangaza nchi, basi serikali itoe *subsidy* kutusaidia ku-*attend* maonesho hayo.

**MHE. STEPHEN M. WASIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Vijiji vya Bukore, Nyamatoke, Mchere, Hunyari, Kihumbu, Mariwanda, Mugeta na Kyandege, vilivyoko kandokando ya Hifadhi ya Grumeti, wamekuwa wanaathirika sana kutokana na yafuatayo:-

1. Uhusiano mbaya katika Para-military inayomilikiwa na VIP kwa kuwakamata wananchi wanaokwenda kunywesha mifugo yao Mto Rubana ili hali wakijua hakuna sehemu yoyote ya kupata maji.

2. Kutozwa faini zisizo halali kufungwa kwa kesi bila sababu za msingi, vifungo hivyo vikihusisha watoto wa shule mmoja akiwa gerezani katika umri wa miaka 13.

3. Uharibifu mkubwa wa mazao unaofanywa na tembo, ambao umesababisha kukosekana kwa usalama wa chakula. Nimewasilisha orodha ya familia 500 zilizoadhirika kwa kukosa chakula kutokana na uharibifu wa mashamba yao. Naiomba Wizara itoe kauli ni lini wananchi hao watalipwa angalau kifuta machozi kutokana na uharibifu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kazi nzuri. Nampongeza pia Waziri, kwa ushindi kwenye Maonesho ya Sabasaba.

Naanza kwa kuchangia upande wa Mapango ya Amboni Mkoani Tanga. Je ni lini mapango hayo yatafufuliwa kwani yamesahaulika kabisa? Mapango hayo ni kivutio kikubwa kwa watalii.

Pili, nitazungumzia hoteli za kitalii, upande wa wafanyakazi. Wafanyakazi wanatakiwa wapatiwe mafunzo ya hali ya juu kwenye upande wa *language* na *customer care*, ili ajira hizi zisichukuliwe na wageni, ziwe za Watanzania wenyewe. Vile vile Vyuo vya Utalii viboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni hayo wawili tu, namalizia kwa kusema, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Kwa muda mrefu sana, nchi yetu imekuwa na misitu na mbuga za wanyama ambazo zinapendeza. Pia napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kutilia mkazo sasa na uhamasishaji wa utalii wa ndani, hii ni faraja sana na ni vizuri kwa utalii. Hivyo basi, naiomba Wizara hii isiwe nguvu ya soda, iwe mpango endelevu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna maliasili nyingi ambazo hutoka ndani ya nchi na kwenda nje ya nchi, hivi mpaka sasa watu hawa ni hatua gani huchukuliwa kwani husikia tu magogo mengi ya Tanzania huenda kwa wingi nchini China na mengine kupita njia za panya. Je, Wizara imefikia hatua gani katika suala hili? Ushauri wangu ni udhibiti mkali uongezeke na adhabu ziongezwe na ziwe wazi.

Mheshimiwa Spika, juzi wakati watu wanapanda Mlima Kilimanjaro, nilipata kumuona kijana mdogo mwenye umri upatao miaka 14 na ni mtoto yatima toka Wilayani Sengerema, inasemekana watu wazima walishindwa kupanda na waliishia njiani, lakini upandaji wa mtoto huyu ni changamoto kwa vijana walio wengi na amewatia hamu watoto wengine. Napenda kushauri kuwa, kwa kuwa mtoto huyo umri wake ni mdogo na ameonyesha maajabu na kuwatia hamasa kubwa vijana wengine. Pia kijana huyo ni mtoto yatima, Mheshimiwa Waziri huoni ni vema kijana huyo Wizara yako ikaweza kumzawadia kwa kumuhudumia gharama zake za masomo, tokea hapo alipo mpaka elimu ya juu ili kuzidi kuwahamasisha zaidi vijana na watoto kama yeye? Mheshimiwa Waziri nakuomba ushughulikie suala hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kusema, naomba basi mboreshe zaidi kisiwa cha Saanane pale mjini Mwanza na muweze kushirikiana na Wizara ya Elimu ili wanafunzi waweze kujifunza na kutembelea kisiwa hicho, kwani kwa wanafunzi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Wilaya jirani, kwani gharama itakuwa ndogo zaidi na vijana wetu watapata kuona wanyama wetu na tayari watakuwa wameanza kufanya utalii wa ndani. Hapo zamani kingali bado ni kisiwa cha kupendeza wanafunzi tulienda huko na hata nyakati za sikukuu watu wengi walitumia nafasi hiyo kutembelea kisiwa hicho. Nawaomba mkiboreshe zaidi, kwani huo ndio mwanzo wa utalii.

Mheshimiwa Spika, pia naomba mboreshe na mkitangaze zaidi kituo cha Bujora ili watu wengi waweze kukitembelea. Hongereni kwa kukuza utalii wa ndani, ahsante.

**MHE. SIGFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Spika, nawapa pongezi kwa kazi nzuri wanazofanya Mheshimiwa Waziri, Naibu na watendaji wote lakini hasa ile ya wanyama pori chini ya Mheshimiwa Tarimo, maana Wizara hii imejaa changamoto nyingi lakini mnazimudu.

Mheshimiwa Spika, mimi tatizo langu ni dogo sana ingawa ni kero kubwa sana kwa Maafisa Wanyamapori wetu kule Rungwa, hawana usafiri yaani hata pikipiki hakuna. Wanakwenda kwa miguu au baiskeli kwenye doria kule Narung'ombe, Nambiranje, Mandawa maeneo ambayo yapo karibu na *Selous Game Reserve*. Wote mnajua kuwa kule hakuna kitoweo,

je, tuna uhakika gani kama hakuna wahalifu wanaoingia maporini na kuwadhuru wanyama? Chonde chonde tunaomba angalau pikipiki ingawa tunachoomba ni gari, ahsante.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni pongezi kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara. Tanzania ni tajiri sana katika eneo hili kuliko nchi nyingine yoyote duniani. Hivyo pamoja na kazi nzuri iliyofanywa, changamoto ni kwamba je, tumekwishafanya yote tuliyotakiwa kufanya? Bila shaka hapana! Kwa uwezo wa rasilimali ulioko katika Wizara kuanzia Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu naamini kabisa wanaweza kutekeleza majukumu kwa ufanisi zaidi na Mungu awatie nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbuga, WMA, jambo hili nimelileta Wizarani kupitia Naibu Waziri, Mheshimiwa Maige lakini sijaona juhudi yoyote wala mrejesho wowote.

Nilipotembelea sabasaba Namtumbo na Tunduru wanafaidi kwa nini iwe ngumu na kimya kwa Mbinga? Ipo *Game Reserve* ya Liparamba lakini pia Litumba Ndyosi. Ninaomba hatua za haraka zifanyike lakini pia nipate majibu ya maandishi *'let us serve the people'*

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kale**,** Mbinga pia inayo maeneo mengi sana ya namna hii. Naomba mtusaidie namna ya kuendeleza. Wapo wazee wa kuonyesha kwa mfano pale Litembo, jiwe la Mbuji, pango kubwa la Lilangongondo.

Mheshimiwa Spika, *cultural tourism,* wakati wa masika Mbinga majembe yanashushwa toka darini na ngoma zinapandishwa na wakati wa kiangazi ni kinyume chake. Naomba msaada wenu, mwezi August ngoma zinaanza, nitafurahi kuwapata *TBC* twende tukachukue picha na kufanya *'documentation'.* Ni kitu cha kipekee na kinachafurahisha wananchi wakifurahi baada ya mavuno *'this is very unique'.*

Mheshimiwa Spika, uendelezaji utalii Bonde la Nyasa. Upande wa Malawi, ufukwe wa Ziwa Nyasa umeendelezwa sana, upande wetu bado kabisa. Naiomba Wizara itusaidie hata kwa upande wa mkakati na uhamasishaji.

Mheshimiwa Spika, nawatakia mafanikio katika mwaka wa 2009/2010. Naunga mkono hoja na ahsante sana.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa idara zote zilizo chini ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utali, ni Wizara ambayo ina majukumu mengi sana ambapo ni changamoto ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina matatizo makubwa yanayowapata, hasa kwenye sekta ya wanyamapori, misitu na kwenye hifadhi zetu, hasa wanavyopambana na wahalifu wakubwa wanaorudisha nyuma maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa misitu, kuna haja ya kuongeza doria na watumishi kwenye misitu yetu. Wapo watumishi wasio waaminifu kwenye idara hii, kuna malalamiko hasa kwenye ugawaji wa maeneo ya uvunaji wa mbao. Naomba uifanyie kazi kubwa Idara ya Misitu, pia kuna uonevu mkubwa wakati wa ukaguzi kwenye maeneo ya misitu.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Wanyamapori, lipo tatizo hasa kwenye maeneo ya uwindaji. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, tazama sana eneo hilo linalalamikiwa sambamba na mambo ya vitalu.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la kutokuwa na uwiano katika suala la ugawaji. Kwa kuwa utaratibu mpya unaandaliwa, ni vizuri mkajipange ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima. Lipo tatizo la uwajibikaji wa watumishi, ni vizuri wote wakafanya kazi kama timu moja, kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kwa Askari walio katika *Game Reserve* ya Wamimbiki kwa upande wa Jimbo la Chalinze, kuna nguvu za uonevu zinatumika sana dhidi ya wananchi. Mfano yupo mwananchi alikamatwa badala ya kushtakiwa kwenye Mahakama za Wilaya Bagamoyo, alipelekwa Morogoro na alikosa msaada wa kindugu hata kupata dhamana kwa sababu Mahakama ya Morogoro ilitaka wadhamini wawe wanaofahamika na wawe wakazi wa Morogoro je, hiyo ni haki kwa kuwanyanyasa wananchi?

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la mipaka kwenye hifadhi zetu, naomba sana mmalize migogoro yote kwenye hifadhi zetu ikiwamo ya mbuga ya Saadani. Tukiwa na uhusiano mzuri na wananchi, tutakuwa tukipata ulinzi shirikishi yaani wananchi na tusipokaa nao vizuri wanaweza kuwa chanzo cha kushirikiana na wahalifu kwenye hifadhi zetu. Malizeni kuweka alama za mipaka na pale ambapo ushiriki wetu unahitajika, kwa kumaliza tatizo kama la Saadani, naomba nishirikishwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho Wizara kupitia idara zake zione sasa kuwapa motisha, kama nyumba, malipo ya ziada, *(overtime)* za mwezi, maisha magumu, watumishi wa idara hizi wapo katika hali mbaya sana. Tuwatunze ili watutunzie maliasili zetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, natoa pongezi zangu kwa Waziri na watendaji wake, kwa hotuba yake nzuri iliyosomwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imechangia kiasi kikubwa kiliingizia pato kubwa la Taifa letu hivyo natoa pongezi katika hilo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndio yenye dhamana na sekta ya utalii, lakini jambo ambalo huwa najiuliza, mbona utalii unatangazwa sana Mikoa ya Kaskazini? Napenda kusema kwamba katika Mkoa wa Mbeya kuna vivutio vingi ambavyo kama vitaimarishwa na kusimamiwa vinaweza kuwavutia watalii wengi na kuliingizia Taifai pato kubwa.

Naomba nivitaje vichache navyo ni Bonde la Ihefu, Mlima Rungwe, Maporomoko ya Kaporogwe yaliyoko Wilayani Rungwe, ambayo yana maajabu yametengenezwa na Mungu, Daraja la Mungu kwenye Mto Kiwira na Milima ya Livingstone, Wilaya ya Rungwe.

Mheshimwa Spika, haya ni maeneo machache lakini yapo maeneo mengine ambayo wakitumwa wataalam wanaweza wakaona, naamini watavipata hatimaye watalii wataongezeka endapo vitatangazwa kisha kuliongezea Taifa letu pato.

Mheshimiwa Spika, huu ndio ushauri wangu, naunga mkono hoja, nawasilisha.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, napongeza hotuba nzuri na kazi nzuri inayoendelea katika Wizara hii. Hata hivyo nitachangia katika maeneo mawili:-

Mheshimiwa Spika, *Ruaha National Park,* hifadhi hii ndiyo kubwa kuliko zote nchini lakini inasikitisha kwamba haitambuliki kama Hifadhi za Kaskazini na haipewi umuhimu unaostahili. Miaka nenda, miaka rudi, jitihada na rasilimali zote huelekezwa *'Northern Tourist Circuit'*, kasoro hii ilibainika na Wizara iliandaa *'Southern Tourist Circuit'* (ninayo nakala yake) lakini kwa kiwango kikubwa, mpango huo umebaki katika makaratasi licha ya Mkoa wa Iringa kuamua kukuza utalii. Kwa kasi hii, itachukua karne nzima kukua.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika Wizara ichukue hatua mahsusi kukuza utalii Mkoani Iringa nje na ndani. Pia naomba Waziri kufika Mkoani atembelee vivutio mbalimbali na kushauriana na uongozi.

Mheshimiwa Spika, *climate change,* taarifa za kitaalamu duniani zinabashiri maafa makubwa katika miongo miwili/mitatu ijayo ambayo ni ukame/mafuriko, ukosefu wa chakula na

jamii kama matokeo ya *"human activity".* Idadi ya watu inaongezeka kwa kasi ingawa ardhi na mahitaji yao yako pale pale kama siyo zaidi. Nchi nyingine hudhibiti uzazi kwa kuweka ukomo wa watoto. Hili siyo tatizo la Wizara moja lakini lazima tuanzie mahali fulani ili kuhakikisha kwamba kuna uwiano unaostahili ili kuepusha matokeo hayo. Je, Wizara inaliangaliaje jambo hili?

Mheshimiwa Spika, *Carbon Trading,* sina hakika na suala hili lakini kumejitokeza habari kwamba mbali ya upandaji miti wa kawaida, kuna mpango wa kuwalipa watu watakaopanda miti itakayopunguza uwepo wa hewa chafu. Sina hakika ni mpango wa shirika au chombo gani. Je, Wizara inahusika na mpango huu? Kama ndiyo, inawezekana kupata uelewa zaidi na jinsi ya kushiriki?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Hifadhi ya Ngorongoro isichukuliwe kiasisa, Taifa litapoteza maeneo ya kihistoria na utalii, wanyamapori lazima walindwe kuleta uwiano wao na mazingira asili.

**MHE. DR. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia uhai na kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge lako hili, nawashukuru sana wanawake wa Chama cha Mapinduzi, Jumuiya ya UWT, Mkoa wa Morogoro, kwa kuniamini na nikawepo hapa, nawashukuru.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati, kwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii, hasa kwa upande au sekta ya utalii, imechangia pato kubwa la nchi yetu. Jambo ninaloliomba kwa Wizara hii ni kuzidi kutangaza utalii hasa utalii unaobainika katika Mikoa mingi ya Tanzania. Utalii mkubwa kwa sasa unatangazwa/unaendelea katika Mikoa ya Kaskazini na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia, Mkoa wangu wa Morogoro, wao utalii wa kutangazwa, sio Hifadhi ya Mikumi yaani wanyama tu, hata huko Wilayani kuna vivutio vya utalii vya kutangazwa kama maporomoko au mito mingi, mabonde misitu, mawe mazuri, wanyama na mambo mengine kama milima ya Uluguru.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni Mkoa wa Ruvuma, una utalii wa kutosha na vivutio vya kila aina. Kwa mfano, historia ya Vita vya Majimaji, Hifadhi ya *Selous*, misitu na mabonde. Pia Mkoa wa Pwani na Kagera una vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Spika, jambo ninaloomba, Wizara wawatume wafanyakazi wa Wizara Mikoani ili wapate vivutio vya utalii vya kutosha. Au Wizara wafanye mikakati ya kupata vivutio kutoka Mikoani ili vitangazwe na kuvutia watalii. Watalii wakiongezeka ni neema kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapa, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wakuu wote wa Idara za Wizara hii, kwa kazi nzuri na hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata ufafanuzi na kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, uvunaji wa Mitiki shamba la Lunguza – Muheza. Mvunaji mkuu *CELMAC,* amechukua muda mrefu kuvuna licha ya kulipa fedha za ununuzi mapema mwaka

2007/2008. Halmashauri ya Wilaya ya Muheza bado haijapata malipo halali au ushuru stahili kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, wala asilimia 5% ya thamani ya mauzo kutoka kwa mnunuzi *CELMAC*. Napenda kuishauri Wizara ya Maliasili na Utalii, kuisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kupata malipo hayo na kubainisha ni kwa nini yamecheleweshwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, uvunaji unaendelea kwa kasi na kugusa maeneo ya mito inayotegemewa sana kutoa maji (Mto Ziggi) kwa Wilaya ya Muheza na Jiji la Tanga. Nashauri upandaji wa miti mipya uende kwa kasi na kutokata miti kando kando ya mito inayopita ndani ya msitu wa Lunguza. Upeo wa Uvunaji. Nashauri uwepo mpango wa uvunaji kwa awamu ili kuepuka uharibifu wa mazingira kwa kuacha wazi maeneo makubwa karibu na maeneo ya hifadhi za msitu wa Amani.

Mheshimiwa Spika, shukrani kwa vijiji vinavyozunguka msitu wa Lunguza kupewa vibali vya uvunaji. Pamoja na shukrani hizo, naomba Wizara isaidie vijiji hivyo katika ujenzi wa madarasa na zahanati unaoendelea katika vijiji vya Kisiwani, Mashewa, Kwemdimu, Bombani Kimbo Kiwanda. Hii ni kuonyesha dhana ya shukrani kwao kwa ulinzi wa msitu wa Lunguza.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sheria ya Utalii ya mwaka 2008. Maboresho yaliopo ndani ya Sheria ya Utalii ya mwaka 2008, yanalenga kuboresha mapato kwa kuwa nafahamu kwamba Kanuni muhimu zimeandaliwa na sera imeanza kutumika. Nashauri maandalizi ya elimu kwa umma na wawekezaji wa ndani katika sekta ya utalii hasa hoteli za kitalii, nyumba za wageni, watoa huduma za usafiri, wapandaji wa milima na wahudumu wengine, wazielewe vizuri kanuni hizo na viwango muhimu vya madaraja vinavyokusudia kuiweka sekta ya utalii Tanzania katika mfumo wa viwango vya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha kuitangaza Tanzania kiutalii nje ya nchi. Tunaipongeza Wizara kwa jitihada iliyokwishafanya kuongeza kasi ya kuitangaza Tanzania katika sekta ya utalii nje ya nchi. Tuendelee kuongeza nguvu katika Bara la Asia (India, China, Japan, Malaysia) na pia Canada na Brazil.

Mheshimiwa Spika, teknolojia ya kuimarisha barabara ndani ya Mbuga za wanyama. Utalii unakuwa na thamani kwa kumwezesha mtalii kuona yale anayotarajia kuyaona katika safari yake ndani ya mbuga za wanyama. Kwa hali hiyo, kuwepo kwa barabara nzuri kuwezesha magari kupita wakati wote ni muhimu sana. Ipo teknolojia rahisi ya utengenezaji wa barabara inapokaribia kiwango cha lami. *TANAPA* wamewahi kuonyeshwa utengenezaji huo wa barabara na wawakilishi wa kampuni kutoka Marekani. Iwapo utekelezaji wa majaribio unaridhisha, ni vema Wizara ya Maliasili na Utalii, ikaunga mkono mfumo huo wa kuimarisha barabara ndani ya mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri ya maandalizi ya bajeti ya Wizara hii katika mwaka wa fedha 2009/2010 na ninaiunga mkono hoja ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mbunge yeyote ameruhusiwa kuzungumzia jambo lolote ambalo liko nje ya Jimbo lake ili mradi ni la manufaa kwa jamii hiyo na Taifa kwa jumla, naomba nichangie machache kuhusiana na Wizara hii muhimu katika uchumi wetu na mchango wangu utajikita zaidi kwenye suala la kero za wanaushirika wa uvuvi na wafuga nyuki katika pori la Akiba la Ugalla kwa mujibu wa maelezo yao na ushahidi wa nakala ya barua Kumb.Na.GD/UGR/TB/D/14/7/Vol.IV/.30 ya tarehe 11/07/2008 ambayo ilihusu ada mpya ya kuingia kwenye pori la Akiba la Ugalla na kusambazwa kwa wenyeviti wa ushirika nitakazozitaja hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, kwa muda wa karibuni, nilitembelea Wilaya ya Sikonge na kwa bahati nzuri, nilikutana na wadau wanaojihusisha na suala la uvuvi kwenye pori la Ugalla ambao walinielezea masikitiko yao ya jinsi wanavyonyanyaswa na Askari wa pori hilo pamoja na kuwa na vibali vya uvuvi kwenye pori hilo. Moja ya nyanyaso, ni kwa Askari hao

kuwapandikiza makosa ambayo mengine hata kwenye mikataba yao hayajaainishwa. Kwa mfano, mtu au mvuvu haruhusiwi kuvua nyakati za usiku jambo ambalo si kweli na kama akionekana anafanya hivyo japo kwa kutumia ndoana huchukuliwa na kuwekwa rumande kwa muda usiojulikana na Askari aliyemkamata huwa hapiti tena Mahakamani kutoa ushahidi wake hadi pale Hakimu anapoamua kumwachia mtuhumiwa kwa kushindwa kupata ushahidi.

Mheshimiwa Spika, wavuvi hao wamekuwa wakipata hasara sana hasa kipindi kile anapokuwa amewekwa rumande ambapo nyavu zake huibiwa na baya zaidi huwekwa rumande bila kosa na hivyo anapoachiwa huru humlazimu kuanza upya kuhangaikia nyavu nyingine na mara nyingine huamua kuachana na uvuvi huo na kuwa jangiri wa ama kukata miti kwa ajili ya mbao au kufanya jambo lingine la kihalifu. Kwa kuwa kuna kero nyingi sana ambazo wanaushirika hao wangependa wazielekeze kwa upande wa Serikali, ninamshauri Mheshimiwa Waziri atembelee Pori la Akiba la Ugalla ili akazungumze na wanaushirika hao.

Mheshimiwa Spika, moja ya kero ambayo hata mimi imenigusa ni ile ya kupandishwa kwa ada za kuingilia kwenye Pori la Akiba hasa ada zinazotozwa magari ambazo zimepanda kutoka kati ya asilimia 100 hadi takribani 5,000 kwa magari yaliyosajiliwa nchini.

Mheshimiwa Spika, suala hili limeleta malalamiko mengi sana kwa wadau wa pori la akiba la Ugalla kwa vile kanuni au taratibu za utozaji ada zilizowekwa kwa mujibu wa Gazeti la Serikali Na.196 toleo la tarehe 14/09/2007, hazikuzingatia kipato wanachopata wadau kutokana na maliasili inayopatikana katika pori hilo.

Mheshimiwa Spika, ninatambua sana Serikali ilikuwa na nia njema tu kwa kuwapa fursa wananchi wake kuzitumia rasilimali zinazopatikana kwenye eneo la pori la Ugalla kwa manufaa yao kwa maana ya kujiajiri na manufaa ya Serikali kwa maana ya kupata mapato. Hata hivyo, kupanda kwa ada ya kuingiza magari porini humo kutoka Tshs.10,000/= hadi 500,000/= (laki tano) kwa siku, kwa magari yaliyosajiliwa nchini, haiwasaidii wadau walengwa bali inawavunja moyo na badala yake wengi wameacha kazi ya uvuvi na kuanza mambo ya ujangiri ukiwemo wa kukata miti kwa ajili ya mbao kitu ambacho Serikali haipati mapato yake na pia hayo haikuyalenga kwa wadau wake.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kupitishwa kanuni hizo za ada mbalimbali, gari lililipiwa Tshs.10,000/= kwa siku na uzito haukuzingatiwa. Naishauri Serikali ada iliyowekwa sasa ipunguzwe na kuwa Tshs.100,000/= kwa gari lenye uzito mkubwa. Hali hii itawafanya wavuvi wengi kurudi kwenye kazi yao ya uvuvi na hivyo kupunguza makali ya maisha. Aidha, namwomba Mheshimiwa Waziri aingilie kati kuhusiana na ada hizo ili wadau wawe na nia njema kwa Serikali yetu katika pori hilo la Akiba la Ugalla.

Mheshimiwa Spika, wadau wakubwa wa uvuvi na ufugaji nyuki katika pori hilo la Akiba la Ugalla ni hawa wafuatao, Ushirika wa Wavuvi Sikonge (SIFCO), Ushirika wa Wavuvi Twikwilagi (USSOKE), Ushirika wa wafuga Nyuki (*TBCS*), Chama cha Ushirika wa Wafuga Nyuki (Mahubha – Nsabho – Kangeme) na Ushirika wa Wavuvi Tabora – Mjini.

Mheshimiwa Spika, endapo Mheshimiwa Waziri atahitaji kivuli cha barua niliyoitaja hapo juu nitampatia, aidha kwa kifupi jedwali lifuatalo ambalo pia linahitaji masahihisho hasa mafungu ya uzito wa magari, linaonyesha ada ya viingilio vya magari kwa siku (24 hrs) kwenye Pori la Akiba la Ugalla.

**UZITO ADA YA GARI KWA SIKU**

| **TANI** | **Gari lenye usajili wa nchini (TShs.)** | **Gari lenye usajili wa nje (US$)** |
|---|---|---|
| 0 – 2 | 20,000/= | 50 |
| 2 – 3 | 50,000/= | 150 |
| 3 – 7 | 100,000/= | 300 |

| | | |
|---|---|---|
| 7 - 10 | 500,000/= | 500 |

Mheshimiwa Spika, Serikali izingatie pia gari linaloingia kwenye Pori la Akiba, litozwe ada kwa pesa za kigeni endapo mwenye kulitumia gari hilo si raia wa Tanzania vinginevyo ada inayotozwa kwa kuzingatia usajili wa gari tu, wageni wengi hutumia magari yaliyosajili nchini kwa nia ya kupunguza gharama.

Mheshimiwa Spika, endapo wadau hao hawatasikilizwa kilio chao, kauli mbiu ya Wizara ya tudumishe matumizi ya maliasili zetu kwa faida ya kizazi chetu na vijavyo, haitakuwa na maana.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa Wanyamapori, Misitu, Utalii na mambo ya kale. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri ambazo mmeanza na kuendelea kuzifanya kupunguza matatizo mengi ambayo yamekuwa yanaikabili Wizara hii. Ongezeni juhudi na msisikilize kelele za watu na wanasiasa, nyie fanyeni kazi zinazoendana na sheria za idara zenu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna upungufu mkubwa sana wa wafanyakazi kwenye idara zote hasa wanyamapori na misitu. Ni jukumu lenu kuhakikisha upungufu huo unaondolewa haraka iwezekanavyo kwani wanyamapori na misitu yetu inamalizwa na majangili hali ambayo mtakuja kulaumiwa sana sana na kizazi kijacho. Sasa hivi wawindaji wa kitalii wametaifisha mapori yetu, wameyafanya kama mali yao, wanawinda wanavyotaka na akiwinda mnyama mdogo akikutana na mnyama mkubwa zaidi anabadilisha kwa kutuma nyara hizo kwa kuwinda yule mkubwa zaidi. Haya yapo kwa sababu hatuna Askari wa kutosha na wenye moyo wa kulinda mapori haya.

Mheshimiwa Spika, hata upande wa misitu, kuna uhaba wa Maafisa Misitu unafanya mapori yetu kwisha kutokana na kukata ovyo misitu.

Pia utaratibu wa kuigawa Wizara hii kati ya Makao Makuu ya Wizara na Halmashauri za Wilaya, yanasaidia sana kutokomeza maliasili zetu kwani kwenye Halmashauri za Wilaya wafanyakazi ni wachache zaidi na Wakurugenzi wengi hawatilii maana maliasili kwa sababu haziingizi kipato cha kutosha kwenye maeneo yao. Bado naomba Wizara hii toka madaraka Mikoani iwe chini ya Wizara. Watumishi wa Wizara hii wanaofanya kazi maporini, wana upungufu mkubwa sana wa vitendea kazi, mavazi, silaha, risasi, magari, uhaba huu Serikali haioni kwamba unawakatisha tamaa ya kufanya kazi na wale wenye kupenda kupokea rushwa wanafanya hivyo na kuruhusu wawindaji haramu au wakata mbao waingie na kuhujumu maliasili zetu?

Mheshimiwa Spika, umefika wakati sasa wa kuomba Idara ya Wanyamapori na Idara ya Misitu ziwe *Agency*, uwezo wa kujiendesha ni mkubwa sana na zikiwa chini ya Bodi mahiri, zitachangia vizuri zaidi pato la Taifa na wao wenyewe kufanya kazi nzuri. Tumekuwa tunaomba kila mwaka mapori ya Akiba *(Game Reserves)* zianzishe mamlaka ili zijiendeshe kama vile Ngorongoro inavyoendeshwa.

Mheshimiwa Spika, Ngorongoro likiwa eneo la saba la maajabu ya dunia, hali siyo nzuri kabisa kwani heshima na umaarufu wa Ngorongoro unashuka kwa kasi ya kutisha mpaka *UNESCO* imependekeza eneo hili lishushwe hadhi, ni aibu kubwa sana kwa nchi. Nakuomba sana, waondoeni wakulima wote na wafugaji wanaokaa na kuendesha shughuli zao kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, hata *TANAPA* sasa hivi hali si shwari, majungu, ukabila uonezi na kadhalika yanatawala. Msukumo ulikuwepo huko nyuma wa kusimamia na kuzilinda hifadhi zetu lakini sasa haupo. Ajira zinatolewa kwa upendeleo hata vyeo pia. Namwomba Mheshimiwa Waziri akae na wataalamu wake, wajipange upya. Hata upande wa Idara ya wanyamapori na misitu, viongozi wasikae ofisini na kufanya kazi kwa kompyuta, watoke waende kwenye maeneo waliko wanyamapori na misitu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuandika kwamba kitu kikubwa kinachorudisha maendeleo ya wanyamapori Ngorongoro na *TANAPA,* ni bodi za kisiasa wanazounda kwa mfano

Ngorongoro Bwananyama mmoja tu. *TANAPA* hakuna Bwananyama hata mmoja, nakushauri angalia sana suala hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini ahadi ya Serikali ya kutoa kifuta machozi kwa walioathirika kutokana na mashambulizi ya mamba, itatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, mamba kwenye Ziwe Rukwa bado wanaendelea kuleta madhara kwa binadamu wanaotumia ziwa hilo na wanaendelea kuzaliana kwa kiwango kikubwa sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaletea amani wananchi wanaoishi kando kando mwa ziwa hilo hasa upande wake wa Wilaya ya Chunya – Jimboni Songwe?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani au mikakati ipi kuanzisha na kuendeleza shughuli za kitalii kwenye Wilaya ya Chunya ambako kuna vivutio vingi vya asili?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba na bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu uko katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa bwawa la Nsango. Naipongeza Serikali kukubali kuchimba bwawa katika eneo hili. Hali hii itajenga uhusiano mzuri kati ya wananchi, wafugaji na wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, mapato ya 25% kwenye Halmashauri. Katika Wilaya ya Bukombe, hatujapata mapato haya. Je, inamaanisha wawindaji hawaji tena kwenye hifadhi ya Kigosi/Myowosi ?

Mheshimiwa Spika, wafugaji wa nyuki, naomba Serikali iendelee kutoa ushirikiano mzuri na wafugaji wa nyuki. Zaidi ya 20% ya wananchi wa Bukombe, wanajihusisha na ufugaji wa nyuki. Elimu itolewe kwa wafugaji mara kwa mara ili kuondoa tofauti, lakini pia kuwawezesha wafugaji kujua shughuli zingine za uhifadhi zinazofanywa.

Mheshimiwa Spika, kutenga angalau 15km za malisho. Nashauri Serikali itenge kilomita 15 toka mpaka wa hifadhi kuingia ndani kwa ajili ya wafugaji. Bukombe imezungukwa na hifadhi ya Kigosi/Myowosi ambapo 60% ni msitu, 40% ni eneo la wafugaji, wakulima, wachimbaji wadogo wadogo na makazi. Kwa hali hiyo, ni vizuri tutenge kilomita tajwa kuzunguka msitu ili wafugaji wanufaike na wote uliopo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali kupitia Idara ya Wanyamapori kwa maendeleo wanayochangia Bukombe. Mfano, Idara imechangia madawati katika sekondari ya Iponya, wamechangia TShs.8,000,000/= (milioni nane tu) kwa ajili ya ujenzi wa shule ya msingi Kashozi. Watumishi wa Idara hii wanawapiga sana wananchi wanapoonekana maeneo hayo. Lakini wanatozwa hela nyingi sana hasa wafugaji wanapokutwa na mifugo yao. Kwa nini wasiwapeleke Mahakamani badala ya kuwapiga na kuwachukulia hela nyingi sana kama wanavyofanya?

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri anahitimisha naomba utoe ufafanuzi wa maeneo yafuatayo:-

(a) Uchimbaji wa bwawa la Nsango utaanza mwaka huu wa bajeti?

(b) Serikali inakubali kutenga kilomita 15 kuingia ndani ya hifadhi kwa ajili ya wafugaji?

(c) Serikali inasema nini juu ya watumishi wa Idara (Askari) Wanyamapori wanakula/chukua fedha kwa wafugaji, wamewafanya wafugaji kama shamba lao? Kwa nini wasipelekwe Mahakamani?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na timu yake kwa kuandaa hotuba hii ya bajeti. Sambamba na hotubu hii, naomba tu kupewa maelezo na ufafanuzi wa yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwa namna gani Serikali inaweka mpango mkakati wa kuoanisha utalii asilia na utalii wa kigeni na hasa kwa maeneo ya ukanda wa Mikoa ya Ziwa ikiwemo Mwanza, Mara, Kagera, Shinyanga na Kigoma?

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya vivutio vingi vilivyopo Mwanza vikiwemo, Ziwa Victoria, Makumbusho ya Bujora yanayohusu Wasukuma, Saanane Island, Rubando Island, Mawe yanayocheza Ukerewe na kadhalika. Vivutio hivi havijapewa makazo na Serikali, licha ya kuwa vinaweza kuchochea utalii na kuliingizia pato kubwa Taifa. Je, Wizara hii imepanga yapi kwa mwaka huu wa fedha?

Mheshimiwa Spika, suala la magari ya akiba na jamii inayozunguka mapori haya. Kwani kuna wakati na hii inatokea mara kwa mara wafugaji kutozwa faini kubwa wakati mfugo inapoingia kwenye hifadhi na hasa wakati wa uhaba wa malisho. Je, Wizara haioni ipo haja ya kuwalinda wanajamii badala ya kuwalinda zaidi wanyama licha ya kuwa wanyama huvamia mashamba na makazi ya watu na kuleta uharibifu mkubwa ikiwemo upotevu wa maisha.

Mheshimiwa Spika, nini mkakati wa Wizara kuitumia *ATCL* katika kukuza uchumi na sekta ya utalii?

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utalii kupewa fedha za kutosha, naomba Serikali ikisaidie ili kutekeleza majukumu yake vema.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kuipongeza Wizara kupitia kwa Waziri wake, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara yake na kwa kushirikiana na Naibu Waziri na watumishi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Serengeti imo Mkoani Mara na katika maendeleo ya Mkoa kwa ujumla wananchi wa Mkoa wa Mara wanaitegemea hifadhi hiyo kwa mambo mbalimbali kwa mfano kuuza vyakula na bidhaa nyingine.

Mheshimiwa Spika, ili uweze kufanya shughuli yoyote ya kibiashara lazima usafiri kutoka Mara hadi Arusha na kwa sababu hiyo wananchi wa Mkoa wa Mara wanakosa faida mbalimbali zinazotokana na hifadhi ya Serengeti ikiwemo ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu mpango wa Wizara yako kukubali kufungua ofisi ndogo ya *TANAPA* Mjini Musoma ili wananchi wapate huduma hii kwa karibu zaidi na kwa wakati ikiwa ni pamoja na vibali vya magari yanayopita hifadhi ya Serengeti kutolewa Mkoani Mara badala ya Arusha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Shamsha Mwangunga pamoja na uongozi wote wa Wizara kwa kutekeleza vema majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Wizara kwa ushindi ulioupata katika maonyesho ya biashara ya kimataifa yaliyofanyika mwaka huu huko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kuutangaza mji Mkongwe na wa kihistoria wa Mikindani ili tuweze kuongeza vituo vya utalii.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, kutembelea eneo la hifadhi la maingilio ya mto Ruvuma na eneo la *Marine Park* ili aweze kuona jinsi gani Wizara yake inaweza kushirikiana na wananchi wanaoishi maeneo yanayaozunguka hifadhi hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia zote ambazo Mheshimiwa Waziri anazihitaji.

**MHE**. **JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kupata fursa hii adimu ili nichangie katika bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, nimpngeze sana Mheshimiwa Shamsa Selengei Mwangunga (Mb), Waziri mwenye dhamana na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekieli Magolyo Maige (Mb), Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, maliasili na utalii, ni moja ya sekta nyeti sana kwa kuliletea pato Taifa letu, nchi yetu imejaliwa sana kuwa na vivutio mbalimbali ambavyo kwa kiwango kikubwa vivutio hivyo vikitumika vizuri vitaliletea pato Taifa na hata kuitangaza nchi yetu ndani na nje ya mipaka yetu kwa masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uendeshaji wa sekta hizi mbili zinazosimamiwa na Wizara lakini bado naona udhibiti na usimamizi wa baadhi ya mambo muhimu hautiliwi maanani au mkazo, jambo hili linachangia katika kukosesha mapato Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeelekeza zaidi nguvu kwa maeneo ambayo kwa kiwango kikubwa sasa yanajulikana kimataifa kutokana na umaarufu ambao tayari unajulikana kwa kiwango kikubwa. Maeneo ya utalii wa mbuga za wanyama kama mbuga za Serengeti, Ngorongoro, Manyara, Tarangire na kadhalika. Mbuga hizi zinazo sifa hadi ya Kimataifa, ni vema sasa nguvu zikaelekezwa kwa maeneo ya Kusini ambako nako viko vivutio mbalimbali ambavyo vinahitaji msukumo wa Wizara ili vifanye vizuri zaidi.

Naiomba Wizara kupitia mamlaka zake isimamie kwa ufasaha uvamizi na uharibifu wa mazingira katika maeneo mbalimbali yenye hifadhi au maliasili ya Taifa ili iwe sehemu mojawapo ya utalii kwa wageni wanaotembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo kwa miaka ya nyuma yalitambulika kama sehemu ya mbuga na hivyo kukawako na wanyama mbalimbali lakini kutokana na kutokupewa kipaumbele kiutunzaji siku hadi siku hadhi ya maeneo hayo yanazidi kupotea. Mfano mbuga ya Wembere kadri siku zinavyokwenda wanyama wamepotea, msitu unakwenda, uoto wa asili unapotea, mbaya zaidi uvamizi wa ujenzi katika mbuga hiyo umeshamiri.

Mheshimiwa Spika, utunzaji au uendelezaji wa mapori tengefu unahitaji ushauri wa kitaalamu ili mapori tengefu yaendelee kuwako. Kwa hivi sasa Pori la Yulansoni, Kinampanda, Msingi, Kidaru na baadaye Mlima Sekenke halipewi hadhi kama pori tengefu. Naiomba Wizara katika hatua za kuona na kulinda maliasili, itoe kipaumbele kwa pori hili hasa katika utunzaji mazingira jambo ambalo baadaye wananchi watafaidi kwa kuvuna magogo na hata uvutaji wa mvua na kwa matumizi kama shamba la mizinga ya nyuki na kadhalika. Namwomba Mheshimiwa Waziri atambue vivutio vya mawe makubwa yanayopandana na yenye ishara

zinazoweza kuainishwa na vitu mbalimbali. Mawe haya yanapatikana Mkoani Singida kwa Wilaya zote, Manyoni, Singida na Iramba.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nyuki, naomba Waziri atambue uzalishaji wa wafugaji wa nyuki toka Jimboni Iramba Magharibi, naomba wafugaji wapatiwe elimu ya ufugaji, zana bora za ufaugaji na mikopo ili waendane na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara ijishirikishe katika kutafuta wabia wa sekta ya hoteli za kitalii ili waweze kujenga hoteli katika Mikoa mbalimbali za kitalii ikiwemo Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Waziri atueleze/alieleze Bunge lako Tukufu namna ilivyojiandaa kukabiliana na changamoto mbalimbali hasa ushindani soko la utalii kwa kanda yetu ya Afrika Mashariki. Mipango mizuri ya Wizara kutafanya sekta ya utalii kupanda haraka sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli utalii ni sekta inayoliingizia pato kubwa Taifa iwapo shughuli zake zitaendeshwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina bahati ya kuwa na vivutio vingi vya watalii lakini baadhi ya vivutio vimetelekezwa katika maeneo mengi ya Ukanda wa Pwani, wananchi walioishi sehemu hizo walijengo ukuta (ngome) ambao sababu ya kujengwa kuta hizo ni wenyeji wa sehemu hizo wajilinde na watu ambao walikuwa ni wezi wa mifugo. Kuta hizo zipo na zina miaka mingi sana.

Mheshimiwa Spika, hivi ni vivutio ambavyo watu wa zamani waliweza kutumia chokaa, mawe na udongo katika ujenzi na majengo hayo yamedumu kwa muda mrefu na hadi leo yapo na yanaonekana.

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la utalii kupitia mbuga zetu za wanyama. Ukienda Wilaya ya Pangani, kuna mbuga ya wanyama ya Saadani, mbuga ambayo wanyama wake wametembea hadi karibu na bahari. Mbuga hii haijatangazwa ipasavyo. Hivi Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kuitangaza mbuga hii ambayo wanyama wale pia hutembelea pwani.

Mheshimiwa Spika, ni juzi tu kumekamatwa nyara za Serikali katika uwanja wa ndege wa Mwalimu Nyerere. Nyara hizi muhusika aliyetajwa ni raia toka China, inaelekea huu ni mchezo wa siku nyingi lakini siku za mwizi ni arobaini. Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti abiria ambao wanasafiri na mizigo mikubwa ambayo haikaguliwi ipasavyo?

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina bahati ya kuwa na fukwe nzuri ambazo ni vivutio vizuri kwa watalii. Iwapo fukwe hizo zitawekewa utaratibu mzuri wa kuziendeleza. Nchi za wenzetu kuna hoteli kubwa ambazo zinajengwa kwenye fukwe zao hoteli ambazo hujengwa katika maumbo mbalimbali. Kuna hoteli hujengwa hema mfano wa meli nyingine kama samaki.

Mheshimiwa Spika, idadi ya watalii inaelekea kupungua tofauti na miaka ya nyuma. Ziko sababu nyingi zinazopelekea kupungua watalii hawa lakini moja ya sababu japo ni ndogo ni wizi unaofanywa na vibaka ambao huwapora fedha, kamera na vifaa vyao vingine. Je, Serikali ina mikakati gani ya kudhibiti wimbi hili la vibaka ambao huwakatisha tamaa watalii.

Mheshimiwa Spika, kuna raia wengine ambao wanaishi maeneo ambayo yapo karibu na mbuga za wanyama na wakati mwingine wanyama kupita katika maeneo hayo mchana na usiku hali ambayo ni hatari. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa elimu kwa wananchi hao ili wahame maeneo hayo kwa usalama wao? Pia wale wanaoishi jirani na mbuga hizo, ni rahisi kupata nyara za Serikali na kuisababishia Serikali kukosa mapato yake.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, natanguliza kumtakia bajeti njema, mimi mchango wangu ni mchache tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hifadhi zetu, Mkoa wetu ulikuwa na vivutio vya wanyama wengi sana lakini kulingana na pori lile kukosa ulinzi wa Maaskari wa wanyamapori, pori lile lilikuwa la majambazi. Sisi Mkoa wa Kagera ulikuwa kama kitega uchumi lakini sasa tunapata hasara kubwa sana, idadi ya mapori yenye kupendeza kwa utalii wetu yanatoweka. Sasa wakati umefika kutunza wanyama wetu katika mapori hayo, wanyama wameanza kurudi na mapori yenyewe ni Biharamulo, Buligi, Kimisi, Uzuri wa Kondoo, Kihengule na Kihaga. Sehemu hizo zote ni mapori makubwa tu kiutalii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira ya Maaskari wa Wanyamapori, hili suala vijana wengi wanapenda kujiunga, je, ni utaratibu gani unaofuatwa? Vijana hawa wanafuatilia hawapati majibu! Je, kuna mikakati gani ukizingatia mapori yote haya niliyoyataja yako Mkoani kwao?

Mheshimiwa Spika, nashukuru kituo cha Gemu katika pori la Biharamulo kimefufuliwa lakini bado kuboreshwa kwa kuwa na vituo vingine kusaidiana na hicho. Katikakati ya mapori yale tuna vivutio vingine viboreshwe viwekwe kumbukumbu ya Mkoa. Kwa mfano, kama magofu ya mipaka yetu hasa Kyaka iliyoathirika kipindi cha vita vya Iddi Amini Dada, ni utalii mzuri sana na kwa kumbukumbu ya vizazi vijavyo ambao hawajaona vita. Hivyo naomba kituo cha Kiloyeya, Bukoba kiboreshwe kulingana na Mkoa wetu ulivyo lakini Wizara yako ikituunga mkono itakuwa vizuri sana. Najua uchapaji kazi wako, nina imani utatutendea haki mama Mwalimu wangu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tutunze vyanzo vyetu vya utalii pamoja na kulinda wanyama wetu, tuone kama uchumi wetu utakombolewa kwa kutumia ujuzi wako. Pomoja na hayo, nashauri Wizara kushirikiana na Wizara ya Ardhi kutengeana mipaka.

Mheshimiwa Spika, natoa maoni yangu, wananchi kukaa karibu na wanyamapori, pawepo na ulinzi wa Maaskari kwa sababu wanapata madhara makubwa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Karagwe, kuna wataalamu wa kufuga nyuki, naomba waangaliwe, hayo yote ni kupanua wigo wa utalii, hifadhi na mapori yetu. Vitendea kazi ni vichache ukilinganisha na nchi yetu ilivyo. Wizara iendelee kutoa elimu pamoja na hamasi kwa watu walio karibu na wananchi wakati wakitaka ajira kwa kufuata uwiano wa sehemu zilizo na mapori au hifadhi ili waweze kufanya kazi kwa ukaribu sana na kwa moyo mmoja.

Mheshimiwa Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri bajeti njema.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Shamsa (Mb), kwa kazi nzuri anayoifanya kwa ushirikiano na Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Maige, Katibu Mkuu, Watendaji na jamii yote, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri maana inatoa dira ya maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kupongeza Wizara hii kwa ubunifu mkubwa walionao watendaji kwa kubuni njia mbalimbali za kukuza utalii hapa nchini na kuiongezea Serikali mapato makubwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa ushindi walioupata katika maonesho ya Taifa ya sabasaba mwaka 2009, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuutangaza Mlima Kilimanjaro ndani na nje ya nchi. Kama tunavyojua, nchi jirani ya Kenya hufanya njia mbalimbali kupotosha ukweli kwamba Mlima Kilimanjaro haupo Tanzania bali upo katika ardhi ya Kenya lakini Wizara hii imefanya kazi kubwa kuutangaza Mlima Kilimanjaro nje ya nchi na sasa watalii wanafahamu vilivyo juu ya Mlima huu. Wizara ya Maliasili na Utalii, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha wanyamapori Mweka, kwa kweli chuo hiki ni kivutio na kitovu kikubwa cha kupata wataalamu wazuri wa wanyamapori katika Afrika yote maana chuo hiki hakisomeshi Watanzania tu. Kwa hiyo, naiomba Serikali mbali na kwamba inasaidia chuo hiki lakini iongeze fungu zaidi kwa maendeleo ya chuo hiki kwa sababu ni chuo kinachofanya vizuri katika programu zake. Serikali inatakiwa iwezeshe vizuri chuo hiki ili kiweze kujitangaza Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kurudia kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Shamsa na Mheshimiwa Naibu wake, kwa ushirikiano wao katika kuiongoza Wizara hii kwa maendeleo makubwa sana. Mungu ibariki Wizara hii na Serikali iendelee kuiongezea fedha zaidi bajeti ya mwaka wa 2010 – 2011.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%, ahsante.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, hifadhi ya Ngorongoro, ni hifadhi pekee iliyoruhusu watu kuishi ndani ya hifadhi hiyo kwa misingi kuwa waendelee kuishi kwa kufuga na sio kilimo. Kwa maamuzi ya kisiasa, kinyume na sheria, wanasiasa waliamua wananchi wa eneo hilo walime kilimo cha kujikimu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa baadhi ya wananchi badala ya kulima kilimo cha kujikimu wanalima kilimo cha mashamba makubwa. Kutokana na hali hii kuna uwezekano mkubwa kwa miaka ya mbele hifadhi kutoweka. Je, Wizara imechukua hatua gani kuinusuru hifadhi ya Ngorongoro ili kuondokana na hali hiyo?

Mheshimiwa Spika, hifadhi ya Ruaha imepanuliwa kiasi ambacho baadhi ya mashamba ya mipunga hasa kwa wakulima wadogo wadogo yameingia katika mbuga hiyo. Kwa vile wananchi wanategemea kilimo hicho kwa maisha yao, si rahisi kusema waache tu mashamba hayo bila kuwa na utaratibu unaoeleweka wapi wananchi hao wataendeleza kilimo chao. Je, Serikali itachukua hatua gani kulitatua suala hilo?

Mheshimiwa Spika, Mapori ya Akiba ili yaweze kujiendesha kwa ufanisi, ipo haja iundwe mamlaka inayolingana na *TANAPA* badala ya kuwa chini ya Idara ya Wanyamapori. Mamlaka hiyo itaweza kuyaendeleza mapori hayo kwa fedha itakayopatikana pamoja na wafanyakazi wake walio katika mazingira magumu kupata malipo yatayowawezesha kuifanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali ina mashamba kumi na sita (16) ya mbao hususan mbao laini lakini taarifa zilivyo, ni kuwa bei ya mbao hizo laini ni kubwa kuliko mbao zinazotoka nchi jirani. Hali hiyo inasababisha gharama za ujenzi kuwa kubwa katika kujenga paa ambapo mbao laini hutumika. Pia hivi sasa Mufindi ambapo ndipo lilioko shamba la *Sao Hill* inasemekana kitanda badala ya kuzwa kwa Shs.14,000/= sasa kinauzwa Shs.70,000/=. Je, naiomba Wizara inieleze, kupanda kwa bei ya mbao kiasi hicho kumetokana na nini? Je, Serikali itafanya nini kuhakikisha bei hizo zinapungua?

Mheshimiwa Spika, ukataji wa miti katika maeneo yetu ni mkubwa mno hususani kwa ajili ya kupata nishati ya kupikia kwa kuwa suala la uhifadhi wa mazingira ni mtambuka. Je, Wizara ina mpango gani kushirikiana na taasisi nyingine ili ipatikane nishati mbadala ya kupikia badala ya kuni na mkaa ili kuepusha ukataji mkubwa wa miti?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kupongeza kwa dhati Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa S. Mwangunga (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa H. Maige (Mb), Katibu Mkuu na watendaji wengine wa Wizara hiyo na taasisi zake kwa hotuba nzuri na kazi nzuri ya kutunza na kuendeleza maliasili na utalii.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mkinga imebahatika kwa kupandishwa hadhi Pori la Mkomazi kuwa hifadhi ya Taifa ya Mkomazi. Bila shaka, Wilaya ya Mkinga itafaidika na manufaa ya hatua zinazoambatana na kupandishwa hadhi Hifadhi ya Mkomazi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na kupandishwa hadhi kwa Hifadhi ya Mkomazi, kumepelekea baadhi ya wananchi wafugaji ambao wamekuwa wakiiishi katika eneo lililopandishwa hadhi kulazimika kuhama kwenda nje ya hifadhi. Kwa kuwa wananchi hao wamekuwa wakiishi katika eneo lililokuwa Pori la Akiba kwa muda mrefu na kwa kuwa walikuwa wanajijengea makazi na miundombinu ya visima na malambo, waliomba wapatiwe muda ili waweze kujijengea makazi na miundombinu katika maeneo mapya ambapo wataruhusiwa kuhamia. Ni jambo la kusikitisha sana kwamba maombi hayo ya muda mrefu na ambayo niliyasimamisha zaidi ya miezi mitatu iliyopita, hayapatiwi jibu pamoja na kufuatilia mara nyingi sana, wangependa *WMA*.

Mheshimiwa Spika, wananchi wafugaji hawa sio tu wamechoshwa na mtindo wa kuchunga kwa kuhamahama bali pia wangependa kuzingatia ipasavyo Sera ya Taifa ya kufuga katika mahali rasmi. Woga mkubwa wa wananchi hawa sio tu wanaweza wakatimuliwa kikuku *(unceremoniously)* hapo walipo sasa bali pia hata huko wkwenye pori tengefu wanapotakiwa wahamie wanaweza wakaja wakaondolewa pindi sehemu hiyo nayo itakapopandishwa hadhi.

Napenda kuishauri Wizara ifikirie ombi hili mapema na lipewe uzito unaostahili ili kuupatia ufumbuzi kero hii kubwa wananchi wafugaji wa eneo la Kimuni katika kata ya Mwanjembe, Wilaya ya Mkinga katika eneo la hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo ambayo Wilaya ya Mkinga inatarajia kufaidika ni pamoja na *TANAPA* kuchangia katika miradi ya jamii ikiwa ni pamoja na ujenzi wa shule, zahanati, kituo cha afya, miradi ya maji na barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara, ni dhahiri kwamba barabara itokayo Mwanjembe kupitia Kimuni kuelekea Wilaya ya Lushoto, itahitaji maboresho makubwa iwapo matarajio ya kuendeleza utalii katika sehemu hiyo ya Hifadhi ya Mkomazi inatarajiwa kupata mafanikio yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la faraja ni kwamba *TANAPA* inashirikiana na wananchi katika masuala ya ulinzi shirikishi. Kwa kuwa idadi ya wanyamapori na pia majangiri inatarajiwa kukua kutokana na maboresho ya hifadhi, hapana budi ushirikiano wa *TANAPA* uwe mkubwa zaidi ili kupambana dhidi ya ujangili na kuwalinda wananchi pamoja na mazao yao dhidi ya uharibifu wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha *Kibo Match*, kina hatari ya kufungwa na kupoteza ajira nyingi. Hii inatokana na kodi kubwa na manufaa mengine kutokana na mgao mdogo sana wa magogo ya kutengenezea viberiti. Nashauri Wizara ifikirie kuongeza mgao wa magogo kwa kiwanda ili kuweza kuzalisha kwa tija na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia 100%.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia mambo machache kwenye bajeti hii kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori ya mwaka 2008. Ni karibu mwaka sasa tangu Bunge lako lipitishe Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori ya mwaka 2008. Jambo la kusikitisha ni kwamba, sheria hiyo bado haijatungiwa kanuni. Naomba kanuni zikamilishwe mapema ili sheria hiyo nzuri ianze kutumika kwa faida ya uhifadhi wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, ujangili kwenye hifadhi, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara katika kupambana na ujangili/uwindaji haramu, bado ujangili/uwindaji haramu unafanywa kwa kiwango cha juu sana. Ujangili/uwindaji haramu hufanywa kwa kiwango cha juu sana katika mapori ya Akiba ya Usangu, Wilayani Mbarali. Nashauri Serikali kupitia Wizara hii, iongeze juhudi za kulinda wanyama wetu. Aidha, nashauri Wizara ifuatilie kesi zote ambazo zipo Mahakamani na kuona matokeo ya kesi hizo. Nashauri pia kwamba Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori ya mwaka 2008 ianze kutumika mapema inavyowezekana ili iwabane majangili na wawindaji haramu.

Mheshimiwa Spika, Kimondo cha Mbozi *(Mbozi Meteriorite).* Mwaka jana wakati wa bajeti ya Wizara hii, nilizungumzia Kimondo cha Mbozi kutotunzwa vizuri.

Aidha, nilizungumza kwamba kimondo hicho bado hakijatangazwa vizuri humu nchini na duniani. Narudia wito wangu wa mwaka jana; Wizara ione umuhimu wa kukitunza yaani kuboresha mazingira ya kimondo hicho kwa kujenga jengo zuri na kuweka/kuajirii mtaalamu (Mwanasayansi) kwa ajili ya kutoa maelezo kwa wale wote watakaokitembelea kimondo hicho kwa minajili ya kujifunza. Naomba pia Wizara ifanye jitihada zaidi za kukitangaza kimondo hicho ili watu wengi zaidi wakitembelee na hivyo kutuingizia kipato.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana ni Shs. Milioni tano (5) zilitengwa kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kimondo hicho. Hata hivyo, kiasi hicho ni kidogo sana kwa kazi hiyo. Naiomba Wizara ione umuhimu wa kutenga fedha zaidi kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, *Bismillahi Rahman Rahim.*

Mheshimiwa Spika, ninachukua fursa hii, kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utaliii kwa hotuba yake ambayo imejaa maelezo na taratibu fasaha za utekelezaji wa shughuli za sekta mbalimbali katika Wizara yake hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii, ki-Katiba sio suala la Muungano, lakini ninawapongeza watendaji wa Wizara hii, hasa katika sekta ya utalii kwa kuweka mazingira yanayovutia shughuli za utalii, lakini kwa ushirikiano wao na Wizara ya Utalii ya kule Zanzibar kwa mambo ambayo wanakubaliana na kuwa katika mazingira yanayofanana. Mbali na ushirikiano huo wa Wizara zetu hizo mbili, ninaona yapo mambo machache ambayo ninapenda kumwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake kuyaangalia kwa ukaribu zaidi na kuona ya kuwa yanaongezewa ushirikiano ili kuwaongezea kipato zaidi wananchi wetu na kuona kuwa shughuli za utalii na maliasili yanakuwa na sehemu kubwa zaidi katika kuinua hali za kuondosha umaskini na kutekeleza mpango wa MKUKUTA na MKUZA.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo ninayalenga ni kama vile kuimarisha bandari ya Zanzibar katika kuvutia meli za utalii kutembelea Zanzibar kama ilivyoainishwa katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa bandari ya Tanzania Bara katika kuiletea fedha zaidi na kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kushirikiana katika kupatiwa masoko ya vitu vinavyotokana na mazao ya asili hasa yanayotokana na mazao ya ufugaji wa nyuki (asali na nta) ambavyo vimerundikana kule Zanzibar kama ilivyokuwa hapa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kuendeleza ugunduzi wa mafuvu ya binadamu wa zamani sio tu katika bonde la Oldpai bali hata kule Zanzibar ambako tunasikia kuwa nako limegunduliwa fuvu la binadamu wa zamani katika pango lililoko kule Jambiani Wilaya ya Kusini Unguja katika pango la Kuumbi – Mfumbwi.

Mheshimiwa Spika, zao la mwani katika miji na vijiji vya Pwani mwa bandari ya Hindi, ni jambo ambalo linahitaji kuzingatiwa kwa umakini zaidi ili mbali na kuwaletea fedha wananchi wanaoishi katika maeneo hayo pia wadumishe mazingira na kuwavutia wageni katika shughuli za utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, ninaiomba Wizara hii kuendelea na kuelekeza kwa dhati nguvu zake katika kuhifadhi, kulinda, kuendeleza, kudumisha, kuvuna maliasili pamoja na kuwaelimisha wananchi faida za kuyatekeleza yote hayo na faida ya Taifa letu. Vile vile ihakikishe kuwa mashirikiano ya dhati yanahitajika katika mafanikio yake. Mungu awazidishie kila la kheri watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Hai, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote hapo Wizarani, kwa kutuletea hotuba nzuri, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, pia niwapongezeni sana kwa ushindi katika maonyesho ya 33, Sabasaba kule Dar es Salaam. Ninaomba nichangie katika mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mapato yatokanayo na utalii wa Mlima Kilimanjaro. Kama ambavyo sisi Wabunge wa Halmashauri tano zinazozunguka Mlima Kilimanjaro tulipendekeza na kushauri umuhimu wa kupewa gawio rasmi *(i.e percentage)* ili wananchi waweze kutambua na kuthamini uhifadhi wa Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, njia mpya ya kupanda Mlima Kilimanjaro. Ile barabara inayojengwa kwa kiwango cha lami kwa ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, Kwasadala – Masama na ambayo watalaamu wenu *TANAPA/KINAPA* wanaifahamu vizuri, ni muhimu mchakato wake ufanyike haraka zaidi ili kuongeza kipato kwa Taifa na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, bei ya magogo. Ni busara zaidi ikaangaliwa upya kwani ni ya juu sana na madhara yake yako wazi hali inayopelekea uagizaji wa magogo kutoka nchi jirani lakini mbaya zaidi wananchi wengi kushindwa kumudu bei ya mbao sokoni.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuongeza jitihada zaidi katika kuvitangaza vivutio mbalimbali nchini tulivyojaliwa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii na kuwatakieni kila kheri katika utekelezaji wake, mbarikiwe sana.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuamka salama, nasema *Alhamdullillah.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umahiri wako, Naibu wako pamoja na Wenyeviti wako, ninasema ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani zangu kwako, napenda kutoa shukrani zangu kwa Waziri wa Wizara husika kwa hotuba yake iliyojaa matumaini ya kukuza uchumi wa nchi yetu pia kumwezesha mwananchi kuiona nuru ya maisha bora kwa kila Mtanzania. Wizara ya Maliasili na Utalii, ni Wizara inayoweza kuipatia nchi yetu uchumi pia inaweza kuwa chachu ya kuua utamaduni wetu. Kwa kuangalia utamaduni wa Kitanzania unaporomoka siku hadi siku na inaonekana wazi mila zetu zinatoweka na kutawaliwa na utamaduni wa nje. Hivyo basi Wizara itueleze hali ya kunusuru utamaduni wetu ikoje?

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya maeneo ya wafugaji na wanyamapori, iko hoja Wizara iwatendee haki wafugaji kwani inaonekana wafugaji wametengwa sana na wakulima pia na Wizara hii. Wafugaji mara nyingi huonekana ndio wakosa na kulazimika kuhukumiwa na kumbe hawana kosa. Mara nyingi maeneo yao huchukuliwa. Kuna baadhi ya maeneo ya wafugaji yanachukuliwa na maeneo ya wanyamapori. Je, Serikali imechukua hatua gani kunusuru migogo hii kwa maeneo hayo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu magogo, pamoja na jitihada ya Serikali kudhibiti magogo yetu, bado njia za panya zimo nchini na zinapitisha magogo yetu. Kitendo hiki kinaipunguzia nchi yetu kipato. Kwa kuwa kitendo cha wizi huu unakua siku hadi siku, napenda kufahamu, je, Serikali imejiandaa vipi kuziba njia hizo za panya ili kunusuru magogo yetu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu viza kwa watalii, mara nyingi kumejitokeza utaratibu wa watalii kulipia fedha za utalii wao huko nje kitendo hiki ni kibovu sana kwani kinaikosesha nchi yetu pato. Pamoja na kelele za baadhi ya Wabunge kuiomba Serikali iondoe utaratibu huo, bado Wizara haijaweza kusimamia suala hilo na bado viza zinazowaingiza watalii hapa nchini, sisi tunapewa

asilimia ndogo sana jambo ambalo hupelekea kukosa kipato cha nchi yetu. Naomba kueleweshwa, ni kigugumizi gani kinachoizuia Wizara kuruhusu Makampuni ya nje kupokea malipo yote nje na kupelekea Serikali kupoteza kodi kubwa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga (Mb), mpenzi wangu, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige (Mb), mwanangu mpendwa, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuboresha Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kutoa mchango wangu, napenda kutamka rasmi kuwa ninaunga mkono bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii mia kwa mia nikiwa ninaimani kuwa mikakati yao yote wataitekeleza vema pamoja na mchango wangu ambao Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii watanipa majibu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuikumbusha Serikali kuwa Askari wa Wanyamapori, ni muhimu sana kwa kulinda vitalu vya uwindaji ili majangili yasiendelee kuhujumu utajiri wa nchi yetu kupitia wanyama. Ingawa Serikali imekuwa ikiwaajiri Askari wa Wanyamapori lakini bado ni wachache sana hasa misitu ya Manyoni na Singida vijijini ambapo bado yana simba ambao ni tishio kwa wananchi wanaopita kwenye maeneo hayo kwa shughuli mbalimbali za kijamii. Nitashukuru Waziri akinisaidia kutuongezea Askari.

Mheshimiwa Spika, magari kwa Askari wa Wanyamapori Manyoni na Singida Vijijini. Kwa kuwa matukio ni mengi ya Idara ya Maliasili na Utalii, Wilaya ya Manyoni mfano tembo na simba bado ni tishio kwa wananchi hasa maeneo ya Doroto, Msisi, Sanjaranda, Gurungu (Mkiwa), Ipande na kadhalika na kwa kuwa Idara ya Maliasili na Utalii Wilaya ya Manyoni haina gari, ninaiomba Serikali kutafuta uwezekano wa kupeleka gari Wilayani Manyoni pamoja na Singida Kusini ili Askari na watendaji wawe wepesi kwenda kutoa msaada maeneo yanayokumbwa na matatizo ya wananchi kushambuliwa na ndovu au simba kwenye maeneo niliyoyataja. Endapo Serikali itapokea hoja hii, nitafarijika kwa niaba ya wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kuainisha vivutio vya utalii vipya Mkoani Singida, napenda kuipongeza Serikali kwani imejitahidi kuibua vivutio mbalimbali vya watalii katika nchi yetu. Pamoja na maeneo mbalimbali yaliyoainishwa na Serikali lakini bado kuna vivutio vingi sana ambavyo bado Serikali haijavitambua rasmi.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iendelee kubaini vivutio vingine ili watalii wanaoingia nchini waendelee kuvutiwa na kuendelea kurudi Tanzania kuja kutalii nasi tuendelee kunufaika kwa kuinua paato la utalii.

Mheshimiwa Spika, napenda Serikali ielewe kuwa Mkoani Singida tunavyo vivutio vingine ambavyo endapo vitatambulika rasmi, watalii wataanza kufika Singida na pato la Mkoa wetu litaongezeka. Vivutio hivyo ni kama, mlima wenye alama maalum yenye kuonyesha *centre* au katikati ya nchi Tanganyika uliopo kijiji cha Sukamahela kata ya Sorya, tarafa ya Kilimatinde, Wilaya ya Manyoni, Mkoani Singida. Ni vema Serikali ikatambua eneo hili.Vile vile Singida kuna mapango ya Wakoloni wa Kijerumani huko Iramba pamoja na ngome za Machifu wa zamani mfano, Mtemi Gelege iliyopo Kisiriri, Kiomboi Iramba pamoja na Chifu Senge Marehemu iliyopo Singida Mjini kata ya Utemini na Sepuka Singida Vijijini (Kusini) Chifu huyu alifuga wanyama mbalimbali ikiwa ni pamoja na simba.

Mheshimiwa Spika, asilimia ya uwindaji, napenda kutoa shukrani kwani Serikali inatoa asilimia ya uwindaji katika Wilaya ya Manyoni kwa sababu ya misitu ya uwindaji. Ninaishauri Serikali kuongeza kiwango hiki cha mrahaba kwani ni kidogo bado hakiendani na faida Serikali inayoingiza kupitia vitalu hivi vya uwindaji vilivyopo nchini pamoja Manyoni Singida. Ninapenda kuieleza Serikali kwamba Mkoa wa Singida unayo asali nyingi sana ambayo inasaidia kukuza pato la Taifai letu. Maeneo yanayotoa asali nzuri sana na nyingi ni pamoja na Wilaya ya Manyoni na

Wilaya ya Singida (Kusini). Jambo la kusikitisha ni kwamba asali hii nyingi bado haina soko la uhakika, ninaiomba Serikali isaidie kupata soko.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mungu kwani hata Mkoa wa Singida una miti ya mbao ambayo ni urithi wa Taifa pamoja na wana Singida. Jambo la kusikitisha ni kwamba bado kuna upasuaji mbao haramu nikiwa na maana wapasuaji hawana leseni na uuzaji wa mbao ambazo hazina mhuri yaani za wizi. Ninaomba Serikali kuweka ulinzi mkali kwani pato la nchi linapotea.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kumsaidia mwananchi wa kata ya Rungwa ambaye ni mlemavu aliyechimba kisima chenye kina kirefu kwa mkono mmoja tu, fedha za kununulia genereta na vifaa vya kumwezesha kuvuta maji kwa umwagiliaji bustani na matumizi mengine kwa jamii kubwa. Nawashukuru sana kwa niaba ya mwananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nimalizie kwa kuunga mkono bajeti hii mia kwa mia nasubiri ufafanuzi wa hoja zangu.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara kwa mwelekeo mzuri wa kuwajali wananchi wanaoishi sambamba na mbuga za Akiba za Rungwa, Mhesi, Kizigo na maeneo ya uwindaji ya Chaya. Nimeuliza viongozi wa kata za Rungwa, Mgandu na Itigi kuhusu mahusiano kati ya watumishi wa Maliasili na wananchi na wamekiri kuwa mahusiano ni mazuri sana.

Aidha, niishukuru Wizara, Idara ya Wanyamapori na Mfuko wa Hifadhi kwa kuamua kujenga upya bwawa la Rungwa mwaka huu. Aidha, pia nishukuru kwa misaada kwa wajasiriamali, shule, zahanati na sekta ya maji. Nashauri fedha zaidi zitengwe kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa kutokomeza tatizo sugu la maji kata za Rungwa, Mgandu, Itigi, Sanjaranda, Ipande na Idodyandole Wilayani Manyoni.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Wanyamapori waharibifu bado yapo hususan tembo na nyani kuharibu mazao ya wananchi. Ukosefu wa risasi na usafiri kwa Magemu unachangia matatizo. Pia kwa Wilaya ya Manyoni, kwa mwaka 2008 hakuna fedha iliyopokelewa kutokana na 25% ya uwindaji wa kitalii na hivyo kusababisha matatizo zaidi kwa watendaji kukabiliana na wimbi la wanyamapori waharibifu. Naomba maelezo juu ya hili.

Mheshimiwa Spika, kifuta jasho/machozi kwa maisha na uharibu wa mazao, bado ni kitendawili pamoja na nyaraka kupelekwa Wizarani kupitia *KDU* Manyoni bado malipo hayajafanywa. Jimboni kuna watu watano (5) waliouawa na simba na tembo lakini mpaka sasa hakuna kilicholipwa. Naomba maelezo juu ya tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara ije na Muswada wa kuundwa kwa Bodi ya Asali na Nta. Mazao haya yanapanuka kwa kasi nchini, kuna miradi mingi sana ya asali imeanzishwa lakini hakuna chombo imara kinachounganisha upatikanaji wa mazao haya ya nyuki. Nilipendekeza tokea mwaka 2007, naomba majibu ni kwa nini Serikali hailitilii maanani zao la asali na nta ? Ni kama vile mazao haya yanaendeshwa kiholela au kwa ulanguzi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. DR. CYRIL AUGUST CHAMI:** Mheshimiwa Spika, pongezi zangu kwa viongozi wa juu na watendaji wote wa Wizara hii muhimu. Kwa kuwa hifadhi ya Mlima Kilimanjaro inaongoza katika kuliingiza Taifa pato kati ya hifadhi zote na kwa kuwa ili hifadhi iweze kutoa/kuwa kivutio kwa watalii muda wote, ni muhimu sana ikalindwa na wakazi wazungukao mlima. Nashauri Wizara iangalie jinsi ya kusaidia program ya kupanda miti katika Wilaya zote zinazozunguka mlima. Watu wakiwa na miti, hawataingilia hifadhi ya mlima na pia watauona mlima huu kama chanzo cha wao kusaidiwa, hivyo kuulinda na hata kusaidia kwa hiari katika kuzuia uharibifu wa mioto na hata majangili.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Halmashauri za Mkoa wa Kilimanjaro (hususan zilizinazozunguka mlima za Rombo, Siha, Hai na Moshi), kupewa sehemu ya mapato ya *KINAPA* kwa shughuli za maendeleo, ni ombi la wananchi karibu wote wa Mkoa wa Kilimanjaro. Kama kampuni za madini na *reserves* zinalifanya hili na kwa *KINAPA* linawezekana pia ukizingatia kwamba migodi ni ya makampuni binafsi ilihali *KINAPA* ni ya umma.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ELISA DAVID MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga, kwa hotuba yake nzuri na nampongeza yeye binafsi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote, kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii. Maliasili na Utalii, ni sekta muhimu sana katika uchumi wa Taifa letu. Wizara hii inachangia asilimia 16.7% ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, utalii ni sekta kiongozi kwa kuchangia fedha za kigeni kutokana na watalii wanaokuja kuona fursa mbalimbali za utalii ukiwa ni pamoja na mbuga za wanyamapori pamoja na uwindaji wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, takwimu za mapato ya fedha za kigeni katika sekta hii ya kitalii, zinaonyesha kuwa katika miaka miwili ya 2007/2008 na 2008/2009, idadi ya watalii waliokuja Tanzania imeshuka kwa asilimia 10% na kipato cha fedha za kigeni pia kimeshuka kutoka dola za Marekani 388 milioni mwaka wa 2007/2008 hadi dola za Marekani 302 milioni katika mwaka wa 2008/09. Huu ni upungufu wa dola 86 millioni katika kipindi cha miaka miwili ya 2007/08 na 2008/2009. Mwenendo huu wa kupungua kwa idadi ya watalii na fedha za kigeni, hauridhishi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tawimu hizi, pamoja na mtikisiko wa uchumi duniani, ni vema Wizara ijitahidi kubuni mbinu mbalimbali ili kuongeza ufanisi na tija zaidi katika sekta ya utalii, kwa nia ya kuendelea kuhifadhi mazingira, maliasili na fursa zinginezo za utalii ikiwepo wanyamapori na mbuga za hifadhi za Taifa. Katika kutekeleza majukumu hayo, nashauri Serikali izingatie baadhi ya haya yafuatayo:-

(a) Hadhi ya Hifadhi ya Ngorongoro imeshuka sana kutokana na kuongezeka kwa shughuli za binadamu. Kumekuwa na ongezeko la watu wanaoishi na kuendeleza shughuli za kilimo na ufugaji katika hifadhi hii. Hivi sasa kuna watu zaidi ya 70,000. Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii isitishe shughuli za kilimo na ufugaji katika hifadhi hii ambayo ni kivutio kikubwa cha utalii.

(b) Kupunguza gharama za visa kwa watalii ili kulingana na nchi za jirani kwa nia ya kutoa unafuu wa gharama kwa watalii wanaokuja Tanzania.

(c) Kuongeza jitihada za kutangaza fursa za utalii za nchi yetu kwenye nchi mbalimbali na kutumia vyombo mbalimbali licha ya *CNN* na *BBC.*

(d) Kuajiri na kutoa matunzo kwa wafanyakazi wa ngazi mbalimbali wakiwemo Askari Wanyamapori na kuwapa silaha zinazoweza kukabiliana na ujangili na uwindaji haramu katika hifadhi za Taifa.

(e) Serikali isimamie kwa karibu uvunaji wa mazao ya misitu kama magogo na mbao katika misitu yake kwa nia ya kudhibiti ubora na kiasi kinachovunwa na hatimaye kudhibiti mapato yatokanayo na mauzo ya mazao haya.

(f) Kutazama upya bei ya fursa ya uwindaji wa kitalii pamoja na kuongeza idadi ya vitalu vya uwindaji.

(g) Wizara isimamie kwa karibu taasisi zake za kufundishia wafanyakazi wake katika fani mbalimbali.

Chuo cha wanyamapori cha Mweka kilichoko Moshi Mkoani Kilimanjaro, kina nafasi ya pekee katika kufundisha wafanyakazi wa wanyamapori.

Chuo hiki kinakabiliwa na upungufu mkubwa wa magari ya kuwapeleka wanachuo katika masomo yao ya vitendo. *(Field Training).* Tatizo hili ni kubwa kiasi ambacho kinaweza kuwaathiri wanachuo hawa wasipate mafunzo hayo ya vitendo. Nashauri Serikali ikipatie chuo hiki magari kwa shughuli za *field training*.

(h) Wizara isimamie kwa karibu huduma zinazotolewa na hoteli zinazohudumia watalii. Viwango vya huduma muhimu zisimamiwe kwa karibu ;

(i) Mwisho, naipongeza Wizara kwa kupambana na vitendo viovu katika Wizara na katika taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, natamka kwamba naunga mkono hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Ngara, kuna uharibifu wa mazao ya wakazi wa Kata ya Murusagamba, Muganza na Bugarama unaofanywa na tembo. Tembo hao hutoka katika hifadhi ya Burigi kwenda mpaka kwenye mashamba ya wananchi wanaoishi katika Kata hizo tatu. Naomba Idara ya Wanyamapori ifanye jitihada ya kudhibiti idadi ya tembo waliopo katika hifadhi ya Burigi ili waweze kupunguzwa au kufukuzwa kutoka kwenye makazi ya watu. Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori (Mweka), ina shughuli muhimu ya kufundisha wahifadhi wa wanyamapori. Hiki ni kituo muhimu katika kutoa mafunzo ya wahifadhi ambao wanatumika katika hifadhi zote nchini. Lakini chuo hiki kinapewa fedha kidogo sana kwa ajili ya maendeleo. Kwa sasa magari kwa ajili ya mafunzo ya *field* yamechoka na kuchakaa sana. Serikali inaombwa kupeleka pesa ya kutosha ili Mweka waweze kununua magari mapya ili wanachuo waweze kupata mafunzo bora.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), ndiyo taasisi pekee inayofanya utafiti katika Tanzania. Taasisi hii ni muhimu sana kwa sababu inatufanya tujue idadi ya wanyamapori waliopo hapa nchini. Lakini cha kusikitisha, taasisi hii inapewa pesa ndogo sana kwa ajili ya mafunzo ya watafiti *(graduate students).* Naomba Serikali ielekeze pesa nyingi kwenye taasisi hii ili tupate wataalamu wa utafiti wa wanyamapori.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo, ninayo machache ambayo napenda, Wizara iyatolee ufafanuzi na majibu.

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Moyowosi, Wilayani Kasulu. Pori hili lipo pia katika Jimbo langu la Kasulu Mashariki na katika eneo hili wapo wawindaji wa kitalii lakini Halmashauri ya Wilaya inapata fedha kidogo sana. Ninaomba sana Wizara yako ifanye ukaguzi wa mara kwa mara ili wawekezaji hawa walipe malipo husika 25% kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Aidha kampuni ya *TGT Ltd*. inayowinda Kasulu, imekuja eti kuomba kibali cha kupiga picha eneo hilo. Halmashauri ya Wilaya wameandika barua Wizarani ili kupata mwongozo wa aina hii ya biashara ya kupiga picha. Ni lini Wizara yako itajibu barua hiyo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu? Barua hiyo tangu imetumwa kwako Wizarani ni miezi saba (7) sasa. Tafadhali jibu barua hiyo haraka!

Mheshimiwa Spika, elimu ya umma ya uhifadhi na misitu. Mheshimiwa Waziri, kumekuwepo na migogoro ya ardhi kati ya hifadhi ya misitu ya *North and South Makere,* Wilayani Kasulu na wananchi. Ninaomba fedha za kuendesha elimu kwa umma kuhusu uhifadhi na misitu. Vipo vijiji zaidi 14 ambavyo vinahitaji mafunzo haya, Halmashauri Wilaya Kasulu na ofisi ya Mbunge Kasulu Mashariki, vitasaidiana na Wizara yako kuendesha mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, mipaka mingi ya mapori ya misitu yalikuwa *Gazetted 1956* chini ya Sheria ya Waingereza. Ninashauri *'up-date'* ya nyaraka zote zihusuzo *forest reserves.* Baadhi ya vijiji chini ya *Operation* Kigoma mwaka 1972, inasemekana vimo ndani ya hifadhi ya misitu. Mfano,

vijiji vya Kigembe, Zeze, Kagera, Nkanda, Mvinza na sehemu za kijiji cha Mvugwe inadaiwa vimo ndani ya hifadhi/misitu. Ninaomba timu yako ije ifanye uhakikji wa ramani hizo.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Moto Kichaa. Hili limekuwa tatizo sana katika maeneo mengi ya Wilaya ya Kasulu. Ninashauri Wizara yako, Kitengo cha Misitu kishirikiane na Halmashauri ya Wilaya, ili kuendeleza kutoa mfunzo, kusaidia kusimamia sheria zilizopo na hata kubuni mbinu mpya za kusaidia kuzuia tatizo hili. Tuleteeni fedha za *capacity building, community sensetization programe etc.* Tshs.50 million zinaweza kusaidia hasa katika vijiji 14 vilivyo jirani na mapori mengi ya misitu. Pia Ofisi ya misitu Kasulu inaweza kuandaa *'project proposal'* kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, uhifadhi wa Ardhioeve Malagarasi Wetland. *Malagarasi Wetland,* ni sehemu ya urithi wa dunia – chini ya mkataba wa Ramsah. Ninapenda Mheshimiwa Waziri anieleze ni nini hasa Wizara inafanya *on Malagarasi Wetland.* Ni kitu gani hasa Wizara inafanya *on protection of this important wetland?* Je, program ya uhifadhi wa ardhioevu inashirikishaje jamii inayozunguka/eneo Mto Malagarasi unakopita? Ninaomba maelezo ya kina.

Mheshimiwa Spika, Sheria mpya ya Wanyamapori ya mwaka 2009, ni lini Sheria hii itaanza kutumika baada ya Bunge kuipitisha? Je, Kanuni zake zitakuwa tayari lini? Ninafahamu yana mchakato huo, lakini kwa sababu ya umuhimu wa Sheria hiyo mpya na hasa *'WMA."* Nashauri, Mheshimiwa Waziri uongeze kasi ya kuandika Kanuni haraka ili Sheria hii ianze kazi mara moja.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kigoma - Gombe National Park. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alifungua barabara ya Chankere - *Gombe National Park,* Wilaya ya Kigoma Vijijini, June, 2009. Barabara hii inasaidiwa/inafadhiliwa na *WFP* chini ya *Program ya Food for Work.* Ninaishauri *strongly TANAPA* na Wizara yako msaidie juhudi ya wananchi na *WFP* ili barabara hii ikamilike mapema. Hadi sasa, Wizara yako haijachangia chochote ujenzi wa barabara hii muhimu, barabara hii itaongeza biashara ya utalii katika mbuga hii.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Maige (Mb), Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa kazi yao nzuri na hotuba yao nzuri hongera sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mtikisiko wa uchumi, watalii wengi waliotarajia kuja Tanzania mwaka 2008/2009, waliahirisha safari zao na kuleta hasara kubwa kwa wenye hoteli, shirika la TANAPA, Ngorongoro na Watanzania. Kwa ujumla kupungua kwa watalii kumeathiri vibaya sana wafanyakazi wa TANAPA, Ngorongoro na waliokuwa wanyakazi mahotelini. Pia uhifadhi umeathirika sana na ndio tembo wengi sasa wanauwawa, Serikali inatakiwa ijipange na iweke mkakati wa kuhakikisha utalii hauathiriki kutokana na mtikisiko wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, *TANAPA* na Ngorongoro lazima bodi zake ziachiwe kufanya maamuzi namna ya kuendesha mashirika haya badala ya kuingiliwa na viongozi toka Wizarani. Ni maamuzi mabaya yaliyofanywa na viongozi toka Wizara ndio yamesababisha *TANAPA* kufilisika leo maana fedha zao zilizokuwa kwenye *reserve* zilichotwa na kutumika kwa mambo ambayo sio ya uhifadhi, leo shirika limefilisika na wafanyakazi wameshindwa kuongezewa mishahara na miradi yote ya maendeleo kusimama. Hivi fedha yote ile iliyokuwa kwenye *reserve* hadi February, 2008 zilienda wapi?

*TANAPA* inafanya kazi muhimu sana na lazima tuhakikishe mapato yake yanatumiwa vizuri na kama hayatoshi basi Serikali iipatie fedha zaidi ili iweze kuendesha shughuli zake na

wafanyakazi walipwe mishahara na marupurupu wanayostahili kwani mazingira wanayofanyia kazi hayawaruhusu kupata kipato zaidi ya mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kujenga hoteli za ghorofa tano kwenye hifadhi, zitaua utalii Tanzania. Hivi watalii kulipa US$ 1500 kwa siku kwa malazi kwa mahoteli kama Gurumeti, Kilawira na Kimpisike, kwa wakati huu wa mtikisiko wa uchumi ni sawa? Nenda South Africa, bei haizidi US$ 100. Nenda leo Gurumeti hamna mtalii na hoteli imejaa popo. Lazima tujenge hoteli nyingine kwa watalii wa kawaida na Watanzania wa kawaida waweze kwenda kwenye hifadhi kUtalii na kuongeza pato. Hivi suala la *Consession Fees* limefikia wapi? Hili lingeshaanza kufanya kazi kama lisingeingiliwa na viongozi toka Wizarani.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa ya kuchangia hoja hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga na Naibu wake, pamoja na timu yake yote ya Wizara kwa maandalizi na uwasilishaji wa hoja ya Wizara hii nyeti na muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, soko la utalii Tanzania, Serikali iongeze juhudi kuitanga Tanzania katika biashara ya utalii. Bado Kenya na Uganda wametupita katika kutangaza utalii wa nchi zao, licha ya hata kutumia rasilimali zetu kama zao.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii, ni sekta ambayo ingeweza kuwanufaisha wanawake kiuchumi hasa ufugaji nyuki na kadhalika. Tatizo kubwa ninaloona mimi, ni uchache wa watumishi wanawake katika sekta hii na Wizara nzima. Serikali iongeze idadi ya watumishi wanawake katika Wizara hii ili wasaidie kuibua miradi itakayowanufaisha wanawake na kuharakisha maendeleo ya jamii (siyo rahisi wanaume kulenga miradi ya wanawake).

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkoa wa Manyara wamezungukwa na hifadhi katika baadhi ya maeneo. Tunaomba Serikali isaidie kukuza *'cultural toursm'* hasa kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi. Wananchi wetu wa Manyara wana mambo mengi ya kiutamaduni ambayo wakiwezeshwa watanufaika nazo kutokana na watalii watakaotembelea maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Manyara, wengi wao ni jamii ya wafugaji ambao hawakopesheki na hivyo miradi ya ujasiriamali ifanyikayo kwa kutumia mikopo ya *SACCOS* na kadhalika haiwanufaishi. Naiomba Serikali/Wizara iipe kipaumbele suala hili la kuwanufaisha wananchi wetu kutokana na utalii katika maeneo yao, ili nao waboreshe maisha yao na kunufaika na juhudi za Serikali za kuinua wananchi kiuchumi. (Mabilioni ya J.K. haziwafikii – haziwanufaishi)

Mheshimiwa Spika, uhamasishaji utalii wa ndani. Zamani wakati wa ukoloni, Watanzania hawakukanyaga kwenye mahoteli ya kitalii na hivyo hawakuwa na picha ya uzuri wa maeneo fulani ya nchi yao. Hali hii bado ipo *indirectly* kwa sababu gharama, hata kwa wazawa ya kula na kulala kwenye hoteli za Ngorongoro, Serena, Mikuni na kadhalika, bado ni kubwa na wananchi walio wengi hawamudu. Matokeo yake wanawaachia Wazungu na wachache wenye uwezo. Tunaomba Serikali iweke *rates* nzuri kwa wazawa ili nao wanufaike na kutembelea na kuona mandhari ya hifadhi, wanyamapori na kupumzika kwenye mahoteli hayo na watoto wao.

Mheshimiwa Spika, utalii wa nje, ukweli ni kwamba mipango mizuri zaidi inahitajika ili kunufaika na maliasili zetu na utalii. Bado Wizara hii inatakiwa ibuni mikakati mipya ili kukabili wizi na ufisadi uliopo katika sekta hii.

Mheshimiwa Waziri tunakuamini sana unaweza. Watanzania watakupa nishani ukileta mabadiliko katika sekta hii kabla hujaenda Wizara nyingine. Maliasili na utalii ni kipaumbele cha kuinua uchumi wa Tanzania, hatupaswi kuwa maskini hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANNE KILANGO MALECELA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukupongeza unavyoliongeza Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanaoomba Mungu mchana na usiku wawe na mnyama hata mmoja tu, Sokwe, lakini hawakujaaliwa, hilo sisi Mungu katujaalia. *Katavi National Park*, ni ya tatu kwa ukubwa, ya kwanza ni Ruaha ya pili Serengeti, ina ukubwa wa kilomita za mraba 4471.

*Mheshimiwa Spika, Katavi National Park* ina wanyama wafuatao Simba wakubwa na wazuri mno, Tembo wakubwa mno, Chui, *Cheeter,* Viboko, Mamba kwa wingi mno, aina zaidi ya 400 ya ndege wazuri sana, Kongoni, Bofu, Mbwa mwitu, Nyati, Nyoka aina zote, Korongo, Nyani, Twiga Albino – weupe, Twiga wa kawaida na wanyama hawa ni wengi.

Mheshimiwa Spika, watalii wanategemewa watoke South Africa, Burundi, Rwanda, Zambia, Zimbabwe, Zaire na sehemu nyingi tu. Nimekwenda mimi mwenyewe kupumzika siku mbili Katavi, ndiyo *National Park* pekee niliyoweza kuona simba saba (7) waliopumzika pamoja wakifanya mkutano unaowahusu wao. *Katavi National Park* iliyopo Mpanda Mkoa wa Rukwa, haina miundombinu stahili inayowakaribisha watalii waweze kufika kwa urahisi. *Katavi National Park* imetelekezwa na Serikali ingepata mapato ya ndani kwa wingi kama ingeamua kuweka pesa za kutosha kwenye kuboresha miundombinu ya kuelekea Mpanda, hakuna mtu anayeweza kupata sasa bila ya kuweka pesa.

Niisihi Serikali ione umuhimu wa kuishughulikia *Katavi National Park* ili tuweze kupata mapato ya ndani kutoka katika hifadhi hiyo. Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha makusudi kwa ajili ya kuvuna fedha zaidi. Kipindi hiki sio rahisi lakini *budget* ya mwaka 2010/2011, Serikali itenge fedha maalum kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya *Katavi National Park.*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi na mimi nichangie juu ya hoja hii. Awali ya yote nataka kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watumishi wote kwa hotuba nzuri waliotuletea. Jambo la tatu nataka kuishukuru Wizara kwa kazi nzuri waliofanya kule Rufiji hususan katika kuhimiza na kuendesha ufugaji wa nyuki na umefanikiwa vizuri na naomba tu kwamba Wizara itusaidie kutupatia masoko.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Wizara imejitahidi sana kukarabati viwanja vya ndege vilivyoko katika hifadhi ya Selous, Kiwanja cha Mtemela, Kiwanja cha Nyakingupira kazi nzuri. Nataka niseme tu kwamba nimsifu Mheshimiwa Waziri kwa hatua za haraka alizochukua kwa sababu kule Rufiji tumeletewa *DC* huyu ni mchapakazi mno, nataka nimtamkie hapa Nakasi Majaliwa tangu aje yeye zimeshakamatwa roli za mbao nyingi, umeshakamatwa mkaa gunia 2,500 na wale Wamalira wanaoingia porini kwenda kukata mikaa sijui wanatoka Mbeya au sijui wanatoka wapi watu 25 wamepelekwa kortini na kupata adhabu moja kwa moja. Jambo hili lilitutia nguvu Warufiji wote kwamba maliasili sasa imepata mtu wa kuangalia vizuri na hafanyi kazi peke yake anakwenda na Kamati ya Ulinzi yote ya Wilaya. Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutuondolea Ofisi mmoja alikuwa ana *backer break* operesheni hii. Tulivyokuletea jina nasikia umeamua mara moja hayupo, hongera sana Mheshimiwa Waziri. Jambo lingine sasa turudi kuboresha hali ya *Selous, Selous* kama ujuavyo ina ukubwa wa *square kilometre* 54,600 ndio kubwa katika Afrika ni kubwa kuliko nchi nyingi hasa Switzerland nchi za Ulaya hali ya mle ndani inahitaji kazi kubwa hasa katika barabara zake. Katika jibu la msingi hapa wiki mbili zilizopita Mheshimiwa Waziri alituambia barabara ndani kule ni nzuri lakini naomba atupie macho zaidi ili kama changarawe iwe changarawe inayopitika mwaka mzima. Barabara zingine ni za masika tu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini ilishindwa kwenda *Stigler's Gorge* kwa sababu hiyo barabara ya kufika kule wakati wa masika inakuwa chepechepe haipitiki, kwa hiyo nilikuwa naomba hili alitilie mkazo kuhakikisha kwamba barabara za ndani ya Selous zinapitika. Hii inakuwa haieleweki sana wakati Selous inatengeneza shilingi bilioni 8 lakini hata kutengeneza barabara imebidi ikopwe shilingi milioni 300. Sasa isingekuwa angalau mkaweka shilingi bilioni moja mkatengeneza barabara ya Selous na shilingi bilioni 7 mkafutika kibindoni.

Kwa hiyo naomba hili lizingatiwe kwa sababu ndio litaboresha hiyo hifadhi ya Selous ambayo ni urithi wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunalo tatizo la kuifikia Selous. Kwa hiyo ningeomba sana TANAPA au Wizara itafute namna ya kuisaidia Halmashauri ya Wilaya kutengeneza barabara inayotoka Utete kwenda Kingupira takribani kilomita 75.

Kama ikiwezekana barabara hii ingechukuliwa na Wizara ili iweze kupitika hatuombi lami kule lakini tunaomba changarawe inayopitika mwaka mzima ili watu waweze kufika Kingupira kirahisi. *Ofcourse* utasema kuna kiwanja cha ndege pale, ndiyo, lakini kama unataka kupanua utalii wa ndani watu wengi watatumia sana barabara kuliko kuruka na ndege kwenda Kingupira.

Vile vile katika *Eastern Selous* upande wa Mloka barabara inayotoka Mkongo kwenda Mloka takriban kilomita 100 hivi kwa kweli ikiachiwa tu Wilaya au sasa hivi tuseme *Town Road* Mkoa tungependa nguvu ya Wizara nayo ionekane pale kwa sababu ile barabara ndiyo inahakikisha kabisa watu wanaotaka kwenda Selous kwa kupitia Mloka ndio barabara ya uhakika na takribani ukienda kule kila siku utakutana na watalii wako njiani wanakwenda Selous. Sasa utakuta tu kwamba mara nyingi wanakwama njiani sasa mtu ana nia ya kwenda kutazama pori hili hazina ya Kimataifa, urithi wa Kimataifa anakwenda kule badala yake ananasa njiani, nilikuwa nadhani tungeweza kabisa kusaidia barabara hii ikawa nzuri.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nizungumze juu ya kupanua nyanja za utalii katika nchi yetu. Kuna vivutio viwili tu nilitaka nivitamke nayo ni pale Mji wa Utete liko boma kubwa la Wajerumani na boma lile halikuja bure ilikuwa ni alama ya *resistance* wananchi wanakataa Wajerumani wasiingie Tanganyika, pale ndipo ilipiganwa vita, Mzee mmoja Majihumbi Mzuzuri koo zake marehemu Ditopile akapiga risasi kumpiga Kamanda mkubwa wa Jeshi la Ujerumani pale na akafa pale pale Utete na Wajerumani wakatamka hapa itajengwa hapa boma kubwa la aina yake kwa ajili ya kutawala Tanganyika. Boma likajengwa na hapo ndipo ninaposema lingekuwa jambo zuri likaongezwa boma hili katika utalii. Jambo lingine hapo hapo Utete Mungu ametujalia kuna chemchem ya majimoto, chemchem hii nilikwisha izungumza hapa lakini ina mambo.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Serikali ya Kijerumani, Wajerumani Tanganyika nzima walikuwa wanakwenda Rufiji kwenda kuoga maji ya moto kutoka chemchem ile na watu wakioga chemchem ile hawapati ugonjwa wa ngozi kabisa.

Nilikuwa naomba umeshafika wakati sasa kwamba Serikali yetu, Wizara hii ipanue utalii huu kwa nchi nzima, kila mahali na kupatangaza na taarifa hizi zipelekwe Ujerumani kwamba wazee wenu kule walikuwa wanaoga maji ambayo ukioga basi hupati tena ugonjwa wa ngozi.

Nilikuwa naomba sana wakati fulani Naibu Waziri aliyepita anajibu swali langu nilimkaribisha kule hata hivyo nazidi kuwakaribisha Mheshimiwa Waziri na Naibu wake njooni Utete muone majimoto haya muone mtasaidia namna gani ili kupanua utalii na kuongeza vivutio vya utalii hapa nchini na hasa Kusini katika wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba sana kuiambia nchi na Serikali yetu watanabahi upya kwamba Wizara hii ndiyo inayotunza maliasili ya nchi hii lakini ina watumishi wachache sana na Bajeti yake ni finyu na ukitaka kuifanyia haki Wizara hii *Manpower* yake lazima upanue mara mbili na Bajeti yake upanue mara mbili pia.

Bila ya hivyo tutaona tu na tutaendelea kulaumu kwamba utoroshaji wa maliasili unaongezeka na hii ni kwa sababu macho yanayotazama maliasili hii ni machache kuliko maliasili tuliyonayo au uwezo wa macho hayo. Huwezi kuwa na duka kubwa halafu ukawa na mlinzi mmoja mahali pa walinzi watano. Nilikuwa nadhani hili ni jambo muhimu sana kuzingatia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nakushukuru sana kwa kunipa nafasi naunga hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana Profesa Idris Mtulia. Naomba kujua hizo dakika.

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge sasa ni wakati ambapo tutasikia kutoka kwa Wizara husika. Tukianzia na Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye atafanya majumuisho kuhusu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa dakika zisizozidi 15 halafu atakuja Mheshimiwa Waziri ambaye yeye haki yake ni dakika 30 ingawa ametaka muda zaidi, lakini tutaangalia namna anavyokwenda.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa sote uzima hata tukaiona siku ya leo, lakini pia nishukuru kipekee kwangu binafsi kwa jinsi anavyonijalia na kunipa nguvu za kuweza kufanya kazi ambazo yeye mwenyewe inampendeza nizifanye.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niwashukuru sana wananchi wenzangu wa jimbo la Msalala mkoani Shinyanga ambao ni wapiga kura wangu kwa kweli wamekuwa ni watu wa faraja na *support* kubwa kwenye mazingira yangu ya kazi hapa Wizarani lakini pia kule jimboni. Wamekuwa wakinipa moyo sana na ushirikiano mkubwa. Niwahakikishie kwamba juhudi kubwa za kufanya Mapinduzi ya kasi ya maendeleo kwenye jimbo letu ambazo wengi wamejionea hata wale waliokuwa na mashaka awali sasa wanashuhudia kwamba jimbo letu la Msalala linapiga kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, niwaombe tu kwamba ushirikiano huu ambao tumeuonyesha kwa miaka takribani 3 iliyopita tuuendeleze kwani kwa hakika yako mengi ambayo tutafanikisha tukiendelea na umoja huo. Pia naomba nitoe shukrani za kipekee sana kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Waziri wangu, Katibu Mkuu Dr. Komba, Wakurugenzi na watumishi wengine katika Wizara ambao pia pamoja na ugumu na wingi wa majukumu katika Wizara lakini hakika wamekuwa wakinipa msaada mkubwa sana na kunipa moyo na kwa kiasi kikubwa ninafarijika na naona tunakwenda vizuri. Lakini kipekee nafikiri ni vizuri nikamshukuru sana msaidizi wangu wa karibu dereva wangu Bwana Oswald Mayunga. Kijana huyu amekuwa akifanya kazi kwa bidii na kwa kweli nampongeza sana. Baada ya shukrani hizo bila ya kusahau kuwashukuru pia familia yangu akiwepo mke wangu na watoto wangu ambao nao wamekuwa faraja yangu na watu wa kunipa moyo. Sasa naomba nipitie tu baadhi ya hoja ambazo zimesemwa na Waheshimiwa Wabunge hasa kwa kuzingatia suala la muda nitajitahidi kwenda haraka kwa sababu hoja ni nyingi sana lakini tutajitahidi kuhakikisha kwamba tutazizungumzia kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge wengi nitawataja akiwemo Mheshimiwa Dr. Chegeni, Mheshimiwa Killimbah, Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Yona Stanley Kevela, Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo, Mheshimiwa Ameir A. Ameir, Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa na Mheshimiwa Stephen Galinoma. Hawa pamoja na wengine kwa sababu nime-*capture* hii *list* haraka haraka mwishoni kuongezea majina yaliyojitokeza mwisho haijawezekana. Wote wamezungumzia sana suala la kuongeza wigo wa utalii, kuzungumzia kwamba utalii usilenge sana ukanda wa Kaskazini peke yake tujaribu kutangaza na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango wa utangazaji wa utalii na kubainisha maeneo Kitaifa upo. Kanda za Utalii tumezigawanya kwenye kanda mbalimbali na kila kanda ina mikakati yake. Kwa upande wa Kanda ya Ziwa kuna Shirika linaitwa la Uholanzi linatusaidia sana katika kubainisha na kuratibu ubainishaji wa utalii asilia. Tayari wameshaanza kufanya mafunzo kwa watu wa maeneo ya Bujora na Butiama katika mikoa ya Mwanza na Mara. Lakini pia kuna mafunzo yanaendelea kwa mkoa wa Kagera. Mwaka 2004 Wizara yangu ilifanya zoezi la kubaini vivutio vya utalii katika mikoa ya Kagera, Mara na Mwanza zoezi lilishakamilika, orodha ya vivutio tulishavibainisha sasa hivi tunaendelea na hatua ya pili ambayo kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa kwenye maeneo hayo ya kuvitangaza vivutio hivyo. Kulikuwa pia na suala la kutangaza mji wa Mikindani kule Mtwara na fukwe zake. Eneo hili pia liko kwenye ukanda wa utalii wa Kusini ambao utangazaji wake unahusisha pia maeneo ya Lindi, Kilwa ambayo tayari nayo mpango wake umeshakamilika kinachobaki sasa ni hatua zile za utangazaji. Kipekee kulizungumziwa kutangaza maeneo ya mambo ya kale. Mji wa Ujiji ameusema rafiki yangu kijana mwenzangu Mheshimiwa Zitto, Mji wa Tabora ameusema Mheshimiwa Mchemba, Mji wa Songea na maeneo mengine kadha wa kadha.

Mheshimiwa Spika, haya maeneo kila moja limewekewa mkakati wake. Kwa upande wa Tabora na Vijiji njia ya watumwa kuanzia Bagamoyo hadi Kigoma kila eneo ambalo kulikuwa na kituo kumeshabainishwa na kuna mpango kabambe wa kufufua njia hiyo ambayo inahusisha mji wa Tabora na Mji wa Kigoma. Upande wa Mji wa Songea kwenyewe tumeshabainisha na tunakusudia kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge kutambua mji huu kama mji wa kihistoria ambayo ni taratibu za kisheria.

Baada ya hatua hiyo kukamilika hatua ya pili sasa ni kuanza kutangaza maeneo hayo ambayo yatakuwa tayari yameshabainishwa.

Mheshimiwa Spika, kulijitokeza pia hoja na kutangaza mikoa ya miongoni mwa wengine Iringa na Mbeya ambazo hasa lilitajwa na Mheshimiwa Galinoma, Mheshimiwa Kevela. Mkoa wa Iringa una vivutio vingi na vingi vimeshaanza kutangazwa na *TTB* pamoja na *TANAPA. Ruaha National Park* pamoja na Kitulo kipekee vinatangazwa. Tatizo ambalo limekuwepo kwa upande wa *Ruaha National Park* ni suala la miundombinu. *TANAPA* wamefanya kazi kubwa sana katika miaka miwili iliyopita mwaka 2007/2008 na 2008/2009 wametumia jumla ya shilingi 1,800,000,000 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya *Ruaha National Park.* Katika kufanya hivyo wamejenga madaraja wanatengeneza barabara, wanatengeneza hosteli kwa ajili ya wageni wanaotembelea eneo hilo, lakini pia wametengeneza *information centre* ya kisasa kabisa kwa ajili ya kupokelea wageni na kutoa taarifa za utalii.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya utekelezaji wa Sheria ya Utalii iliyotolewa na Mheshimiwa Herbert Mntangi. Sheria hii ya Utalii ilikwishakamilika, kanuni zake zimekamilika, kwa hiyo hatua sasa hivi inayofuata ni ya kutoa elimu kwa umma na kuanza kutekeleza kanuni ambazo tayari zimeshakamilika. Kulikuwa na hoja ya uhamasishaji wananchi uendelezaji wa utalii wa ndani. Hii imesemwa na Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Zakia Meghji, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Dr. Wanyancha na Mheshimiwa Selelii.

Mheshimiwa Spika, tuna mikakati mingi tunayoifanya kutangaza utalii. Kwanza tunaendelea kushiriki katika maonyesho mbalimbali ya biashara hapa nchini. Kuna maonyesho ya utalii yanaitwa *"Karibu Fair"* kule Arusha, tumekuwa tukishiriki na kuonyesha na kutangaza vivutio vyetu Maonyesho ya Saba Saba, Nane Nane na kwa kweli kwa wale ambao walitembelea banda letu hata mwaka huu wameona jinsi ambavyo tunajitahidi kutangaza vivutio vyetu. Lakini pia katika kutangaza utalii wa ndani tumeendelea kudhamini mashindano mbalimbali ambayo pia ni njia mojawapo ya kutangaza utalii, kuna mashindano ya Mbio za Kilimanjaro, kuna Mashindano ya *Bongo Star Search* ya muziki lakini pia kuna mashindano ya aina mbalimbali ambayo wanapokuwa wakishindana tumekuwa tukidhamini na hivyo kutangaza utalii wetu. *(Makofi)*

Kuna pia vichapisho mbalimbali vimechapishwa na kusambazwa sehemu mbalimbali za nchi lakini pia tunaendelea kushirikiana sekta binafsi ili kuwashawishi watengeneze *packages* ambazo zitarahisishia wageni wetu au wanaotembelea vivutio vyetu waweze kuvitembelea.

Kuna vipindi vya redio na televisheni vinaendelea ambavyo vimekuwa vikisaidia kutangaza utalii na vivutio vyetu lakini pia kuna misafara ya Waandishi wa Habari ambayo tumekuwa tukiifadhili kila mwaka kutembelea vivutio vyetu na hivyo kutoa habari ya vivutio vyetu kwenye vyombo vyao vya habari. Shirika la Hifadhi ya Taifa *(TANAPA)* wamekuwa wakijitahidi sana kuboresha hosteli kwenye maeneo ya mbuga zao ili wageni waweze kupata *accommodation* ya bei nafuu. Kuna Basi pia ambalo linamilikiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ambalo linawasafirisha watalii kutoka mji wa Arusha kwenda Ngorongoro kila *weekend* na linafanya kazi vizuri na nafikiri mpango huu pia unaboreshwa ambalo limekuwa likifanya kazi hizo toka mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Killimbah aliyotaka Mheshimiwa Waziri azungumzie jinsi Serikali inavyojipanga kukabiliana na ushindani wa utalii katika ukanda wa Afrika Mashariki. Mkakati wetu kwanza katika kutangaza kuna mazungumzo yanayoendelea ya

kuona namna gani tunaweza tukatangaza vivutio vyetu kwa pamoja. Tunategemea njia hii ya kutangaza kwa pamoja *East Africa Destination* itatusaidia kuweza kutangaza vivutio vyetu. Lakini wageni wanapofika mpango wetu ni kuhakikisha kwamba vivutio vyetu wanavitembelea kwa malipo ambayo hayawekwi katika *package* ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kama *Destination* na hivyo tunafikiri kwamba mpango huu utaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya Dr. Mwita Haji Mwita anazungumzia bandari ya Zanzibar ni ya kuvutia na hivyo inahitaji kutangazwa, ni wazo zuri tumelichukua tunalifanyia kazi. Kuna hoja ya Mheshimiwa Mariam Mfaki pamoja na Mheshimiwa Estherina Kilasi wamezungumzia tupanue vyuo vyetu ili kuweza kutoa mafunzo kwa wahifadhi wengi zaidi. Mpango wa miaka mitano ijayo ni kupanua Chuo cha Wanyamapori Mweka kinachodahili kwa sasa wanafunzi 418 kufikia 700. Lakini pia Chuo cha Pasiansi chenyewe kinapanuliwa kwa sasa hivi kinadahili wanafunzi 100 na tunategemea kitafikia angalau 150 mwisho wa mwaka ujao.

Kwa hiyo, hili tumelichukua na pia tulipendekeza na tunaendelea na mazungumzo ya kutoa mafunzo ya haraka kwa wahitimu wa JKT ili waweze pia kuajiriwa katika mtindo wa *Fast Track*. Mazungumzo yanaendelea nafikiri hilo nalo litatusaidia kuweza kupata jibu la uhaba wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi ameomba tujenge kituo cha *TANAPA* kwenye mji wa Musoma. Ni wazo zuri lakini matatizo ya kifedha kwa sasa kutokana na mtikisiko wa uchumi hayatupi nafasi ya kulifanya jambo hilo lakini tutalizingatia katika Bajeti zetu hasa kuanzia mwaka ujao wa fedha kutegemea na hali ya uchumi. Mheshimiwa Aloyce Kimaro amezungumzia kufungua njia mpya hili tulizungumza naye vizuri sana jana tukaelewana kwamba jambo hili ni zuri lakini linahitaji utafiti na utafiti unaendelea baada ya Bajeti kupitishwa ambayo ni maombi yetu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu yeye amezungumzia suala la Mabwana Nyama kuwa ni wachache na hawana usafiri. Ni tatizo lakini tunaangalia namna ya kuweza kusaidia tatizo la usafiri kwenye eneo hilo. Hili tumelichukua na tutalifanyia kazi. Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa amezungumzia suala la kupandisha ada za kuingia kwenye pori la akiba la Ugalla pamoja na wananchi kubambikiziwa kesi.

Suala la kiingilio kwenye hifadhi kwamba ni kikubwa ni kama ambacho tumekipokea ingawa kwenye maeneo mengine hatujapata malalamiko haya tunafanya utafiti kujua ni nini hasa tatizo la eneo hili kwa sababu viingilio katika hifadhi zote ni sawa lakini hapa kunaonekana kuna tatizo.

Tatizo la kubambikiziwa kesi hatuna ushahidi nalo sana kwa sababu mara nyingi mambo haya yanakuwa ni ya hisia zaidi. Kwa hivyo tunafikiri ni vizuri tukatoa elimu kwa wananchi ili waweze kuelewa na kujua mipaka yetu lakini pia kwa askari wetu ili kama kuna watu ambao si waadilifu wanaofanya mambo hayo waweze kuacha na ikibainika basi hatua kali zitakuwa zikichukuliwa.

Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni amezungumzia wafugaji wanaoingia kwenye hifadhi hutozwa faini kubwa, hili ni suala la kisheria na kanuni zake ambazo zimeweka faini hizo. Nafikiri ni vizuri tu tukiwaelimisha wasiingie kwenye hifadhi badala ya kuzungumzia faini zipunguzwe ili waingie kwa wingi kitu ambacho kitakuwa kina-*contradict* misingi ya uhifadhi.

Kaka yangu Mheshimiwa Msindai amezungumzia suala la askari wanyamapori wahamishiwe Serikali Kuu. Ni wazo ambalo sisi tunafikiri lina-*contradict* ile dhana ya *D by D* tunafikiri pengine tutafute namna ya kutatua matatizo ya utumishi wao badala ya kuzungumzia kuwahamishia kwenye Mamlaka ya Ajira.

Kwa hiyo, tunamshauri kwamba pengine atupe nafasi tuendelee kufanya kazi na wenzetu wa TAMISEMI kuona namna gani tunaweza tukaboresha au kudhibiti upungufu wa kimaadili katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, amesema pia Idara ya Wanyamapori iwe na Mamlaka. Sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009 imependekeza hivyo na baada ya Kanuni zake kukamilika basi mara moja jambo hilo litaanza kutekelezwa. Mheshimiwa Kayombo pia amependekeza kuanzisha WMA kwenye eneo la akiba la Liparamba na Litumbandyosi. Ni wazo zuri lakini utaratibu ni kwamba wananchi lazima washirikishwe na tutatumia wataalamu wetu wa eneo hili kuweza kuwahamasisha wananchi pamoja na yeye Mheshimiwa Mbunge ili waweze kuridhia kutumia ardhi yao kwa ajili ya uhifadhi badala ya matumizi mengine. Kaka yangu Luhahula sijui kama yupo, lakini alizungumzia kuchimbwa bwawa la Nsango kule kwetu Bukombe. Wazo hili ni zuri na tutalizingatia.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri sasa nitamwita mtoa hoja ambaye ndiye Waziri wa Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo kuhusu hoja walizotoa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali walipokuwa wakichangia hotuba ya Wizara yangu ya Bajeti mwaka 2009/2010. Kwanza naomba kutoa shukrani kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ikiongozwa na Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kwa kushirikiana na Wizara yangu katika kuandaa Bajeti ya mwaka 2009/2010.

Wizara ilifarijika sana kwa maelezo na maelekezo mbalimbali yaliyotolewa na Kamati hii kwa lengo la kuboresha taarifa ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuongea na waliochangia kwa maandishi kwa michango yao mizuri ambayo kwa kweli yote ina faida na ni mambo ambayo ya muhimu katika Wizara yangu. Kabla ya kuanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge naomba sasa kuwatambua jumla ya Waheshimiwa Wabunge 24 waliochangia hotuba ya Bajeti yangu kwa kuzungumza hapa Bungeni kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Msemaji wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi na Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Anne Killango Malecela, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Halima Mamuya na Mheshimiwa Kaika Telele.

Waheshimiwa Wabunge wengine ni Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo, Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mchemba, Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto na Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, naomba pia kuwatambua Waheshimiwa Wabunge 72 waliochangia hotuba yangu kwa maandishi kama ifuatavyo. Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu, Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mheshimiwa Ramadhani Athumani Maneno, Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya, Mheshimiwa Steven Galinoma na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengine ni Mheshimiwa Dr. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Dr. Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Juma Killimbah.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Archt. Fuya Kimbita, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Prof. Banyikwa, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa James Wanyacha, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Anne Malecela, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Festus Limbu na Mheshimiwa Benson Mpesya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Teddy Kasela-Bantu, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Zakia Meghji, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Lucas Selelli, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Kanali Feteh Saad, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Steven Wasira, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir na Mheshimiwa Dr. James Msekela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru kipekee hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambaye imeunga mkono jitihada na dhamira za kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, tumefarijika sana na mapendekezo yaliyotolewa kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, ni nyingi na kutokana na ufinyu wa muda, sitaweza kuzijibu zote ila napenda kuliahidi Bunge lako Tukufu, nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kujibu hoja nyingi niwezavyo na zile ambazo sitazijibu tutaziandaa na kutoa katika maandishi na kumpelekea kila Mbunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kutoa maelezo ya jumla ya hoja kwa hoja zile ambazo zilichangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na baadhi ya hoja zingine ambazo nitaanza kuziongea zilizochangiwa kwa maandishi na baadaye nitamalizia na zingine.

Mheshimiwa Spika, suala la bei kubwa ya mbao. Ni kweli bei ya mbao imekuwa kubwa kuliko nchi jirani na kuwa wingi wa kodi umechangia kwa kiasi kikubwa bei hizo kuwa kubwa. Kodi hizo ni kodi za *VAT, LMDA, royalty, Cess* ya Halmashauri na malipo mbalimbali ya vibali. Wizara imekwishaliona tatizo hilo na imechukua hatua zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, tumewashirikisha Hazina, hoja ya *VAT* kutotozwa mara mbili na Hazina wamekubali, wanashughulikia. Wizara imeunda Kikundi Kazi ambacho kinalifanyia kazi suala hili pamoja na kutembelea Malawi ili kuona sababu za tofauti kubwa ya bei ya mbao kati ya Tanzania na Malawi. Matokeo ya kazi ya Kikundi Kazi hicho, yataiwezesha Serikali kupanga upya bei za misitu na mbao.

Mheshimiwa Spika, Waziri Kivuli Mheshimiwa Magdalena Sakaya, mdogo wangu, yeye alikuwa na hoja nyingi alizotoa katika kuchangia kwa upande wa Kambi ya Upinzani, kati ya hoja hizo, moja alisema uwepo wa rasilimali za misitu hazijatumika ipasavyo ili kuiongezea Serikali kipato. Kwa sasa Serikali inafanya tathmini ya misitu kwa nchi nzima na matokeo yake yataweza kuonesha aina za miti katika misitu ikiwa ni pamoja na miti au mimea itakayotumika kwa dawa za asili.

Mheshimiwa Spika, pia aliongelea kwamba utafiti ufanyike nchini ili kubaini wingi wa miti ya aina ya mng'ong'o ambao hutumika kutengeneza kinywaji chenye umaarufu mkubwa duniani, kinywaji cha Amarura. Tunashukuru kwamba pia tathmini ya misitu hiyo itabainisha suala hilo na yenyewe itakuwemo katika kufanyiwa utafiti.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kutoka kwa Mheshimiwa Ndesamburo ambapo yeye alisema kwamba viwanda vya mazao ya misitu vinabinafsishwa na kwamba kilichopo Handeni Tanga hakifanyi kazi. Natoa maelezo kwamba kuna Kikundi Kazi kinachoshughulikia suala hili, hivyo Idara inatarajia kupata taarifa na itaifanyia kazi ipasavyo kulingana na ushauri wa Kikundi Kazi hicho kuhusu msitu huo wa Handeni.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji wa Kiwanda cha *Sao Hill* na *Saw Mill,* Serikali haijapata pato lolote kutoka kwenye kiwanda hicho tangu kibinafsishwe na mbaya zaidi Mwekezaji anaonekana ana lengo tofauti na lile lililomo kwenye mkataba. Napenda kusema kwamba tutafuatilia suala hilo na kubaini mwenendo na ulipaji kodi wa kiwanda cha mwekezaji huyu.

Mheshimiwa Spika, pia ufafanuzi wa *TANESCO* kununua nguzo za umeme kutoka nje ya nchi kwa gharama kubwa wakati miti ya nguzo ya umeme ipo kwa wingi hapa nchini. Suala hili pia tutalifuatilia na maelezo tutayatoa kwa sababu kwa kweli sasa hivi nguzo hizi ziko nchini kwetu na pia hata baadhi ya wananchi wanasafirisha kutoka hapa nchini kwetu na kwenda nchi za nje. Tutalifuatilia suala hili *TANESCO* ili tujue ni nini kinachofanya wenyewe waagize mbao hizo nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu kiasi cha fedha ambacho Serikali imepoteza kwa kipindi chote tangu makampuni mawili ya mazao ya misitu yabainishwe, tutafuatilia. Pia tutazingatia ni kiasi gani kimepotezwa kutokana na kuagiza nguzo za umeme nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala kutoka kwa Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambaye anasema kwamba ubinafsishaji wa Shamba la Mitiki la Lunguza kwa Kampuni ya Kilombero haukufanyika kwa maslahi ya taifa. Kiasi cha shilingi bilioni saba, ambacho anasema kwamba shamba hilo liliuzwa kwa bei hiyo ndogo ambapo msitu ule una thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 38. Napenda kutoa maelezo kwamba hiyo siyo kweli maana Serikali haijawahi kubinafsisha shamba lolote la miti yakiwemo mashamba ya Misaji.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Misitu na Nyuki inaendelea na utaratibu wake wa kuuza miti iliyokomaa. Miti ya Misaji kutoka shamba la Luhunguza imekuwa ikiuzwa kwa njia ya zabuni au mnada. Kati ya mwaka 2005 – 2008, jumla ya mita za ujazo 63,689 zimeuzwa na kuingiza jumla ya shilingi 9,071,841,000/= na sehemu ya shamba dogo karibu asilimia kumi tu ndiyo ambayo iliyovunwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo Mheshimiwa Sakaya anauliza ni kwamba hadi lini nchi yetu itaendelea kuwavumilia watendaji wasiokuwa na uzalendo na uaminifu pale wanapouza maliasili za Taifa kwa kuweka mbele maslahi yao. Je, hatua gani watachukuliwa? Wizara hutumia Kanuni na Sheria kushughulikia watumishi ambao hawatimizi wajibu wao ipasavyo na kuna baadhi ya watumishi ambao tumewasimamisha wengine wameshafukuzwa na baadhi kesi zao ziko Mahakamani. Kwa hiyo tunafuata Sheria na Kanuni na tuki-*prove* kwamba mtu amekosa anashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika suala lingine ambalo Mheshimiwa Sakaya aliliongelea lilikuwa linahusu mambo ya uharibifu wa misitu unaochangiwa na watendaji wa Serikali wasiowaadilifu, hilo nimesema kwamba ni suala ambalo tutalifanyia kazi na kama nilivyosema tutafuata Sheria na Kanuni kushughulikia suala hilo. Mheshimiwa Spika, baada ya hilo niendelee kuwajibu wengine na Mheshimiwa Sakaya kama kuna lolote nitakuwa nimelisahau basi nimeahidi tutayajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuzungumzia suala la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ambaye yeye hoja yake ilikuwa inasema kwamba ulinzi wa nyara za Serikali ni hafifu. Hivi karibuni shehena kubwa ya meno ya tembo imekamatwa huko Vietnam na inadaiwa meno hayo yamesafirishwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam. Wizi na utoroshaji wa rasilimali za maliasili za nchi, unaathiri maendeleo ya Taifa na wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kwa kuwa mstari wa mbele na kuwa na uchungu na mali ya nchi na kutumia jitihada zake binafsi

kutafuta taarifa ambazo zinaweza zikasaidia mambo mbalimbali ya ubadhirifu au mambo ambayo yanaweza kuwa na uhusiano na ufisadi. Namshukuru kwa hilo na namwomba kwamba kila mara akipata chochote tuwasiliane, sisi tutakuwa tayari kufanya naye kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa nataka kusema kwamba mambo haya aliyoyaongea Mheshimiwa Anne Malecela, ni mambo ambayo kwa kweli yanatokea na sisi tuna taarifa kamili na Wizara imekuwa bega kwa bega ikishughulikia suala hilo na napenda nianze kuongea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwezi wa Machi na Mei, 2009, Idara ya Wanyamapori ilipokea taarifa kutoka *Interpol* Dar es Salaam kuwa Kontena mbili zikiwa na meno ya tembo zilisafirishwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam, yalikamatwa Vietnam na Philippines. Aidha, taarifa hizo ziliwasilishwa pia *Lusaka Agreement Task Force* ambayo sisi tunafanya nayo kazi katika kudhibiti ujangili.

Mheshimiwa Spika, Idara kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, kitengo cha *Interpol* Dar es Salaam, *Lusaka Agreement Task Force* na *World Custom Organization,* waliendesha upelelezi na watuhumiwa tisa wamekamatwa na kuhojiwa. Kati yao, wanne wanatarajiwa kufikishwa Mahakamani. Maelezo ya makontena yaliyokamatwa kama ifuatavyo:-

Moja, tarehe 1/3/2009, Maafisa wa Forodha wa Bandari ya Manila Kusini, walikamata tani tatu za meno ya tembo yakiwa yamefichwa kwenye maboxi 18 ndani ya makontena na kontena moja namba ESMU na yalisafirishwa tarehe 25 Oktoba, 2008 kwa Meli inayoitwa Delmas Nakala kupitia Bandari ya Dar es Salaam Tanzania yakiwa yamesajiliwa kama mzigo wa vifurushi 80 vya *plastic sheet.*

Pili, tarehe 4/3/2009, Maafisa Forodha wa Bandari ya Manila Kusini, Philippines walikamata tena meno ya tembo tani 1483 yakiwa yamefichwa kwenye makasha ndani ya kontena namba TSLU 621954. Meno hayo yalisafirishwa tarehe 25/10/2008 kupitia Bandari ya Dar es Salaam mzigo ukiwa umesajiliwa kama *recycle of plastic waste*. Tarehe 5/3/2009, Maafisa Forodha wa Dinhivu, Nguyenthi, Thanmbi, Haifon ambako ni Vietnam walikamata vipande 1224 vya meno ya tembo vyenye uzito wa tani 6,232 yakiwa yamefichwa kwenye takataka za *plastic* ndani ya maboxi 114 kwenye kontena namba ESMU 162184. Meno hayo yalisafirishwa tarehe 28 Desemba, 2008 kwa meli ya Delmas Nakala kupitia Bandari ya Dar es Salaam Tanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nadhani usahihishe. Hizo tani 1000 na tani 6000 haziwezi kukaa kwenye kontena, ni kilo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, sahamahi ni kilo sio tani.

Aidha, kufuatilia jitihada zilizofanyika, watuhumiwa wanne wamekamatwa na kuhojiwa, uchunguzi zaidi bado unaendelea. Wizara imetenga jumla ya shilingi milioni 25 kwa ajili ya kuiwezesha Timu ya Upelelezi toka Idara ya Wanyamapori, Polisi, *Interpol* wa Dar es Salaam na *Lusaka Task Force* kwenda Vietnam kufuatilia na kupata vielelezo zaidi vitakavyosaidia katika kuendesha mashtaka dhidi ya watuhumiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa vile upelelezi huu unaendeshwa na *Interpol* ikishirikiana na Kikosi dhidi ya Ujangili cha Idara ya Wanyamapori na *Lusaka Agreement* pamoja na *World Custom Organization,* napenda kumsihi Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwamba avute subira kwa kuwa timu ya wataalam inayofuatilia suala hili ni timu ya kitaalam ambayo ina ujuzi mkubwa na haijakamilisha kazi yake na kutoa taarifa, ili tujue ripoti yao italeta nini ili tusiweze kuuharibu upelelezi wao.

Mheshimiwa Spika, licha ya matukio ya karibuni kama inavyonesha hapo juu, kumbukumbu zetu zinabainisha kwamba mnamo tarehe 4/7/2006, Maafisa Forodha wa Bandari ya Quinsu Taiwan Kusini, walikamata meno ya tembo tani 5.27 yakiwa yamefichwa kwenye maboxi 18, yalikuwa ndani ya makontena mawili yenye namba PNU 073898 na namba zake zingine MAU 791500453. Makontena hayo yalisafirishwa tarehe 14 April, 2006 kwa meli ya Munhista kupitia

Bandari ya Tanga, Tanzania yakiwa yamesajiliwa kubeba marobota 60 ya Mkonge kwenda nchini Ufilipino.

Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa hizo, Wizara kwa kushirikiana na *Interpol*, iliendesha upelelezi ikiwa ni pamoja na kwenda Taiwan kufanya uhakiki na matokeo ya upelelezi ni kwamba jumla ya watuhumiwa kumi walikamatwa na kuhojiwa. Kati ya hawa, watuhumiwa sita wamefikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Tanga na kufunguliwa kesi Na.2 ya mwaka 2006. Kesi hii bado inaendelea kusikilizwa na mashahidi sita wa upande wa mashitaka wametoa ushahidi wao. Mashahidi watano bado hawajatoa ushahidi wao pamoja na kuwasilishwa kwa ushahidi wa picha zilizopatikana katika uchunguzi uliofanyika huko Taiwan.

Mheshimiwa Spika, biashara na usafirishaji haramu wa meno ya tembo yanayokamatwa nje ya nchi, unatokana na Wizara kutohusishwa kikamilifu katika mchakato wa kukagua vifurushi vinavyopakiwa katika makontena. Kukagua wakati wa kufunga na nyaraka kabla ya kusafirishwa kwenda nchi za nje kupitia bandari zetu. Kwa kuwa Wazira yangu haihusishwi na taratibu zote hizo, inakuwa si rahisi kujua kwenye makontena hayo yamepakiwa nini isipokuwa kwa kutumia *Intelligence* yetu na pia kutumia Lusaka *Agreement* ndipo ambapo huwa tunapata habari za kuweza kuingilia kati tukishafahamishwa. Utaratibu wa sasa unaotumika, unaruhusu baadhi ya Maafisa wa Forodha na usalama kukagua peke yao, kuhakiki, kusimamia upakiaji na usafirishaji wa mizigo iendayo nje ya nchi yakiwemo mazao ya maliasili. Ni dhahiri kwamba ili kudhibiti hali hii, unahitajika ushirikiano mkubwa kati ya ofisi yangu na vyombo vinavyosimamia usafirishaji wa mizigo bandarini.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa usafirishaji harama wa nyara nje ya nchi, ni changamoto kwa Wizara kwa kuwa Tanzania ni lango la kupitisha bidhaa mbalimbali kutoka nchi jirani kama Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo, Uganda, Burundi, Rwanda, Zambia na Malawi. Aidha, biashara haramu ya meno ya tembo inaendelea kwa kificho na ujanja mkubwa katika nchi hizo soko kubwa likiwa ni nchi za Asia.

Mheshimiwa Spika, licha ya juhudi hizi za kupambana na uhalifu huo wa kimataifa na pamoja na ukweli kwamba idadi ya Askari wa Wanyamapori, ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji. Kwa ufanisi mkubwa, Wizara imeendelea kupambana na wimbi la ujangili na biashara haramu ya nyara nchini kwa kuendesha doria na ukaguzi wa kudumu katika viwanja vya ndege na kuwashtukiza katika bandari, vizuizi barabarani na vituo mipakani. Hata hivyo, kama ilivyo katika uhalifu mwingine wanaojihusisha na biashara haramu wa nyara ni mtandao wa wenye fedha nyingi. Wana mbinu nyingi za kukwepa vyombo vya dola na pia kuwarubuni baadhi ya watumishi wa umma wasio waaminifu kufanikisha kazi hiyo haramu. Katika tukio hili, Maafisa Bandari ni miongoni mwa watuhumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na ujanja wa kutorosha nyara, doria za kipamoja kati ya Askari ya Wanyamapori wa Kikosi dhidi ya Uujangili Kanda ya Mashariki, Dar es Salaam na Jeshi la Polisi zilizoendeshwa kati ya tarehe 30 Aprili mwaka huu hadi tarehe 6 Mei mwaka huu, zimekuwa na matokeo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kumekamatwa meno ya tembo yenye uzito wa kilo 357 sawa na thamani ya shilingi milioni 26,419,000. Silaha zimekamatwa *riffle* ya pointi 375 na magobole mawili pamoja na risasi zake. Watuhumiwa wamefunguliwa mashtaka katika vituo mbalimbali vya Polisi na Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kukamatwa kwa meno ya tembo vipande 45 venye uzito wa kilo 81.6 katika maeneo ya Changombe Maduka Mawili, watuhumiwa watatu wamefikishwa katika Kituo cha Polisi Chang'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kukamatwa meno ya tembo vipande 22 venye uzito wa kilo 53.5 katika kizuizi cha Nangurukuru, watuhumiwa wawili wamefikishwa katika Kituo cha Polisi cha Kilwa Masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kukamatwa jino la tembo moja zima na vipande vinne vyenye kilo18. Mtuhumiwa ndugu Donata Kasolo, amefikishwa Kituo cha Polisi Uwanja wa Ndege na kesi kufunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na nyara hizi, nyara nyingi nyingine zimekamatwa ikiwa ni pamoja na vinyago, taswira za binadamu 55, mamba 14, faru 14, tembo mmoja, ndege aina mbalimbali watano, simba watano, kiboko wawili, pete 28, vibanio vya nywele sits, vidani 73, *hanger* moja, *stand* za meza 92, mapambo, pembe manne na duara tatu, bangili 28, kucha za simba 60 na meno 11, bangili 82 na meno nane na maganda ya kasa. Wanyama hai kama digidigi, mbuzi mawe, swala tomi, ngozi ya digidigi, swala pala na meno ya ngiri vyote hivyo vimekamatwa katika kipindi hicho nilichoeleza kwa Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi ni baadhi tu ya juhudi za kupambana na ujangili unaotokana na ushirikiano wa wahalifu katika jiji la Dar es Salaam na Pwani. Aidha kulingana na taarifa zilizopo, ninapenda kusisitiza kwamba pamoja na ujangili mwingine unaoweza ukafanyika nchini kwetu, ni dhahiri pia kwamba Bandari yetu ndio lango la kupitisha bidhaa kutoka nchi za jirani, ikiwemo nyara zitokanazo na wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tena niseme kwamba, naomba Waheshimiwa Wabunge wote wasisite wakijua kuna taarifa ambayo inaweza ikasaidia kuwakamata wahalifu na hawa wezi wa mali zetu za Taifa, tunaomba ushirikiano wao tuweze kufanya kazi hizo, kama Mheshimiwa Anne Kilango Malecela alivyojitolea na kuongea ukweli ambao alikuwa anaufahamu na ni kweli kwamba mambo hayo yametokea na sisi tulikuwa mstari wa mbele tumehakikisha kwamba mambo yote yanakwenda sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nirudie tena kumwambia Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwamba kufuatana na taarifa hii na jinsi nilivyoonyesha juhudi ya Wizara, jinsi tunavyojitahidi kuyakabili, namsihi na nakuomba kwamba asitishe kutoa tamko la kutaka kuunda Tume kwa sababu napenda nimhakikishie kwamba kazi hii tunaifanya, tunaimudu na vyombo vya mataifa tunashirikiana navyo kwa karibu na sasa hivi hata Mikoani pia kuna mambo mengi ambayo tunayakamata na mara nyingi huwa nawashirikisha Waandishi wa Habari kuyafahamu, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya kumbukumbu, napenda pia kuwafahamisha Wabunge pamoja na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kuhusu hiyo meli ya Vietnam iliyokamatwa na mizigo, niwataje waliokamatwa ni akina nani na uchunguzi ambao unaendelea. Waliokamatwa kwa majina ni Eldaus Colnel Tesha pamoja na mwenzie Gabriel Chambo Barua. Hawa wana Kampuni ya *Team Freight* ambayo inashughulika na upakiaji wa mizigo Bandarini. Baada ya kupekuliwa katika kompyuta zao na kila mahala kwa kutumia ujanja tuliouweza, ndiyo hawa waliweza kupatikana na *invoice* zao zikaonyesha kwamba wanahusika na utoroshaji huo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna bwana mwingine anaitwa Shabani Yabulula, huyu ni Mkurugenzi wa Kigoma *Entreprises* ambaye ndiye alikuwa wakala wa kupakia bidhaa zilizosadikiwa kuwa ni plastiki chakavu kwenye kampuni ya *Team Freight* na ndiye aliyekabidhi *Seal* kutoka kwa wakali wa meli iliyosafirisha mzigo ijulikanayo kama Delmas Nakala.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna bwana anaitwa Eric Lelo Morant, huyu ni Afisa wa *Customs*, ambaye tarehe 23 Disemba 2008, alisimamia na kufanya ukaguzi wakati mzigo wa *recycle waste plastic* unapakiwa na kufanyiwa *stuffing* hiyo ya kiharamu. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba hao wote wapo wamekamatwa.

Mheshimiwa Spika, meli ile ya pili ya Ufilipino wamekamatwa Issa Asanali Lweno, Gabriel Chambo tena, amekamatwa na wenzie wengine. Pia napenda kusema kwamba hawa wote watafikishwa Mahakamani uchunguzi utakapokamilika na kama nyuma yao kuna wengine wowote, hatutaogopa watakamatwa, hata akiwa ni mtu wa aina gani tutamkamata na atafikishwa Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua muda unanikimbia, sasa naomba kwa haraka tu niweze kuendelea na hoja zingine. Hoja nyingine ilikuwa inatoka Kambi ya Upinzani ambayo inasema matumizi mabaya ya fedha ya Amana ya jumla ya shilingi 7, 360,000,000 ambazo Mkaguzi wa Hesabu amegundua kwamba zimetumika vibaya. Napenda kusema kwamba, tumelifuatilia na nimeshirikiana na *TANAPA* kujua nini kilichotokea. Lakini ukweli ni kwamba ripoti ya kwanza ilipofanywa ilikuwa bado Wakaguzi wa Nje hawajakaa kushirikiana na *TANAPA* kujua na kuuliza maswali waweze kufahamu yalivyo. Lakini baada ya hapo, ilikwenda kwa *CAG* mwenyewe na yeye akaitangaza. Lakini baada ya mawasiliano, alipohojiwa kwamba *TANAPA* haijashirikishwa, aliruhusu kikao kifanyike na kikao kikafanyika ili kutoa majibu, baada ya hayo majibu kutolewa yafuatayo yalibainika:-

Mheshimiwa Spika, hoja iliyotolewa na Mkaguzi inahusu jumla ya Dola za Marekani 4,108, 811 ambazo ni sawa na shilingi 4,930,561,860/= na si kama ilivyoandikwa kwamba ni shilingi 7,360,000,000. Kwa hiyo, ilifanyiwa ufafanuzi na ikaonekana hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, mchanganuo huo wa Amana, ulionyesha kwamba pesa hizo zilikuwa zimewekwa kwenye Akaunti ya Amana, moja ilikuwa na thamani ya US Dola 2,064,146 ambayo ilikuwa kwenye tarehe 30 Juni, 2008. Amana hiyo, iliiva tarehe 1 Julai 2008 thamani ya amana hiyo ilikuwepo katika mahesabu ya Wakaguzi na waliridhika.

Mheshimiwa Spika, amana ya pili ambayo ndio inajumuisha pesa hizo zote ambayo ina namba EB/97/51 yenye thamani ya US Dola 2,048,655 na yenyewe pia ilithibitika baada ya kuonyeshwa kwamba hiyo nayo ilipelekwa na imeiva tarehe 9 Juni na pesa zake kuwekwa kwenye *credit* pia na hiyo ikaonesha kwamba hakukuwa na tatizo. Kwa hali hiyo, *CAG* anaanda taarifa ya mwisho ambayo ataiwasilisha kwenye *POAC* mwisho wa mwezi Julai. Naomba kwa jambo hilo, tuvute subira tuone mwisho wake utakuwaje kwa sababu yote hayo yameonekana kwamba kulikuwa hakuna upotevu.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nizungumzie kuhusu kiwango cha *Concession Fees* ambapo Mheshimiwa Aloyce Kimaro aliliongelea kwamba ni kidogo. Napenda tu nizungumzie kwa kifupi kwamba, mwanzoni jinsi ambavyo hizi fedha zilivyokuwa zinachajiwa ilikuwa Serikali tunapoteza mapato mengi na ilikuwa ni njia ambayo Maafisa wanakwenda kwenye mahoteli, wanamuangalia na kukadiria wenyewe wewe utatoa shilingi kadhaa. Hiyo hatuwezi kuona kwamba ni njia sahihi tukaamua kwamba tutafute njia sahihi. Njia sahihi ya kwanza, ilikuwa kwamba watoe katika *flat rate*, lakini katika hiyo *flat rate* baadaye ikaonekana pia bado Serikali tunapunjwa. Kwa sababu kuna mtu ana hoteli kubwa mwingine hoteli ndogo, itakuwaje wote watoe sawa?

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo tukaamua kukutana pamoja na wadau wetu ambao ndio wenye mahoteli na sisi Wizara na wataalam kukubaliana muafaka tufanye nini. Ndiyo muafaka ukakubaliwa wa kutoza kwa kutumia *percentage*. Hii *percentage* ni kwamba ina kiwango cha chini ambacho kila mwenye hoteli anatoa, zaidi ya hiyo ndiyo inatumika sasa ile *rate* ya kuongezea kufuatana na ukubwa na uwezo wa hoteli yake na ana vitanda vingapi na ana chaji kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, hii kwa kweli inafanya kazi vizuri na nina uhakika kwamba *TANAPA*, Ngorongoro na wengine wote wameridhika nayo na hii tunapata hela nyingi kuliko ile Dola 25 ambayo Mheshimiwa Kimaro alikuwa anasema ni kubwa. Sasa hivi tunapata zaidi ya hapo na ni njia halali ambayo tumekubaliana na wadau wetu na mahoteli makubwa yanalipa zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda pia niongelee suala la Mheshimiwa Mariam Faki kuhusu mambo ya lhefu ambayo yanayohusu wanavijiji ambao wengine walisema kwamba hawakulipwa sawasawa fidia zao na wengine wakasema kwamba mipaka ile imeingilia sehemu ambazo wananchi wanakaa. Jambo hili tunalitatua, tumeshirikiana na Mheshimiwa Mbunge Estherina Kilasi na timu yangu ya wataalamu na tumekubaliana ile ramani tunairudia upya na kweli kuna vijiji ambavyo majina sasa hivi siwezi kuyakumbuka sawasawa lakini tumeona vijiji kama vitatu au vinne, tutavitoa ndani ya hifadhi, vyenyewe vitakuwa kwa nje. Kwa hiyo, tunaanza kuchora upya na tutaleta kwenu kwa idhini yenu ili tubadilishe *GN*.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kwa haraka niongelee masuala ambayo yalijitokeza kwenye upande wa Idara ya Mambo ya Kale ambapo Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya na Mheshimiwa Col. Feteh Saad pamoja na Mheshimiwa Gaudence Kayombo, wenyewe wote hoja yao ni kutambua na kuboresha maeneo ya malikale na makumbusho ya Taifa. Napenda kusema kwamba yote hayo tumeyapokea na baadhi ya hayo tayari sasa hivi tumeshaanza kuyaainisha yakiwemo mengi na kwa sababu ya muda ni mdogo, naomba hawa Waheshimiwa baadaye tunaweza tukaonana mimi na wenyewe pamoja na Mkurugenzi wangu wa mambo ya kale ili tuweze kuwafahamisha wapi tumeainisha na yote ni kwamba sasa hivi ndio mwelekeo tunaoelekea kuhakikisha kwamba utalii huu wa utamaduni na wa historia tunausisitiza zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ujiji, njia ya kati ya Utumwa, sasa hivi ni eneo ambalo tunaliweka liwe la kitalii. Kwa hiyo, kuanzia Ujiji, njia ile ya kati ina vituo saba kupitia Tabora kwenye Tembe la Kwihara, unashuka nayo kote mpaka Pwani, ile yote tumeshaitambua na tumeiainisha na sasa hivi tuko katika jitihada za kutaka iorodheshwe katika Urithi wa dunia.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, pia naomba nizungumzie suala la Ngorongoro. Kwa upande wa Ngorongoro kuna masuala mawili ambayo napenda niyazungumzie haraka. La kwanza, linahusu kilimo cha kule Ngorongoro. Baada ya kuanza kutembelea hizi Mbuga mbalimbali nilipita kule, kwa kweli mimi mwenyewe nilisikitishwa na jinsi ndani ya *Crater* ng'ombe walivyokuwa wamejaa wanazunguka mle mpaka na mmomonyoko wa udongo unaanza kuathiri. Lakini kwa nje sehemu mbalimbali nilishituka kukuta mashamba.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, niliwaomba pia Kamati ya Mazingira na wenyewe wakatembelee waone hiyo hali, wakaenda na wenyewe kuona hiyo hali na ndio ambao Mheshimiwa Ndugai alitoa mchango wake pale mwanzoni. Ukweli ni kwamba kwa kufuatana na taratibu zilivyo, ni kwamba mle ndani hakuruhusiwi kulima. Lakini hata hivyo Serikali iliweza kutoa kipindi kifupi kwamba wajikimu kwa mazao madogo madogo ya kuwasaidia, lakini wakati wakitafutiwa sehemu za kudumu kwenda kulima. Kazi hiyo kwa upande wa Ngorongoro ilishafanywa na Ngorongoro katika kufanya kwake kuna sehemu mbili, moja inaitwa Sale na nyingine Oldonyo Sambu, huko tayari tumeshahamishia jumla ya familia 586 na kule tunawatengenezea miundombinu, shule, maji, barabara na kila kitu. Lakini pia kazi hiyo tunaomba ushirikiano, kwa sababu kimaelekezo ilitakiwa Mkoa wa Arusha ndio walipewa agizo la kutafuta sehemu hizo na sasa hivi tuko katika mazungumzo na Mkoa wa Arusha kuwakumbushia kwamba watusaidie na wenyewe kutafuta sehemu nyingine ili wenzetu hawa waweze kuhamia wale wanaotaka kulima.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba lile eneo linaweza kuhifadhi jumla ya familia 8000 na sasa hivi kuna familia zaidi ya 64,000 ambapo kwa kweli ni mzigo mzito ambapo sehemu ile haitaweza. Lakini hata hivyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Ole Telele kwamba sisi hatuna ugomvi na ndugu zetu wa Kimasai wanaoishi mle kama wanaendelea kuchunga, ugomvi wetu ni kulima. Kwa upande wa kulima, kwa kweli kule hatuwezi kuruhusu kwa sababu itaharibu taratibu zote na ni sheria ambayo tulijiwekea. Lakini kwa upande huu, napenda kuwaambia pia na ndugu zetu wote na wapiga kura wako kwamba hakuna anayefukuzwa kwa sababu ya kukaa na mifugo, tunawaondoa ambao wanataka kulima mle ndani na taratibu tutazifuata kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanatafutwa.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili pia ilikuwa kuhusu malalamiko ambayo Mheshimiwa Ole Telele... *(Hapa Kengeele Ililia kuashirikia muda wa mchangiaji kwisha)*

**SPIKA:** Endelea kidogo Mheshimiwa Waziri, ulikuwa na...

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, asante! Lalamiko la pili ni kwamba Mheshimiwa Ole Telele alimwuliza Waziri Mkuu kuhusu kwamba kulikuwa na *operation* iliyofanyika nyumba zikachomwa na mali za watu zikaharibiwa. Suala hilo mimi nimelifuatilia, ni suala ambalo kwanza nilitaka kujua kama Wizara yetu au Ngorongoro inahusika, lakini maaskari wetu wa

Ngorongoro hawahusiki na *operation* hiyo. Hata hivyo nikafuatilia kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa akasema kwamba *operation* hiyo ya kuwahamisha wamefanya wenyewe Mkoa wa Arusha. Lakini kwa kufuatana na maelekezo ya Mkuu wa Mkoa, yeye alichosema ni kwamba walijaribu kutoa elimu na pia wakawashirikisha viongozi wa Wamasai wafugaji na watu mbalimbali na waliwapa muda wa kutosha ili wahame, lakini baada ya hapo kwa kufuatana na maelekezo ya Mkoa ni kwamba wananchi wale wafugaji wenyewe waliondoka kwa hiari yao, hakuna aliyesukumwa kwa nguvu. Lakini pia kufuatana na ripoti hiyo inasema kwamba wenyewe waliamua kwa sababu wanahama, kuchoma yale maboma yao. Hiyo ndiyo ripoti niliyoipata.

Lakini, hata hivyo, Mheshimiwa Ole Telele kama nilivyokuahidi, ni kwamba mimi nitakuja kule ili tuweze kuangalia, tuweke sawa ili kuwe na amani kati ya mwekezaji na wananchi wa kule kwa sababu wanaishi vizuri kwa kweli. Mara ya kwanza nilipokwenda kukagua, nilikuta mwekezaji na hawa wananchi hawana tatizo kwani mwekezaji kwanza, kawajengea shule ya sekondari, shule za msingi, barabara, madaraja yote kawajengea. Halikadhalika pia kawajengea zahanati ambayo ndiyo ya Wilaya na kila kijiji kinapewa milioni 50 za kutumia kwa ajili ya kazi zao. Kwa kweli hana mgogoro nao. Kama kuna mambo machache mengine, yanatokea kwa kufuatana na watu mbalimbali. Tuna *NGOs* kule nilikwenda kuzionya ambazo hizo pia zinasaidia kuweka mtafaruku kati ya wananchi na mwekezaji. Nimezionya nikawaambia kwamba wakiendelea hivyo, tutawafutia leseni wasitoe misaada kule. *(Makofi)*

**SPIKA:** Una dakika tano tu sasa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Lah! Haya! Mambo ni mengi sana, hata kwa dakika tano sijui nitafanya lipi! Lakini naomba tu niongelee la matangazo ya *CNN* ambalo pia hilo lilikuwa ni jambo ambalo wengi wangependa kujua. Ni kweli kwa sasa hivi Wizara ya Maliasili tumefanikiwa, tunatangaza kwa kutumia *CNN* Duniani kote na watu wanatufahamu na kutusikia. Lakini pia napenda kuongelea mikataba iliyofanywa. Mikataba ya *CNN* ilikuwa miwili. Mkataba wa kwanza ulikuwa mwaka 2007/2008 ambapo Dola za Kimarekani 750,000 zililipwa kwa *CNN* kwa ajili ya kutangaza na hela hizo zilitoka *TANAPA*. Kwa ajili ya kuweka mahesabu sawa, ilishauriwa ni vyema *TANAPA* ndio wasaini mkataba ili kwao kwenye vitabu vyao hata *Auditor* akija isije ikaonekana kwamba hela imetolewa, kuna mkataba na *TANAPA* haikuhusika kwa njia moja au nyingine. Lakini la pili, pia kuna mkataba wa pili wa *CNN* ambao ulikuwa wa mwaka 2008/2009 na pia *TANAPA* walilipa jumla ya shilingi milioni 950 za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna mkataba mwingine ambao tumefanya kwa ajili ya utangazaji, naomba nalo lifahamike kwamba kuna mabasi 100 Mjini London na Taxi 100 Mjini London na Vituo 25 vya Treni vya *Undeground* Uingereza, halikadhalika na viwanja vya ndege vinne kikiwemo na *Hethrow* ambako kote huko tumeweka matangazo yetu. Kazi hiyo ilifanywa na kampuni inayoitwa *Jambo Publications Limited* na ambapo kwa kazi hiyo walilipwa jumla ya Paundi za Kiingereza 272,006. Yalishindanishwa makampuni matatu ikiwemo *Jambo Publications*, nyingine inaitwa *London Outdoor Advertising Company* na nyingine *TaxiAD Company* zote za Uingereza na Jambo *Publications* ndiyo iliyoshinda ikapewa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba bado yako mengi, lakini naomba niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba yale yote ambayo kwa muda huu sikuweza kufanikiwa kuyasema, lakini naomba niwahakikishie kwamba tutayaleta kwa maandishi na yote tumyapokea na michango yote ni mizuri na ni michango ambayo itanisaidia katika kufanya kazi zangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja! *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa, sasa kwa mujibu wa shughuli zetu, kulikuwa na kusudio la kutoa hoja ya kuunda Kamati Teule, sasa utaratibu wa Kanuni ya 117 unahitaji hoja hiyo iwe hapa kwa maandishi, sijaipata. Kwa hiyo, basi hiyo nayo sina namna, ni kwamba hoja sasa haipo, kwa sababu kwa mujibu wa kanuni ni lazima niwe nayo. Sasa naona kinachonyooshwa siwezi kukipata kwa muda muafaka. *(Makofi)*

Kabla hatujaendelea kwa hatua inayofuata, naona baadhi ya wageni wanaondoka na wengine ni muhimu. Wapo wageni wa Mheshimiwa Dr. Gaudentia Kabaka, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambao ni Viongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu wakiongozwa na Makamu wa Rais anaitwa Bwakea Johnia, yule pale. Halafu Edwin Ennos, Waziri Mkuu, Gosbert Bedson, Waziri wa Mikopo na Joseph Silvanus, Naibu Waziri wa Mikopo. Ahsanteni sana. Ahsante. Mnafanya mazoezi mazuri, baadaye mtakuja kushika nyadhifa hizo, tunawaombea Mungu katika masomo yenu na pia katika shughuli zenu za uongozi. Uongozi hutaka mtu upate uzoefu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, lakini kwa utaratibu wa Kanuni ya 100 na 101 nitamwomba Katibu atuelekeze hatua inayofuata.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 69 – WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

Kif. 1001 – *Administration and General*…………………Tsh.3,753,362,800/=

**MWENYEKITI:** Ngoja nichukue majina. Mheshimiwa Nsanzugwanko, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Nakei, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Kimaro, Mheshimiwa Manyinyi, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Luhahula, Mheshimiwa John Samwel Malecela, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Sijapata, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Malangalila na Mheshimiwa John Paul Lwanji na Mheshimiwa *Bishop,* eh! Hata wewe Askofu! Haya bwana! *(Kicheko)*

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *programme* hiyo hiyo 10, yenye mshahara wa Waziri, laini sina nia ya kuushikilia hata kidogo kwa sababu kwanza dada yangu siuhitaji mshahara wake bila shaka. Mimi ninalo dogo tu la kisera. Kule Kasulu hasa Kasulu Mashariki wakati wa *Operation* Kigoma kuna vijiji vilivyoanzishwa, lakini kutokana na mkanganyiko huo sera zetu hizi, tunaambiwa sasa vile vijiji viko kwenye maeneo ya *Forest Reserves*; vijiji vya Kigembe, vijiji vya Zeze na vijiji vya Mvugwe.

Mheshimiwa Spika, sasa mkanganyiko huu umekuwa mkubwa na hawa wanyama waharibifu hawa tembo wakienda kulisha mazao tunaambiwa wako nyumbani kwao kwa sababu ni sehemu ya *Forest Reserve*. Nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi na *assurance* tu, nilikuwa nimezungumza na Mkurugenzi wa wanyamapori tukaelewana kwamba anipe *assurance* na wananchi wasikie kwamba wakati umefika kuja kuhakiki upya ramani zile ili wananchi hao waendelee kufanya kilimo chao kwa amani na usalama. Nilikuwa naomba tu suala la ufafanuzi na *assurance* kwa Mheshimiwa Waziri. Nashukuru.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu kaka yangu Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko na napenda nimpe uhakika kwamba tutapita kwenda kuhakiki tena na h ii napenda kwa Waheshimiwa Wabunge wote wenye matatizo ya mtindo kama huo, naomba wala msisimame, napenda niwaambie kwamba sasa hivi tunapita sehemu mbali mbali na kuhakiki hii mipaka kwa sababu hali zinabadilika na kweli kuna sehemu zingine ambazo inabidi na sisi tuweze kubadilika na na kuweka hali inavyotakiwa. Isipokuwa tu, napenda kusema kwamba sehemu zile ambazo kutakuwa kuna jambo la muhimu ambalo halitawezekana, tutafahamishana kule tutaelewana. Lakini kwamba tutafanya, hakiki zote kuangalia hali halisi na jinsi mambo yanavyokwenda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Natumaini wale ambao mna suala kama hili hili tu, itakuwa ni kupoteza muda. Kwa hiyo, nikiwafikia mnaweza mkajitoa tu.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti. Ahsante sana. Mimi kwanza nianze na mimi kusema kwamba nampongeza sana na leo nimefarijika sana na Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyojibu hoja na kuweza kulishughulikia suala la Mbarali. Sasa nilikuwa naomba tu ufafanuzi na *assurance* ili kusudi wananchi wa Mbarali waweze kutulia. Kuna kero moja ambayo baada ya kufunga mjadala wa mipaka na furaha niliyonayo, ninaomba tu Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo kwamba kumekuwa na malalamiko ya fidia kwa wale ambao wameathirika na kuhamishwa na mimi nimechangia kwenye hoja, viwango kuwa vidogo, lakini vile vile wengine hawakuweza kulipwa kabisa. Kazi hii ilifanywa kwa ukaribu kabisa kati ya Halmashauri na *TANAPA* ambayo iko chini ya Wizara yake. Sasa kuna malalamiko mengi ambayo yaliwasilishwa kwenye Halmashauri kwa wale wananchi ambao hawakupewa fidia kikamilifu au kidogo sana au chini ya kiwango ambacho walistahili kupewa. Sasa ninaomba Waziri, kwa sababu Halmashauri haina pesa na *TANAPA* kwa hali waliyofikia hatujui yale malalamiko ya wananchi Waziri amewekea mkakati gani ili aweze kufunga mjadala huu wa kupanua Hifadhi ya Ruaha na *TANAPA* waweze kuwa na nafasi nzuri ya kuweza kutekeleza majukumu yao. Naomba ufafanuzi!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Estherina Kilasi kwamba suala hilo tulilizungumza, lakini pia na baadhi ya wananchi wake walikuja Ofisini kulalamikia kuhusu fidia kwamba waliyopewa ni ndogo na kuna baadhi ya wazee waliniambia kwamba walipewa mpaka Sh. 7,000/=. Kweli na mimi hilo sikulipenda, hata hivyo nikawaagiza *TANAPA* walifanyie kazi na tuone kwamba wenyewe wakati wakishirikiana na Halmashauri hizi pesa zilikwenda wapi? Nimeomba kwamba tunataka tuone saini ya kila mwanakijiji, kwa sababu mtu kama amepewa hela awe amesaini. Tuone saini ili tujue kwamba huyu alipewa ngapi na alipewa kiasi gani. Pia bado kuna wale wengine ambao wana malalamiko kwamba walipunjwa ambao ilihakikiwa kwamba ni kweli na kuna baadhi ambao bado hawajalipwa, kuna awamu ya tatu ya malipo yataendelea. *(Makofi)*

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba kuna mgogoro wa *TANAPA* – Tarangire na wanavijiji vya Ayamango, Gedema na Gijedabu na ana ahadi ya kuja Babati ili kujionea hali halisi. Sasa ninachoomba ni kwamba atakuja lini Babati ili aonane na wananchi wa maeneo yale halafu waweze kuzungumza na kuona ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo?

**MWENYEKITI:** Akimtuma Naibu itatosha au unataka aje yeye tu? *(Kicheko)*

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aah, ni yeye mwenyewe kabisa aje! *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ni yeye tu, haya! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge jambo hilo aliponiambia mara ya kwanza nakumbuka ilikuwa kama miezi miwili iliyopita tukiwa hapa hapa Dodoma na nilimwahidi kwamba nitafunga safari. Sasa naomba nimhakikishie kwamba baada ya Bunge hili la bajeti litakapokwisha, nitatafuta tarehe muafaka, nitakwenda. Suala hilo nalifahamu na tumelizungumza naye kwa kirefu, nitakwenda mimi mwenyewe. Ahsante.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi. Naomba tu kupewa ufafanuzi. Mwaka jana nilizungumzia Kimondo cha Mbozi (*Mbozi Meteorite*). Kimondo cha Mbozi kinasadikiwa kwamba kilianguka zaidi ya miaka 2000 iliyopita na mahali kilipodondokea kijiji cha Ndolezi ni mahali ambapo pako wazi sana na kuna watu ambao wanakwenda kuangalia Kimondo chenyewe kwa ajili ya kujifunza. Unapofika pale, unakiona moja kwa moja, kiko wazi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mtu kukiangalia, halafu anakwenda kwenye kibanda kilichopo pale, unamwambia sasa pengine lipa Sh. 1000/= au Sh. 2000/=. Sasa mtu mwingine tayari ameshakuja pale, amekiona, haoni sababu ya kulipa hela tena. Kwa hiyo, mwaka jana nilimwomba Mheshimiwa Waziri, waboreshe mazingira ya mahali pale, wajenge kitu kama wigo na

kuboresha mazingira zaidi, lakini pia wakitangaze Kimondo chenyewe kwa sababu ni jambo la kisayansi kubwa sana. Inasadikika vimondo hivi viko sio zaidi ya saba duniani. Kwa hiyo, nikamwomba Mheshimiwa Waziri atupe pesa, mwaka jana wakatenga shilingi milioni tano. Shilingi milioni tano hazijafanya tofauti yoyote. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri tena atupe ahadi wananchi wa Mbozi na hasa wale ambao wako katika eneo ambalo Kimondo chenyewe kipo pale. Kama yeye mwenyewe atakuja Mbozi, atembee aone umuhimu pengine wa kukijengea vizuri zaidi ili kiwe pia ni chanzo cha mapato kwa ajili ya nchi yetu. Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi! Inaelekea mwaka huu utakuwa na utalii wa ndani, huendi nje kabisa! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwaka jana tumeongea hilo jambo na ndio hapo tukapeleka hiyo pesa. Tatizo kubwa ni kwamba vivutio nchi hii vya kihistoria na vya kiutamaduni viko vingi sana na Idara ya Mambo ya Kale sasa hivi wameanza kuvitafuta na kuviweka sawa. Mpaka sasa hivi tunavyo zaidi ya 500 nchi nzima. Tatizo ni bajeti yetu ndogo kwa sababu kila moja inatakiwa tuiendeleze ikae kwa njia ambayo inaweza sasa ikatumika. Lakini napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kwake tulishaanza, tutatuma tena pesa kwenda kusaidia kumalizia. Ahsante.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kunipatia nafasi. Mimi nilikuwa nataka tu kupata ufafanuzi juu ya masuala mazima ya *percentage bed fee*. Kwa ruhusa yako, ningependa kunukuu *Hansard*. Mwaka jana nilileta swali hili ilikuwa tarehe 31 mwezi wa Nane kuhusiana na masuala mazima ya *Hansard*, ninukuu jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri lililosema kwamba: "Serikali imefanya mapitio na kuandaa kanuni zote zitakazoanza kutumika hivi karibuni. Kanuni hizi mpya zimeainisha viwango vya mapato ambapo mgawanyo utakuwa asilimia 15 kwa Halmashauri na asilimia 65 kwa Jumuiya za Wananchi na asilimia 20 tu ndiyo itakayokwenda Serikali Kuu. Asilimia hizo ni kwa mapato yote ya makusanyo ya ada ikiwa ni pamoja na na *bed fee*. Hivyo, kanuni hizi mpya za mapato kwa wananchi na Halmashauri zitatumika pia kwa Halmashauri ya Serengeti".

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hivi sasa tunavyoongea, Halmashauri hii ya Serengeti haijaanza kupata mapato haya. Nilikuwa naomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha mdogo wangu Mheshimiwa Rosemary Kirigini kwamba kanuni tumeshamaliza kuziandaa na ziko tayari na zimeanza kutumika kuanzia tarehe 1 mwezi huu wa Julai. Kwa hali hiyo ni kwamba, sasa inatakiwa tutoe elimu sehemu mbalimbali na kuwaelimisha jinsi ambavyo watatumia kanuni hiyo kwa ajili ya kuweza kutoza hizo tozo mbalimbali. Namhakikishia kwamba na kwao huko kote tutapeleka na sio kwao tu, kila mahali tutawapelekea zile kanuni waweze kujua kwa upande wa tozo watatoza namna gani.

**MWENYEKITI:** Kumbe zilikuwa hazijaanza! Zimeanza Julai Mosi, wote tujue hivyo kwenye Wilaya zetu.

**MHE. MASOUD ABDALAAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kupata ufafanuzi juu ya mbao 1981 zilizokamatwa pale Mabagala za kijana Makame Ali Baruti ambapo alifunguliwa kesi Namba CC.328 ya 2006 na kesi kwisha mwaka 2007 na hukumu ikatolewa, vielelezo nikampa Mheshimiwa Naibu Waziri. Nilikwenda Wizarani mara mbili, Mheshimiwa Naibu Waziri akaniahidi kwamba jambo hili linashughulikiwa na ufumbuzi utapatikana. Naomba ufafanuzi kwa kina.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kulikuwa na taarifa hiyo. Kama nilivyomwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kuwa nimeongea na Mkurugenzi wa Idara ya Misitu akasema anafanya uchunguzi kwenye hicho kituo, sasa kwa bahati mbaya sana baada ya kuwa tumezungumza hivyo, alisema kwamba atawasiliana na kijana mwenyewe na nikawa nimempa jina lake. Sasa mawasiliano kati yao na mtu mwenyewe mhusika sikujua yamefikia wapi. Jana baada ya kuwa limejitokeza, tukawa bado hatujakamilisha kupata taarifa kamili kwamba limefikia wapi. Namwomba Mheshimiwa Mbunge

kwamba kwa sababu ni jambo mahsusi, tutalifuatilia na kwa hakika kwa sababu hukumu ya Mahakama ilishatoka, ni utaratibu wa kawaida wa kumrejeshea na kama kuna lolote lililotokea, tutatafuta nyingine tuhakikishe kwamba tunamrejeshea mbao zake.

**MWENYEKITI:** Msichukue muda mrefu!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu ufafanuzi wa Waziri kuhusiana na maelezo aliyokuwa ameyatoa kuhusu ile *issue* ya Nyara za *Vietnam*. Zile Nyara zinatoka wapi? Ni Ndovu wanauwawa kwenye Mbuga zetu au ni Nyara ambazo zinakuwa zinakatwa zinahifadhiwa Wizarani kama Nyara ambazo zimekatwa na majangili na zinaibiwa? Kama zinaibiwa Wizarani, kuna utaratibu gani wa Wizara kufanya *stock taking* mara kwa mara ili kuweza kugundua, maana kiwango cha Nyara ambacho kimetajwa ni kikubwa sana? Pia tungependa kufahamu thamani ya Nyara ambazo zimekamatwa kule Vietnam ni kiasi gani.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kusema kwamba, sio rahisi kufahamu kwamba zile nyara yaani meno yametoka wapi, kwa sababu yameingia kisirisiri, Wizara ya Maliasili hatukufahamu. Yamepelekwa bandarini kama mzigo wa plastiki. Kwa hali hiyo, kama nilivyosema wakati nikizungumzia suala hilo kwamba kuna mianya mingi hata nchi za jirani wakatumia bandari yetu kuleta meno ya tembo wao yakasafirishiwa hapa. Lakini napenda nimhakikishie kwamba kwa upande wa meno tuliyonayo sisi kwenye ghala letu, jambo la kwanza, nilimwagiza Mkurugenzi wa Wanyamapori, hakiki meno yetu: Je, kuna *loss* yoyote, kuna kitu kilichopungua? Isije kuwa kuna ujanja, yanachukuliwa hapa, yanakwenda huko. Amenihakikishia mpaka juzi kwamba ghala letu liko *intact*, hakuna hata jino moja lililopungua kwa sababu kwa njia tuliyoyapanga kuna *style* ya kuhakiki, kuhesabu kila wakati.

Likichomolewa tu, pale patabakia *gap*. Kwa hiyo, ni kwamba kwa upande wa kwenye ghala letu, hakuna kilichotoka. Sasa jibu ni kwamba, hayo yanayokamatwa huko, yanaweza yakawa aidha yametoka humu humu kwenye mapori yetu kwa majangili ambao kwa njia zao wakati mwingine wanatuzidi maarifa na nguvu, wanaua tembo wetu, ndio yanaweza yakawa yamekusanywa huko au inaweza ikawa ni mzigo umetoka nchi za jirani lakini wepesi wa bandari yetu au na mtandao wao ulikuwa unawaruhusu waingilie kwa huku kwetu. Kwa hiyo, yote yanawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpatie Mheshimiwa baadaye kuwa ni thamani kiasi gani ya meno yaliyopatikana Vietnam au kama akitaka na zile nyingine zote, naweza nikampatia baadaye. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani kwa kuwa pia kuna uchunguzi wa Kimataifa, *INTERPOL* Kimataifa inashughulikia, tuwe na subira, tutajua yote hayo.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu jana, nilimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kupunguza bei ya *Visa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka ufafanuzi; wageni kutoka Marekani kawaida *visa multiple* ni *dollar* 100 na *single entry* ni *dollar* 50; je, zimeshuka bei sasa multiple itakuwa ni 50 na single ni 25? Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, kama Mheshimiwa Rais alivyosema kwamba, tutapunguza visa na tulikubaliana *flat rate* ya *50 US Dollars*. Makubaliano zaidi kati yetu na wenzetu Wizara ya Mambo ya Ndani ni kwamba, hatukufikia kama *flat rate* ni aidha *multiple* au *single.* Hiyo sasa ni yale ambayo Mheshimiwa Rais amesema kwamba, tunawasiliana kuhakikisha inapunguzwa.

Bado hatujakaa kikao, tukishakaa tutawatangazia wadau wetu wote kwamba, *visa* imekuwaje na ninyi muweze kupeleka habari kwa wateja wenu nchi za nje.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati nachangia, nilihoji maana ya kuweka ongezeko la thamani kwenye miti ya Serikali kule *Sao Hill;* lakini katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri hakufafanua hilo. Naomba anipe maana yake halisi ni nini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, kwa lugha nyepesi tunasema, mti unachajiwa VAT mara mbili, wengine wanasema *double taxation.* Kwa wataalamu wenyewe, ukiwaambia *double taxation* watakukatalia hawawezi kuiita hivyo, lakini kwa sisi tunaona ni *double taxation;* kwamba, kwanza, kama Mheshimiwa alivyosema na sisi wenyewe tunafahamu hiyo inachajiwa kabla mti haujavunwa. Pili, inachajiwa 20% ya *royalt* kabla mti haujavunwa na pia inachajiwa kupitia mbao, imeshakuwa *value added*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo hata Wizara yangu tumelipeleka sehemu zote na tumeweka mawasiliano na wenzetu. Kwanza, tulijaribu kushirikiana na TRA, wakasema kwamba, wao wamepewa kazi hiyo labda tujaribu Hazina. Hazina tumeongea nao, Mheshimiwa Mkullo amenihakikishia kwamba, wanalifanyia kazi kwa ajili ya kuangalia kutoa ile VAT ya kwanza. Napenda kusema kwamba, amesema wanalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaomba wafanye hivyo, lakini napenda tu nikueleze zaidi, kwa sababu wadau wako walipokuja ofisini kwangu, tuliongea kwa kirefu na nilikuahidi kwamba, tutalishughulikia na limefikia ngazi hiyo. Pia yale mambo mengine ya MDA, yote hayo tuna uwezo nayo. Wizara tunaangalia jinsi ya kupunguza MDA ili kupunguza unafuu zaidi. Ahsante.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba yangu, nilizungumzia suala la muwekezaji wa *Grumet Reserve,* jinsi ambavyo ilikuwa ni matatizo na karibu kila mwaka tunazungumzia kuhusu muwekezaji huyu. Nilizungumzia matatizo yalivyoongezeka kwa wananchi wanaoishi jirani na eneo lile, kiasi kwamba wapo wananchi wawili wamepigwa risasi mwaka huu ndani ya Hifadhi hiyo kwa sababu walifuatilia ng'ombe wao ambao walipotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kusikitisha zaidi, yupo mtoto wa darasa la saba, ambaye alikuwa amalize shule mwaka jana, amekatizwa masomo amefungwa miaka mitatu kwa sababu alikwenda kunywesha maji ng'ombe wa Baba yake kwenye Mto Lubada. Ng'ombe wakamtoroka wakaingia kwenye Hifadhi hii, akakamatwa amefunguliwa mashtaka na amefungwa. Naomba Serikali itoe ufafanuzi nini hatima ya sula hili?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, habari hizo Wizara yangu inazifahamu. Aliyekuwa wa kwanza kutoa taarifa hiyo kwangu, alikuwa Mheshimiwa Stephen Wasira, ambaye sehemu hiyo ni Jimbo lake.

Hata hivyo ni kwamba, nilimtuma Mkurugenzi wangu wa Wanyamapori, kwenda kuangalia hiyo hali na kuweza kuiweka sawa. Hatua ya kwanza tuliyoichukua kuhusu mgogoro kati ya *Grumet* na Wananchi na Maaskari; ni kwamba, kuanzia sasa wale maaskari ambao walikuwa wakilinda chini ya *Grumet* sasa watakuwa moja kwa moja chini ya Wizara. Sisi wenyewe ndio tunawaajiri na ndio tunawalipa, wala hakuna mtu mwingine anayefanya hivyo. Kwa hiyo, watakuwa chini ya *Command* ya Wizara na watafuata taratibu za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hilo la pili kuhusu huyo kijana ambaye amefungwa, sasa ule ni utaratibu wa mahakama. Kwa sababu walipelekwa huko na mahakama, ndio watenda haki, sijui wenyewe kufuatana na misingi ipi waliweza kutoa hukumu ya namna hiyo? Suala likishafika mahakamani linakuwa haliko chini ya uwezo wangu, lakini hata hivyo ni kwamba, mimi na Mheshimiwa Wasira tumekubaliana wiki hii tunakwenda kwenye sehemu hizo za migogoro kwenda kuweka mambo sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni mpaka ambao wananachi wanataka kunywesha ng'ombe wao na upande wa pili ndio mpaka wa Hifadhi. Ng'ombe hana akili, akifika pale anavuka; akishavuka tu kwenda kuweka mambo sawa, avuke kiasi gani awe salama isije ikaleta mgogoro kwa sababu maaskari wanatumia Sheria ambazo tunataka tukubaliane tuwekeane muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe hata kama anavuka, aswagwe arudishwe bila kuwa na vurumai za aina yoyote. Kuhusu huyo mwingine aliyejeruhiwa; hayo yote tukienda sisi tutakwenda na Mheshimiwa Mbunge muhusika wa pale tukayaangalie halafu tutatoa tamko rasmi.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba ufafanuzi tu, kwa sababu nilipewa taarifa zisizo rasmi kwamba, Wizara imeamua sasa kutumia fedha zilizotengwa mwaka 2006/2007, kiasi cha shilingi 5,000,000 kuanza kujenga Bwawa la Rungwa. Utaratibu wa awali, walisitisha kwa ajili ya upembuzi yakinifu, sasa imeonekana hakuna haja ya kuendelea na hatua hiyo, kumbe inawezekana kujenga lile bwawa kwa kutumia fedha hizo hizo.

Sasa habari hizo siwezi nikazichukulia kama ndiyo rasmi moja kwa moja, kwa sababu ni kama za kwenye makorido, ambayo hayawezi kunithibitishia uhalali wangu mbele ya wananchi kule Rungwa, kama nikiwaeleza hivyo. Naomba wanithibitishie hapa wenyewe kama kazi hiyo ipo na inaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Lwanji na niseme tu kwamba, jambo hili mimi na yeye tumekuwa tukilifanyia kazi kwa karibu sana. Hata hizo fununu za awali, *actually* ni mimi nilimdokezea.

Sasa nimthibitishie tu kwamba, tumekubaliana kwamba, badala ya kuendelea na utafiti, kuna namna ambayo tunaweza kufanya haraka ba ujenzi kuanza na kwa hiyo hizi 100,000,000 zitaanza kutumika mwaka huu wa fedha, ambao unaanzia Julai Mosi na tunategemea mwaka ujao wa fedha, tutaweza kukamilisha lakini kazi itaanza mwaka huu.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Watalii wengi huwa wanakuja Mkoa wa Kigoma, wakati wanakwenda Hifadhi ya Gombe huwa wanaogopa kupita ndani ya maji. Sasa hivi kuna barabara imejengwa kuanzia Chankele mpaka Mwamgongo na imefika upande wa Hifadhi ya Gombe; na kwa kuwa sasa hivi TANAPA ikitusaidia kujenga kile kipande kilichobakia Watalii wanaweza wakaja kwa wingi na tukapata fedha nyingi kwa ajili ya kwenda kuangalia Sokwe walioko pale; je, TANAPA wanaweza kutusaidia kujenga kipande kilichobakia?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande kilichobakia ni urefu wa kilomita tatu. Hata Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuja mwezi Juni mwaka huu, kufungua hiyo barabara ambayo inaendelea kujengwa, alituagiza kuwa TANAPA tuangalie uwezekano wa kumalizia hiyo barabara ya kilomita tatu ili iingie ndani ya Gombe na hilo suala tumelipokea na tunalifanyia kazi, tutatafuta fedha tutafanya kazi.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shida na mshahara wa Waziri. Nataka ufafanuzi tu na hatua za kuchukua.

Katika mchango wangu wa maandishi nilieleza jinsi Wafanyakazi wa Chuo cha Olmotonyi cha Misitu wanavyoishi kwenye nyumba chakavu kabisa, ambazo nyingi zilirithiwa wakati wa Ukoloni, lakini bado Serikali imeendelea kuwakata pango Wafanyakazi hawa. Ninaishauri Serikali iwaache waishi katika nyumba hizi na isikate pango kama motisha; mazingira ya chuo kile ni magumu jamani.

Mheshimiwa Waziri, naomba *intervention* yako, waacheni Wafanyakazi hao waishi bure na msiendelee kuwakata pango kwa sababu nyumba zile zinatia huzuni na mpaka wakati mwingine unaweza kumwona aliyeko ndani.

**SPIKA:** Hiyo ndiyo huruma ya Kimissionari.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba na mimi mwezi wa nne nilikwenda kutembelea Olmotonyi na hali ya hizo nyumba naifahamu. Tumepokea ombi la Mheshimiwa, lakini pia hata bila ombi ni wajibu wetu kuangalia Wafanyakazi hao.

Ninamhakikishia kwamba, tutalifanyia kazi. Tutaangalia uwezekano wakae bure kwa muda, tukishazikarabati tunaweza kurudisha ada fulani.

**MHE. DKT. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka kuuliza swali moja kuhusu wale ambao wanajeruhiwa na wanyamapori na kupata kifuta jasho. Wale wanaouawa hawapewi chochote na wakati wana ndugu zao, wana watoto wao na familia zao; je, Mheshimiwa Waziri unasema nini kuhusu suala hilo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na Sheria Mpya ya Wanyamapori, ambayo mliipitisha hapa Bungeni na sasa hivi tuko katika maandalizi ya kuandaa kanuni zitakazotumiwa. Mojawapo ya sehemu ambayo tunaishughulikia itakuwa ni hiyo ya fidia na vifuta jasho vya aina mbalimbali. Napenda kusema kwamba, mtu anapokufa ni kwamba, huwa tunatoa aidha fidia au kifuta machozi.

Mheshimiwa Spika, huwa tunahakiki tuweze kujua kwenye mirathi inasema nini; kwa wengi tunashindwa kutoa mapema kwa sababu tunangojea *report* ya mirathi ya kimahakama kwamba, nani ndio mrithi aweze kukabidhiwa pesa hizo. Kwa hiyo, nawasihi Waheshimiwa Wabunge, kama kuna sehemu yako inayokuhusu kwenye Jimbo lako, kuna hali kama hiyo, wasaidie Wananchi kupata ile hati ya mirathi tujue tunamkabidhi nani. Hii ni kwa sababu, hati ya mirathi huko mahakamani huwa ngumu kwa mtu kuhangaikia mwenyewe, tunaomba muwape ushirikiano.

**MHE. DKT. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia sina nia ya kukamata mshahara wa Waziri, lakini ningeomba maelezo mafupi tu kuhusu maombi ambayo niliomba mwaka jana. Mwaka jana nilisema njia fupi kuliko zote ya kwenda *Ruaha National Park* ni kutoka Mpunguzi, Mwitikira, Mmanda na Ilangali; na nikajibiwa kwamba, jambo hili lingeliangaliwa. Katika hotuba ya mwaka huu, sikuona maelezo popote kama kuna chochote ambacho kitafanyika na TANAPA ili kuitengeneza barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo ningependa nimwombe Waziri, afikishe shukrani zetu kwa TANAPA, kwa kusaidia kujenga Shule ya Sekondari ya Mhayungu; ambalo ni jambo jema.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hiyo barabara anayoisema Mheshimiwa DKT. Malecela, kwa sababu na mimi ni mwenyeji kidogo naifahamu na ni fupi wala siyo uwongo. TANAPA katika bajeti yake, kati ya njia ambazo watazitengeneza huwa wanaongelea kwa jumla kuwa, watatengeneza kilomita kadhaa; lakini utaratibu kwamba wapi na wapi ndipo watafanya kazi hiyo wanafafanua wenyewe.

Sasa kwa sababu ni ombi na ni ahadi ambayo tuliitoa mwaka jana, naomba kumuahidi kwamba, nitazungumza na TANAPA, tuone jinsi gani ambavyo kwa mwaka huu tutaweza kuitimiza ahadi hii.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHUILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Waziri na Wizara kwa ujumla, kwa sababu wamekubali kwenda kuchimba bwawa katika Kijiji cha Nsango. Huu ni ujirani mwema na hata msaada ambao wameutoa wa shilingi 8,000,000 kwa ajili ya kusaidia Shule ya Msingi Kashozi**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nipate ufafanuzi; Wafugaji wa Wilaya ya Bukombe wanapata shida sana na kama alivyoeleza Mheshimiwa Nsanzugwanko, shida ambayo tunaipata ni kwa ajili ya tatizo la mpaka. Wanaposogea kule wafugaji wanakamatwa na Idara ya Wanyamapori, wanatozwa hela nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba, kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji hawa, wakati mnakuja kurekebisha mipaka, ikiwezekana hata kuongeza mipaka kidogo. Wilaya Bukombe yenye makazi 40% na mifugo mingi sana ili mtusaidie wafugaji hawa wasiendelee kunyanyaswa na hasa Idara ya Wanyamapori, inavyowatesa kule wafugaji wangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kumhakikishia usalama wa wafugaji.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nitaweza kumhakikishia ni kwamba, tutakwenda kuangalia hali; lakini kusema kwamba, tutaweza kupunguza ile mipaka ni jambo ambalo kisheria sasa hivi mpaka ni mpaka na hatuna uwezo wa kuubadilisha. Tukiona kwamba, kweli kuna tatizo ambalo litahitaji mabadiliko, tutaleta Bungeni kwa Waheshimiwa Wabunge ili muweze kuliridhia, kwa sababu Sheria hizo mliziweka ninyi na mipaka ile pia mliiridhia ninyi.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la hoja yangu ya jana lilikuwa ni kuongeza mapato ya Serikali. Katika maelezo yangu nilisema kuwa, utarartibu wa zamani TANAPA walikuwa wanakusanya takriban Sh. 4.6 na katika utaratibu waliokubaliana wa *dollar* 25 kwa kitanda, TANAPA wangepata takriban shilingi bilioni thelathini. Katika utaratibu mpya wa Wizara, TANAPA watapata takribani shilingi bilioni 5.5. Katika majibu yake, Waziri hakutoa takwimu yoyote ila alisema kwamba, mapato yataongezeka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa yote yameingia kwenye Hansard na tutapata takwimu mwaka ujao, sasa nakubali kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja na mshahara wa Waziri. Kwenye mchango wangu wa maandishi, niliulizia jinsi gani sasa familia za Kilimanjaro zitashirikishwa katika kuotesha miti na kuweka uhifadhi wa Mlima Kilimanjaro katika hali nzuri, kwa sababu ile theluji inazidi kuyeyuka.

Kwa vile Wabunge wote wa Kilimanjaro waliwahi kukutana na Mheshimiwa Waziri na kumwomba katika mapato ya Mlima huo, uwepo mgao ambao utafikia familia hizo hususan wanawake, ambao wangependa uhifadhi wa mlima na kwa vile wanateseka katika yale maporomoko ya mlima. Nilikuwa naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upandaji miti kisera ni kwamba, tuna utaratibu wa kupanda miti kila Mkoa. Upandaji huu unafanyika na wananchi wenyewe na Wizara imekuwa haitoi ruzuku yoyote zaidi ya kuhamasisha jambo hilo. Sasa hivi kuna mazungumzo yanaendelea kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kuhusu kudhibiti ongezeko la joto Duniani.

Mheshimiwa Spika, kuna mpango unaitwa *Reduced Emition Through Degradation and Deforestation* (RED*),* Mradi huu utakuwa unatoa fedha. Misitu ambayo imehifadhiwa itakuwa na uwezo wa kuomba fedha kutoka kwenye Mfuko Maalum, kwa ajili ya kuimarisha misitu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafikiri kwamba, hii njia inaweza ikasaidia sana kwenye eneo hili. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Mbunge atupe fursa ili tuweze kukamilisha Mpango huu na tuone ni namna gani Wananchi wa Kilimanjaro wataweza kunufaika kwa kuwepo msitu huu.

**MHE. ENG. STELLA M . MANYANAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesadifu utendaji wako wa *speed and standard;* na kwa kuwa katika majibu mengi aliyotupa yanaashiria Mkoa wa Ruvuma kunufaika kwa kuufanya kuwa Mji wa Kihistoria na kishujaa kwa ajili ya Utalii;

Katika misingi ya sasa ya ufuatiliaji na upimaji, yaani *monitoring and evaluation,* inatakiwa tuwe na *smart indicators.* Katika jibu lake, hakukuwa na *time frame;* nilikuwa naomba anifahamishe kuhusu suala hilo la kuutangaza Mji huo; na kwa kuwa kuna sheria inatakiwa kubadilishwa kwa kadiri ya taarifa yake alivyoizungumza; je, anategemea utaweza kufanyika ndani ya kipindi kufikia tarehe 27/2 mwaka unaofuata ili uwe umeshatangazwa rasmi na yeye mwenyewe kuwa sehemu ya maandalizi ya kutangaza rasmi siku hiyo?

**MWENYEKITI:** Siku hiyo ina maana gani sasa 27/2?

**MHE. ENG. STELLA M . MANYANYA:** Hakika kabisa kama itawezekana.

**MWENYEKITI:** Nasema hiyo siku ni ya nini; kwa nini husemi March au April?

**MHE. ENG. STELLA M . MANYANAYA:** Nimeichagua siku hiyo, kwa sababu ndio siku ambayo tumekuwa tukisherehekea shughuli zile za Maji Maji.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Maji Maji ni suala ambalo sasa hivi Wizara yangu tunalishughulikia. Suala hili tulianza kulifanyia kazi tangu Mheshimiwa Monica Mbega akiwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma na ndiye yeye alileta maombi rasmi. Nilituma *team* huko inashughulikia na tunahakikisha kwamba; ni kivutio kimojawapo ambacho baada ya muda, kitakuwa tayari ni sehemu ambayo tutaanzia kutangaza mambo mbalimbali ya ushujaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyokwisha ahidi, namwomba avute subira; ila sina uhakika na sitaki kumuahidi kwamba, kwa tarehe hiyo anayoitegemea yeye patakuwa tayari, kwa sababu maandalizi ni mengi na tunataka tupaweke pakae vizuri ili hata watalii wakija pale wawe na sehemu ya kukaa na kupumzika.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya mwisho katika kuhitimisha hoja hii. Imani yangu ni kwamba, nadhani sasa majibu yangu yatakuwa ya matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nimesema Mkoa wa Mara na Mji wa Musoma kwa ujumla, unaitegemea sana Serengeti pamoja na Arusha katika mahitaji yake ya kila siku. Mfano, magari yote yanayofuata mizigo Arusha, lazima yapite katika Hifadhi ya Serengeti, lakini kutokana na ile mbuga ya wanyama tunahitaji kupeleka kule vyakula kwa ajili ya wananchi. Hali kadhalika na ajira zinazopatikana pale Mbugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa bahati mbaya sana, Ofisi zote za TANAPA na SENAPA, zipo katika Mkoa wa Arusha. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba, kwa nini isiwepo Ofisi hiyo ya TANAPA na SENAPA pale Mkoani Mara (Musoma) ili kuwezesha wale Wananchi wa Musoma kupata hizo fursa kwa karibu zaidi kuliko kila wakitaka kupata mpaka wasafiri kwenda Arusha na kutokana na hali hiyo kwao inakuwa ni adha?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Mbunge alitaka ufafanuzi kwenye eneo hilo. Jibu ni kwamba, TANAPA katika mipango yao ya zamani, walikuwa wamelenga zaidi kuimarisha vituo vilivyokuwepo. Jana tulijadiliana nao kwa kina na tukawa tumekubaliana kwamba, jambo hili watalifikiria kuona namna gani wataweka kituo kidogo kwenye eneo hilo, kutokana na umuhimu wake. Kwa hiyo ni jambo ambalo wataliweka kwenye mipango yao, kadiri fedha zitakavyoweza kupatikana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*.................................. Sh. 817,274,400
Kif. 1003 - *Policy and Planing*............................................Sh. 777,893,000
Kif. 1004 - *Communication Unit*................................ Sh. 62,973,800
Kif. 1005 - *Internal Audit Unit*...............................................Sh. 115,955,400
Kif. 1006 - *Procurement Management Unit*..................Sh. 262,512,300
Kif. 1007 - *Legal Unit*............................................................Sh. 68,860,000
Kif. 1008 - Management Information System................Sh. 180,000,000
Kif. 2001 - *Wildlife*...................................................... .Sh. 13,462,301,900
Kif. 3001 - *Forestry and Beekeeping*...........................Sh. 14,753,515,600

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif**.** 3002 - *Fisheries* ..........................................................................Sh. 0

**MHE. BALOZI DKT. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisimami hapa kutoa shilingi, bali naipongeza Wizara hii inayoongozwa na mwanafunzi wangu Shamsa Mwangunga. Naomba tu anifafanulie kwamba, Fisheries ni sekta mtambuka; ina *concept* ya vitoweo kama inavyokuwa chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Vilevile kuna *concept* za Maliasili katika suala zima la viumbe hai, ambao wako majini wanahitaji uhifadhi na *Development* ya *Wildlife*. Samaki nao ni *Wildlife;* je, kwa nini Waziri asifikirie zile *concept* haziwezi zikakaa tu chini ya Wizara ya vitoweo inapaswa pia ikae katika Maliasili?

**MWENYEKITI:** Kwa maana nyingine huku nako kuwe na fungu siyo? Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba mwalimu wangu Mheshimiwa Dkt. Mongella kuwa, jibu la harakaharaka sitakuwa nalo, lakini naomba nipokee ushauri huo ili tukaufanyie kazi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 - *Tourism* … … … … ......................... Sh. 6,126,984,100

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumai swali langu litaangukia 410700 - *Feasibility Studies, Project Preparation and Design.* Kulikuwa na suala la ujenzi wa barabara kutoka Machame Girls kwenda Getili, kuna wananchi walipata shida, mazao yao na baadhi ya majengo yaliharibika. Nilikuwa nimemwomba Waziri awafikirie fidia.

**MWENYEKITI**: Ilikuwa ni *KINAPA* ndiyo walikuwa wanachonga barabara.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, kifungu cha *Feasibility Studies, Project Preparation and Design,* kwa sasa hivi pesa zilizopo hapo ni kwa ajili ya mambo ya kazi ya *consultant* na kulipia *fees* kwa ajili ya kazi mbalimbali, zinazohusu mambo ya *hotel classification.*

Kwa kujibu swali lake ni kwamba, *KINAPA* ambayo ipo chini ya wanyamapori, ndiyo kwenye fungu lake imeweza kuongelewa lakini napenda kusema, nimepokea ombi lako na nitawasiliana na *TANAPA* na *KINAPA* ili tuhakiki jambo hili tujue tutasaidia kwa namna gani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4002 - *Antiquities Unit* ...............… … … …..........Sh. 4,409,366,700

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

**Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kif. 1001 - *Administration and General* ......... ... ... ... Sh. 244,648,300
Kif.1002 - *Finance and Accounts* … … … …............. Sh. 514,081,500

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … … … ......................................Sh. 0

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* Namba 1003, Subvote 4620. Naona kifungu hiki cha *Management of Natural Resources Program,* hakijapangiwa chochote. Katika mchango wangu nilisema ni kwa jinsi gani ambavyo wataalam wengi hata wa misitu, hawana utaalam wa kuweza kutathmini misitu kwa kitalaam ili kuweza kuthaminisha na kuweza kuendana na hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nategemea kwamba, Norway hawajatoa hela, lakini pia hata Serikali haijatoa hela kwa ajili ya kuandaa hizo programu mbalimbali za kuwawezesha Watanzania ili tuweze kusimamia vizuri rasilimali zetu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki ndicho ambacho Norway haikutoa pesa, lakini ni kwa muda tu, tunasubiri maamuzi mbalimbali yaweze kutolewa ili *Project* hii ambayo ni ya Serikali Mbili; ya Tanzania na Norway iweze kuendelea. Kusema kwamba, Tanzania peke yake watoe pesa kufuatana na ule mchanganuo, hautaweza kukidhi shughuli mbalimbali za huo mradi. Kwa hiyo, tunavuta subira kwa kuwa sasa hivi kulikuwa na mambo ambayo tulikuwa tunajadiliana yaliyositishwa. Baada ya muda tukishakubaliana, tukipata pesa zao na zetu ndiyo tutaendelea na *Project* hii. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Wildlife* … … … … ........................................Sh. 6647,031,800

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Programu ya Wildlife; kuna 6539 - *Wetlands Management and Sustainable Development.* Nataka ufafanuzi kidogo tu; chepe chepe ya Mto Malagarasi ambayo pia ni eneo kama ilivyo Kilombero pale, linaharibika sana kimazingira. Nilitaka kujua kama hii 1.9 bilioni ina-*involve* na Mto Malagarasi katika programu zao, kama siyo je, wanafikiri nini kuhusu *Ramsar Site*s ya chepechepe ya Bonde la Mto Malagarasi kwa sababu huu mto unapita kwenye Jimbo langu?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, pesa hizi pia Malagarasi, Moyowosi, imo ndani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

.

Kif.3001 - *Forestry and Beekeeping* … … … … .....Sh. 12,399,214,600
Kif.4001 - *Tourism* … … … …......................................... Sh. 4,444,215400

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.4002 - *Antiquities Unit* … … … … ........................Sh. 1,763,145,400

**MHE. DKT. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza kuhusu item 6530 inayozungumzia habari za *culture*; je, kule kulikoanzishwa Vita vya Maji Maji (Kipatimo Kilwa); pesa hizo nazo zipo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 6530 kinasema, *house and culture projects;* hizi ni pesa zimetengwa kwa ajili ya kukarabati *Museum* ya Dar es Salaam na pia kujenga *Museum* mpya pale pembeni, ambayo sasa hivi karibu itamalizika. Kufuatana na suala lake, nitamtuma Mkurugenzi wa Mambo ya Kale ili aweze kwenda huko kuona ni kitu gani ambacho tunaweza kukifanya. Sasa hivi tupo katika kuainisha shughuli zote hizi za utamaduni na historia. Kwa hiyo, atakuja huko pia kuangalia na tuweze kujua tushauriane tunafanya nini.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya*

*Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi, imepitia makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako likubali kuyapitisha makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2009/2010 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo imetolewa na imeungwa mkono; tunawatakia Waziri, Naibu Waziri na Timu yao yote, mzitumie fedha vyema ili kuzidi kuiendeleza nchi yetu na kupunguza umaskini katika nchi yetu ili maisha bora yatufikie wengi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo kidogo hapa; Mheshimiwa Job Ndugai anaomba Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, mkutane katika Ukumbi Namba 219. Ametamka hapa ni saa saba mchana, lakini nadhani kwa hali halisi ilivyo, pengine wanaweza kwenda moja kwa moja wakakutana ili wamalize mapema. Kwa hiyo, baada ya kuahirisha shughuli za leo, Kamati ya Ardhi Maliasili na Mazingira, Ukumbi 219, ghorofa ya pili.

Waheshimiwa Wabunge, kesho saa tano asubuhi kutakuwa na semina, iliyoandaliwa na Wizara ya Nishati na Madini. Mada yenyewe kwa Kiingereza ni *Power System Master Plan* na *Financial Recovery Plan* ya *TANESCO*. Kwa hiyo; ni Mpango Kabambe wa Nishati katika nchi yetu na pia namna ya kuikwamua *TANESCO*. Semina hiyo itaendelea halafu inapokamilika, kutakuwa na semina ya *EWURA,* ambao watakuwa wanajitambulisha kwetu. Kwa hiyo; ni mfululizo wa semina za *TANESCO* na *EWURA,* wenyeji wetu wakiwa ni Wizara ya Nishati na Madini.

Waheshimiwa Wabunge, hii ni muhimu sana nilikwishaisema, naomba sana muweze kuhudhuria, saa tano asubuhi, Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, leo Jumamosi tarehe 11, saa saba mchana Waheshimiwa Wabunge wa Kamati zifuatazo au makundi yafuatayo: Wabunge wote wa Mkoa wa Dar es Salaam, ambao siwaoni hivi sasa, Wenyeviti wa Kamati za LAAC, Miundombinu na Huduma za Jamii pia na Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mawaziri wa Afya na Utawala Bora, TAMISEMI, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Maji na Umwagiliaji, Fedha na Uchumi, watakutana katika Ukumbi nadhani itabidi uwe wa Pius Msekwa B na Mameya na Wakurugenzi wa Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam. Nadhani kuna jambo mahususi kuhusu Jiji letu la Dar es Salaam. Mawaziri hao au Manaibu wao, pamoja na Wabunge wote wa Mkoa wa Dar es Salaam, ukijumuisha pia wa Viti Maalum, mnaombwa mkutane pale saa saba Ukumbi wa Pius Msekwa B, kwa warsha muhimu na ambayo siyo ndefu sana.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa Klabu ya Kulenga Shabaha, Mheshimiwa William Shellukindo, ameniomba niwatangazie kwamba, lile zoezi la kulenga shabaha kule Makutupora, halitakuwepo kesho kwa sababu ya ile semina ambayo nimekwishaitangaza. Kwa hiyo, mtajulishwa tarehe nyingine ili wanachama wa klabu ya kulenga shabaha muweze kufanya shughuli hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa matangazo, napenda kwa niaba yenu, nimshukuru sana Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa jinsi alivyojibu mambo yake hapa. Tunapenda kuwapa Mawaziri ukweli wa namna hiyo, inasaidia sana kuliko mambo kuyaweka pembeni. Bunge la sasa huwezi kukwepa hata kidogo, ukijaribu ujanja utafikia pagumu tu. Kwa hiyo, nilikuwa naona niliseme hilo likae kwenye rekodi, kwa sababu yeye pamoja na Naibu wake, wamejibu kwa ukweli na vizuri na hili ndilo tunalotaka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu pia kwa tukio la jana, napenda kuwashukuru sana Kamati yetu ya Tafrija, ilifanya mambo mazuri sana kwa mpangilio mzuri. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alifurahi sana na nitoe shukrani maalum kwa wale wanamitindo, ilikuwa vigumu sana kama mtu huelewi sura zao, ilikuwa ni rahisi kuamini kwamba, hawa ni Wanamitindo wa Kimataifa kumbe ni Wabunge. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo inanifikisha kutangaza jambo lingine la leo; leo kuna mechi za netball na soka, baina ya timu zetu na Timu ya Tanzania Breweries. Shughuli zitaanza saa tisa pale Uwanja wa Jamhuri na baada ya shughuli zote kukamilika, saa mbili usiku kwenye Ukumbi wetu ule ule kutakuwa na burudani itakayotumbuizwa na bendi ya Ngwasuma; sijui maana yake nini lakini kwa akina Rosemary Kirigini na Mercy Emmanuel nadhani wanatambua hii kitu ni nini. Kwa hiyo, mnakaribishwa. Mgeni rasmi atakuwa Mama Tunu Pinda, kuanzia saa mbili. Viburudisho vyote vitakuwepo kuanzia vinywaji na vitafunwa. Kwa hiyo, baada ya hizo mechi, hiyo ndiyo shughuli itakayofanyika saa za jioni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo la faraja lipo la kuchangia sasa; Kamati ya Uongozi tulipoketi kuna mchango unaoendelea wa kusaidia kuwanunulia vifaa walemavu wa aina mbalimbali katika nchi yetu. Sisi Bunge tulikuwa hatujachangia, mchango huu unapelekwa kwa *Tanzania Education Authorithy* ili kuwanunulia vitu mbalimbali; kwa mfano, wasioona wapate vifaa vitakavyowawezesha kufuatilia hotuba na kadhalika, lakini siyo tu Wabunge ni pamoja na jamii kule.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tumekubaliana kwamba, sisi Wabunge tutachangia shilingi elfu ishirini kila mmoja na hiyo itatupa takriban shilingi milioni sita. Katibu amenieleza hapa kwamba, Ofisi itachangia kiasi cha shilingi milioni nne; kwa hiyo, ukichanganya za Ofisi na zetu Wabunge tutaweza kufikisha *TEA* kiasi cha shilingi milioni kumi, kuwaunga mkono walemavu wa nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, nawatakia *weekend* njema na sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi Jumatatu ijayo, saa tatu asubuhi katika Ukumbi huu.

*(Saa 6.17 Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 13 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*